ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nane - Tarehe 25 Juni, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 102

Tatizo la Msongamano katika Huduma za *PBZ*

Mhe. Saleh Nassor Juma- Aliuliza**:-**

Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) ndio benki pekee iliyoanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa lengo la kutoa huduma za kibenki kwa Wanzanzibari wote, na kwa kuwa hadi leo hii ile dhamira ya Benki hii ya kuimarisha mazingira ya kutoa huduma za kibenki kwa wakati muafaka na ufanisi hadi leo hii haijafanikiwa, kwani kunakuwa na mrundikano mkubwa wa wateja pale wanapotaka kuchukua mishahara yao katika kipindi cha mwisho wa mwezi; jambo ambalo linaleta usumbufu sio tu kwa wateja lakini hata kwa wafanyakazi wa Benki hiyo.

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo.

(b) Kama Serikali inalifahamu tatizo hilo ni hatua gani zimechukuliwa ili kuondosha usumbufu huo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:-Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma suala lake lenye a,b na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali inalifahamu tatizo la mrundikano wa wateja hasa siku za mwisho wa mwezi ambapo wateja wengi wa *BPZ* huenda Benki kwa ajili ya kuchukua mishahara yao.

(b) Mhe. Mwenyekiti, Serikali baada ya kubaini tatizo hili imechukua hatua za kuitaka Benki ya Watu wa Zanzibar kuimarishaa huduma zake kwa kufungua matawi Mikoani pamoja na kuweka huduma mbadala za kutumia *ATM* na *SMS Banking*. Ili wateja waweze kutoa pesa zao kwa Mashine za *ATM* na katika ya huduma za *M-Pesa*, *Ezy-Pesa*, *Tigo-Pesa* na *Airtel Money*. Aidha utumiaji wa *SMS banking* utamuwezesha mteja kuweka na kuchukua fedha zake benki kwa kutumia *SMS* bila ya yeye mwenyewe kwenda benki.

Mhe. Mwenyekiti, napande kulijuilisha Baraza lako tukufu kuwa *PBZ* pia imo katika mtandao wa Umoja Benki ambao unajumuisha benki 24, mwanachama wa *BPZ* anaweza kutoa fedha zake kwa kutumia *ATM* yoyote ya benki hizo. Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuliarifu Baraza lako Tukufu pamoja na wananchi kuwa *PBZ* tayari imeshafungua matawi huko Wete na Mkoani Pemba pamoja na Makunduchi, pia imeongeza Mashine za *ATM* na kuziweka katika maeneo mbali mbali. Kwa upande wa *SMS* benki huduma hii inatarajiwa kuanza mwezi wa Julai mwaka 2013.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo niulize swali dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hizi Mashine za *ATM* hivi sasa tunapata wasi wasi kwamba kuna tatizo la kuchukuliwa kwa fedha za baadhi ya wateja kupitia mashine hizi, huu ni wizi na kwa kuwa Mhe. Waziri umejibu kwamba mbali na mambo hayo ya *ATM* unataka kuanzisha na *Ezy-Pesa*, ilimradi mambo haya ya *SMS*.

(a) Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mmeshafanya sana *feasibility study* mkaona kwamba katika utaratibu huu wa kutumia mambo ya *Ezy-Pesa* na *SMS* hizi fedha za wateja wa *PBZ* hazitaibiwa kama ambavyo sasa hili tatizo la kimataifa kuibia fedha mmeshafanya kujua hilo.

(b) Kwa kuwa mna *install ATM- Machine* sana katika maeneo ya Mjini na kuacha maeneo ya shamba yakiendelea kuhangaika. Je, ni lini hizi mashine nazo mtazipeleka katika maeneo ya vijijini kama vile Vitongoji Umangani, Vitongoji Uwandani, Vitongoji Kibokoni na kadhalika.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:- Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Saleh Nassor Juma, huyu ni baba yangu nataka nimpongeze sana kwa maswali yake.

Lakini vile vile mara nyingi akizungumza huwa huumsikii kwa sababu ya nguvu zake Mwanamapinduzi huyu. Lakini leo nimemsikia vizuri na mimi nataka nimjibu maswali yake mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Utafiti wa kina umefanyika na huwezi ukapewa kibali na Benki Kuu kama hujafanya utafiti wa kina. Hiyo imefanyika na nashukuru jana mchana tu nilikuwa na viongozi wa *PBZ* wamenithibitishia hivyo, na tayari wanasubiri kibali tu kutoka *BOT* wameshaambiwa kuwa kibali kitapatikana cha kuanza utaratibu huu wa kutumia *Mobile Banking*.

(b) Alitaka kujua ni lini tutazipeleka hizo mashine za *ATM* huko vijijini. Nilikuwa nikisema kwamba mashine hizi zinaweza kuwekwa hapa popote pale inategemea na hali ya usalama na soko la pale pahala. Ametaja maeneo ya Vitongoji basi nitawashauri sana wenzangu wakayaangalie maeneo ya Vitongoji na maeneo mengine ya vijijini kama kuna soko watu wengi wameweka pesa kupitia benki na hizi mashine iwekwe ili kuweza kusaidia wasipate matatizo.

Nimeeleza katika kipindi fulani kwamba tunatarajia kuweka mashine kule Tunguu. Hili ni katika utaratibu huo huo kuhakikisha kama kuna soko kwa maana watu walioko kule wengi wameweka pesa zao benki. Basi mashine hizo zinaweza kuwekwa bila ya matatizo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Benki ya Watu wa Zanzibar ndio benki pekee tuliyonayo hapa kwa Wazanzibari na ninavyokumbuka siku za nyuma ilikuwa ikitoa huduma zake kwa ufanisi mzuri na ilikuwa na majumba yake Wete, Mkoani. Lakini kilitokea kipindi majumba yale yakafungwa watu wakastaafishwa ikabakia Chake Chake peke yake kwa Pemba na kwa Unguja ni matawi mawili tu.

Je, kulikuwa na kitu gani mpaka ikasababisha vile leo hali ile ile ikarudi ikawa Benki ya Watu wa Zanzibar sasa inakodi majumba ambayo wenyewe wameyauza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kipindi kile Benki ya Watu wa Zanzibar ilikuwa inafanya vibaya na ilikuwa inapewa leseni na *BOT* ya kufanya biashara ya Benki kwa miezi mitatu mitatu. Na kama hatukuchukua *reform* hivi sasa tungekuwa hatuna Benki ya Watu wa Zanzibar. Tukalazimika kupunguza baadhi ya wafanyakazi, kufunga baadhi ya vituo, tukalazimika kuipeleka kwenye *Automation* baada ya *Manual*.

Hiki kitu kilitusaidia sana na sasa benki inafanya vizuri mahitaji yameanza kuongezeka kwa sababu mahitaji yameanza kuongezeka, kwa sababu wateja wengi wanaweka pesa zao benki ndio tumeirudisha tena. Jengo la Wete tayari tumeshafungua jengo la Mkoani tayari tumeshafungua na Makunduchi sasa hivi inafanya kazi na Ijumaa inazinduliwa.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa *PBZ* walikuwa wana matatizo makubwa ya miundombinu ya majengo hasa Pemba. Lakini kwa sasa Pemba pale maeneo ya Chake Chake kuna jengo zuri kubwa ambalo linakidhi haja. Lakini kwa sababu wanatumia sehemu moja katika kutoa huduma zao.

Je, Mhe. Waziri hii ni kwa sababu hawana wafanyakazi wa kueneza katika vile vidirisha vyao kutoa huduma kwa uzuri au ni vipi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo:- Mhe. Mwenyekiti, hilo tatizo ambalo amelieleza Mhe. Bikame Yussuf Hamad sijawahi kuliandika pale Pemba. Lakini kwa sababu tu amelieleza namuomba anipe na mimi nafasi nifanye safari kwenda Pemba nikaliangalie hilo tatizo na baadae tuweze kuongeza hizo huduma. Kwa sababu kama alivyosema kweli jengo la Chake Chake ni kubwa na ni zuri, hivyo inapaswa tulitumie ili *value for money* iweze kuonekana. Na mimi namshukuru sana Mheshimiwa kwa kunishtua hili.

Nam. 113

Takwimu za Mapato Yanayotokana na Nishati ya Mafuta

Mhe. Mohammed Haji Khalid- Aliuliza**:-**

Njia moja wapo ya kukusanya mapato ya Wizara hii ni kupitia bidhaa ya mafuta (petroli, dizeli na mafuta ya taa) inayokusanywa na Mfuko wa Barabara. Inasemekana kuwa kila lita moja ya bidhaa hii inayouzwa Serikali inachukua Shilingi mia moja (shs. 100/-).

(a) Je, ni kweli kuwa Serikali inachukua shs. 100/- kwa kila lita inayouzwa ya bidhaa hii.

(b) Kama ni kweli kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na 2012/2013 Mfuko umekusanya Shilingi ngapi.

(c) Ni barabara ngapi na zipi zilizojengwa Unguja na Pemba kwa kipindi hicho kupitia fedha hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa kabla ya kujibu swali la Mhe. Moh'd Haji Khalid lenye kifungu a, b na c naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ilianzisha mfuko wa Barabara kwa sheria namba 2 ya mwaka 2001 na kufanyiwa marekebisho mwaka 2008. Mfuko huo ulianzishwa kama hatua maalum za kuweka utaratibu endelevu wa upatikanaji wa fedha kupitia uuzaji wa mafuta ya petroli na dizeli kwa ajili ya matengenezo ya barabara.

Lengo la mfuko ni kuhakikisha kuwa barabara zilizojengwa kwa gharama kubwa matengenezo yake yanakuwa endelevu. Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo haya mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatozwa shilingi mia moja kwa lita ya petroli na dizeli inayouzwa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mfuko wa barabara umekusanya fedha zake kama ifuatavyo.

Kwanza mwaka 2011/2012 shilingi bilioni sita milioni mia nne na thalathini na mbili. Mwaka 2012/2013 hadi tarehe 20 Juni mfuko wa barabara umekusanya shilingi bilioni sita mia moja na ishirini na mbili milioni hamsini na nane elfu na shilingi mia mbili.

(c) Mhe. Mwenyekiti, dhana ya mfuko ni matengenezo na sio ujenzi. Kwa maana hiyo barabara zilizofanyiwa matengenezo hizi zifuatazo:-

Mwaka 2011/2012 kwa Unguja: Kikwajuni- Madema, Mfenesini Polisi hadi Kihinani. Fuoni- Tunguu, Malindi - Kinazini, Kwamchina mwanzo- Nyumba mbili, Soko la Mchina- Mbuyu Mnene, Mwanakwerekwe- Nyumba mbili, Fuoni - Jitimai, Kiashangwe- Muyuni, Hanyegwamchana- Chuchumile, Mashine ya Maji- Nyarugusu. Uwekaji wa alama za barabarani upakaji wa rangi barabarani pamoja na ujenzi wa *culvert* Kitundu Ndagaa. Pamoja na ufukuaji wa misingi kwa barabara ya Bububu Mahonda.

Mhe. Mwenyekiti, barabara zilizotengenezwa kwa mwaka 2011/2012 kwa Pemba ni Mpuguani- Kironi, Chake Chake - Ikulu, Weni - Wete, Wesha - Mkumbuu, Wawi- Mgogoni.

Ujenzi wa Mitaro: Ole- Konde, Sizini -Weni, Wete - Chake Chake na Timbirinzi. Uwekaji wa lami barabarani pamoja na upakaji wa rangi barabarani kwa barabara ya Chake Chake Mkoani.

Barabara zilizojengwa kwa mwaka 2012/2013 kwa Unguja ni hizi: Mkunazini - Kikwajuni- Madema- Chukwani, Buyu - Tunguu, Nyambiza- Mazizini- Vitambulisho.

Ufufuaji wa Mitaro Bububu, ujenzi wa Mitaro Kilimani- Magereza, Kilimani - Migombani.

Aidha kazi za matengenezo bado zinaendelea kwa barabara ya Amani- Mtoni kwa kutumia kifungu cha mchago wa mifuko wa miradi ya barabara zinazotolewa na SMZ.

Junction Mchina Mwanzo- Upenja, Kiwengwa - Kivunge, Mkokotoni- Sharifu Msa, Bububu- Mfenesini, Kama KMKM- Mkwajuni na Mshelishelini.

Kwa barabara za Pemba mwaka 2012/2013, Chake Chake - *Street*, Finya- Kicha, Ole-Vitongoji, Shindi- Mwambani, Mkuyu- Kiuyu, Mti Juu- Maziwani. U jenzi wa barabara za Kicha na Pujini pamoja na ujenzi wa *culvert* kwa Shangafu na Mtambile. Uwekaji wa umeme Kware na Vitongoji.

Aidha barabara za Macho manne, Meli tano na Chake Chake Wesha zinaendelea na matengezo. Vile vile daraja la Mkia wa Ngo'mbe linaendelea kujengwa.

Mhe. Mwenyekiti, samahani sana kama majina nilivyoyataja nimetamka sivyo kwa wale ambao wametoka katika maeneo hayo naomba mnisamahe.

Mhe Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakushuruku ili kuweka sawa nimeomba nitoe maelezo yafuatayo kutokana na majibu aliyoyatoa Mhe. Waziri.

Ni dhahiri kwamba Mfuko wa barabara kama alivyotaja ni sahihi barabara hizo isipokuwa utaratibu ni kwamba sisi wizara yetu inaingia mkataba maalum na mfuko wa barabara kupitia Idara ya Ujenzi na utunzaji wa Barabara *UUB* kujenga barabara hizo.

Kwa hivyo, wanaotoa fedha ni mfuko wa barabara watekelezaji wa shughuli hiyo ni *UUB*. Kwa hivyo, pasijeonekana kwamba Wizara ya Fedha ndio inayojenga barabara na pakawa na masuala zaidi. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Moh'd Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri pamoja na yale ya nyongeza yale ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Kwa kuwa mfumo huu kazi yake ni kufanya ukarabati wala si kujenga na fedha zilizokusanywa hizo fedha ni nyingi. Je, fedha hizi zote zimetumika na kiasi gani kilichobakia.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Miundombinu, Idara ya Miundombinu, Idara ya Barabara na Mfuko wa barabara huwa unawekeana mikataba ambayo inapaswa kufanyiwa matengenezo.

Kikawaida ukiachia mbali zile pesa ambazo zimekwenda katika Utawala ambazo mara nyingi inakuwa haizidi bilioni moja na nusu fedha zote zilizobakia zinakwenda katika matumizi ya matengenzo ya barabara.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri.

Mhe. Waziri naomba unisahihishe Kiswahili cha mfuko huu. Mfuko huu madhumuni yake ni kutengeneza au kujenga. Kama ni kujenga itakuwaje leo mfuko huu ukatengeneze Barabara ya Mkapa *road*. Wakati barabara ya Mkapa *road* Amani hiyo mwaka jana fedha zake zilikuwepo na mkasema Serikali imeziazima tu halafu mtazirejesha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ukisoma sheria ya mfuko huu kazi zake ni matengenezo si ujenzi. Lakini kwa makubaliano na Serikali na kwa kiwango maalum mfuko huu unaweza kutumia sehemu ya fedha zake kwa kujenga barabara. Lakini kiutaratibu sisi hatupendelei zitumike kwa ujenzi, lakini inapotokea dharura kama barabara ya Mtoni - Amani, na vile vile Mhe. Makame Mshimba alisema kwamba barabara ile ilikuwa na pesa zake. Zile pesa zake

zilizokuwepo zilitumika na zikamalizika na mahitaji ya barabara bado yanahitajia fedha nyingi zaidi.

Nam. 40

Tatizo la Kutuama kwa Maji Katika Uwanda wa Ndege

Mhe. Salim Abdalla Hamad- Aliuliza**:-**

Serikali imetumia fedha nyingi kwa matengenezo ya sehemu ya barabara inayotuama maji katika eneo la Kiembe Samaki kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Zanzibar.

(a) Ni kiasi gani cha fedha zilizotumika kwa kazi hiyo.

(b) Ni akina nani waliokabidhiwa kazi hiyo

(c) Ni sababu zipi zilizosababisha maji kutuama katika barabara hiyo na ni hatua gani zinazochukuliwa kudhibiti hali hiyo

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano- Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla sijajibu swali la Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Barabara ya Mnazi Mmoja kupitia Kiembesamaki hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ni miongoni mwa barabara muhimu sana hapa nchini inayotumiwa na viongozi wa Kitaifa na Kimataifa wanaoingia na kutoka nchini kupitia Uwanja wa Ndege huo. Hivyo, barabara hiyo ni kama kioo cha nchi hasa kwa wageni wanaokuja nchini.

Barabara hiyo iliyojengwa kwenye miaka ya 70 na Kampuni ya *MOLEM* ambayo haikujengewa mitaro ya maji kwa vile wakati huo maji yalikuwa yakitawanyika kwenye sehemu za wazi pembezoni mwa barabara ambayo yalikuwa hamjajengwa majengo kama yaliyomo hivi sasa na kwa sababu hiyo hapakuwa na suala la maji kutuama barabarani muda wote wa mvua za vuli na masika.

Mnamo miaka ya 90 ujenzi usiozingatia mipango miji, maeneo mbali mbali yaliyokuwa wazi yalianza kujengwa ikiwa pamoja na sehemu zilizokuwa

yakikaa maji yaliyotoka barabarani. Athari ya kutuama maji sehemu aliyoitaja Mhe. Mjumbe ilianza kwenye miaka ya 2000 na kusababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa barabara hiyo kutokana na kuwa hapakuwa na mbadala wa njia ya maji hayo kwenda baada ya maeneo yote kujengwa nyumba za makaazi, na hivyo kusababisha maji hayo kukaa barabarani kwa siku nyingi hadi kugeuka rangi na wakati mwengine kuilazimu Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Manispaa kulazimika kutumia gari la kunyonya maji hayo ili kuyaondoa barabarani.

Mnamo mwaka 2008/2009 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iliamua kutafuta namna ya kuondoa maji mahali hapo na ndipo ilipoomba kiasi cha Tshs. 300, 000,000 kwa ajili ya kujenga mtaro ambao utakaounganishwa na ule wa Uwanja wa Ndege.

Utekelezaji wa ujenzi huo alianza kwa kuchimba upande mmoja na kujengewa kwa mawe na saruji kiasi cha mita 700 kuanzia Mkunazi wa Kwanza mpaka Uwanja wa Ndege ambayo jumla ya Tshs. 89, 255,000 zilitumika kwa kazi ya ujenzi wa mtaro huo. Kujengwa kwa mtaro huo umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ukaaji wa maji barabarani kwani hivi sasa inachukua muda mdogo tu maji kukaa baada ya mvua kumalizika.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Jumla ya Tshs. 89, 255,000.00 zilitumika kwa kazi za ujenzi wa mtaro huo.

(b) Wafanyakazi wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara ndio waliokabidhiwa kazi hiyo.

(c) Mhe. Mwenyekiti, sababu zilizosababisha kutuama kwa maji kwenye barabara hiyo ni kutokana na kukosa sehemu ya kwenda baada ya sehemu zake za asili kujengwa na wananchi bila kuzingatia mipango miji.

Mhe Salum Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri kwa swali hili.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyofahamu ile sehemu zaidi ya kazi aliyoitaja Mhe. Waziri palikuwa pakitengenezwa kwa maana ya kutengezwa hasa kwa kujazwa sehemu hii na hii ili yale maji yasituwame.
Lakini sehemu ile ya juu afadhali lakini sehemu ya krosi pale Uwanja wa Ndege kuelekea katika Baraza la Wawakilishi. Ikiwa lengo ni kuweka usafi ili

barabara hii muhimu iweze kutumika vizuri na hasa kwa sababu wanatumia watalii wengi sana haoni kuwa iko haja ya kujaza zile sehemu ambazo zinatumiwa kwa wingi na wakati mitaro imeshajengwa ili maji yale yasiendelee kutuama kwa wingi namna ile.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano:- Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana sana na Mhe. Mwakilishi kwa sababu kama ambavyo sote tunakuja huku tunaitumia njia ile siku zote karibu. Kwa hivyo, nnaijua wakati wa jua nnaijua wakati wa mvua.

Na kwa taarifa mimi nimeshazungumza na Mkurugenzi kumueleza maeneo hayo hayo ambayo ameyataja yeye ambayo yanatuama maji na tayari analishughulikia hilo suala ama kuchimbua misingi upande wa mkono wa kushoto kama ukitokea Uwanja wa ndege, kuanzia kwenye kituo cha daladala na kuelekea mbele au kufanya mjazo kama alivyosema yeye. Kwa hivyo, wataalamu wanalishughulikia sasa hivi ili tuone kwamba kuna njia ya kuchimba mtaro kuanzia kituo cha daladala cha Uwanja wa ndege na kujia mjini mpaka karibu na eneo la Msikiti wa pili ambapo tayari mtaro upo na umeshajengwa. Kwa hivyo, eneo hilo nalijua na tayari nimeshalitolea maelekezo ili wataalamu walifanyie kazi na kuona nini kitafanywa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mhe. Waziri alisema walihitaji shilingi milioni 800 kuweza kukamilisha suala lile la ujenzi wa mitaro. Lakini katuambia kwamba wametumia chini ya hapo, yaani wametumia shilingi milioni 83, kuanzia Mkunazini mpaka sehemu gani ambapo ujenzi takriban haukumalizika na ndio sababu ambayo imepelekea maji kuendelea kutuama katika eneo lile. Sasa Mhe. Waziri anaweza kunieleza tu kuwa;

(a) Je, ile kazi ambayo mmefanya ni asilimia ngapi ya kazi yote.
(b) Hizi milioni 800 hamkupewa, mmepewa milioni 83 kufanyia hiyo kazi. Je, ni kweli kuwa hamkupewa au ni kutokana na ubakhili wa serikali hii iliopo madarakani na khiyana kuwa msipewe hizo zilizobakia, au ni kutokana na wizara yake haiko makini tu katika kufuatilia haya mambo.
(c) Kwa kuwa yeye mwenyewe amesema kwamba barabara zile ni muhimu kwa taifa na kimataifa, na kwa kuwa keshokutwa hapa tukijaaliwa Rais Barack Obama anakuja Tanzania, napata wasi wasi kwamba atakapofika Tanzania huyu mtu ataamua kutembelea Zanzibar na atateremka katika uwanja wa ndege wa Karume Airport. Je, wakati akiteremka ikiwa maji yamezonga pale, haitakuwa aibu kwa nchi yetu hii, hapo sasa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Kwanza naomba aweze kurudi nyuma wakati nilipokuwa najibu kwamba kazi ilifanywa mwaka 2008/2009. Lakini ni imani ya wakati ule kwamba shughuli ile iliyofanywa ingetosheleza kuyapeleka maji yote sehemu ambayo yanatakiwa. Lakini tatizo lililojitokeza sasa hivi ni sehemu ya upande wa pili wa njia ambayo iko mkono wa kushoto ukitokea Uwanja wa ndege wa kimataifa.

Lakini la pili kama nilivyosema kwamba wakati ulipokuwa unachimbuliwa huu mtaro, nyumba zilikuwa tayari zimeshajengwa. Kwa hivyo, kwa njia yoyote ile ule utaratibu wake lazima ilikuwa uendane sawa na zile nyumba ambazo zipo, tofauti ya kuchimba mtaro kwa kuelekeza kule unakotaka kwa vipimo vya kitaalamu. Kwa hivyo, suala lililobaki nimesema mwanzo kwamba mimi nimeshaliona na linashughulikiwa kitaalamu, ili tutakapokuja kufanya kazi iwe zile fedha zimetumika kiuhakika na kwa ajili ya kuondoa lile tatizo bila ya kurudi tena nyuma.

Kwa ufupi, kama ulikuwa upo katika mwaka 2008/2009 maji yaliyokuwa yakituama wakati huo sio yale yanayotuama sasa. Kwa hivyo, ni suala ambalo limefanikiwa, lakini halikufanikiwa kwa asilimia mia moja. Naamini kwa mikakati tuliyonayo baada ya kuangalia vipimo vyetu na wataalamu wakatoa ushauri wao, kazi tutakayoifanya itaweza kukamilisha suala hilo na hapatakuwa na tatizo jengine lolote na kwa sababu mvua hakuna, nafikiri akija Rais Obama hatoona maji, labda yawe mule. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kakiri kwamba baada ya matengenezo yale maji yaliyokuwa yakituama ya zamani sipo yanapotuama maji yaliopo sasa hivi. Sasa kwa sababu wameondoa huku halafu yamekuja sehemu nyengine na wakati wanakusudia kutengeneza tena.

Je, hawaoni wakiyaondoa pale watayapeleka pahala pengine, kwa sababu yale maji atakubaliana na mimi kama yale maji kutuama ni kwa sababu ya hayana njia ya kwenda moja kwa moja baharini, kwa sababu hayana njia ya kwenda moja kwa moja baharini ndio maana yanaondoka hapa na kuja hapa. Je, haoni kuwa iko haja ya kuchimba mtaro mkubwa ili yale maji yakaondolewa moja kwa moja na kupelekwa baharini, kuliko kuyaondoa hapa na kuyapeleka sehemu nyengine. Pia atakubaliana na mimi kwamba kwa yale maji ule mtaro uliopo sasa hivi ni mdogo sana na yale maji hayana njia nyengine ya kupita sasa yanasogea sogea tu pale.

Kwa hivyo, je jitihada yake itafika vipi ili kuona kuwa yale maji anayapeleka baharini.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni sahihi maji yanapotolewa sehemu moja ni lazima yapate pahala pa kuelekea. Lakini niseme kwamba hii sehemu ya pili ya utekelezaji wa huu mradi tumeshawakabidhi wataalamu waifanyie kazi. Kama yataunganishwa na yale ya mwanzo yanakokwenda ambapo yalikuwa yanapelekwa katika mtaro mkuu wa uwanja wa ndege. Ule mtaro mkuu wa uwanja wa ndege wenyewe umeshaelekezwa pahala yanakopelekwa maji. Kwa hivyo, kama itafanikiwa hiyo basi itaendelea hiyo, na kama haukufanikiwa utaalamu huo, basi wataalamu watatuelekeza ni nini cha kufanya ili maji yale tusije tukayatoa na kuyapeleka sehemu nyengine yakaenda yakatuama, yakaondoka njiani lakini yakaenda kutuama pengine. Kazi hiyo ni ya kitaalamu na ninamuomba Mhe. Mwakilishi avumilie ili wataalamu wafanye shughuli yao na baadae kuja na jibu ambalo ni muafaka kabisa, ahsante sana.

Nam. 37

Kuwasaidia Wananchi Katika Vikundi vya Ushirika

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Ni jambo la kufurahisha sana kuona serikali inafanya juhudi za makusudi katika kuinua hali za wananchi kiuchumi na kuwajengea misingi imara ya kimaendeleo. Miongoni mwa juhudi hizo ni kuwasaidia kupitia vikundi vya ushirika, Mjini na Vijijini.

(a) Je, ni vikundi vingapi kwa mwaka hunufaika na misaada ya kimaendeleo.
(b) Je, kuna asilimia ngapi zinazoonesha ongezeko la kipato cha wananchi na kupungua umaskini mijini na vijijini.
(c) Je, kuna ufuatiliaji wa tathmini unaofanywa ndani ya vikundi husika kuthibitisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 37 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, idadi ya vikundi vilivyofaidika na misaada ya kimaendeleo. Jibu ni kwamba;

Ni kweli serikali inafanya juhudi za makusudi katika kuinua hali za wananchi kiuchumi na kuwajengea misingi imara ya kuwaletea maendeleo.

Misaada ya kimaendeleo inatolewa kwenye vyama vya ushirika kupitia wizara yangu, ni pamoja na upekuzi wa shughuli za vyama na ushauri wa kitaalamu, mafunzo kazini. Ukaguzi wa hesabu za vyama, mafunzo ya uongozi na uendeshaji wa vyama hivyo.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Vyama vilivyofaidika kupitia huduma mbali mbali ni kama ifuatavyo. Vyama 186 vimefanyiwa ukaguzi wa hesabu zao. Jumla ya vyama 1102 vimefanyiwa upekuzi wa vitabu vyao vya hesabu ili kuangalia shughuli wanazozifanya na namna wanavyofuata katika vyama vyao na kupewa ushauri wa kitaalamu juu ya kurekebisha kasoro hizo. Jumla ya vyama 38 vimesaidiwa kuandaa mipango ya kibiashara ili waweze kuitumia katika kutafuta mikopo ya kuendeleza shughuli zao.

Mafunzo juu ya uongozi, utawala bora na uendeshaji wa vyama yametolewa kwa washiriki 40 wa vyama vikuu vya ushirika na shirikisho la vyama vya ushirika Zanzibar, yaani KUZA. Aidha, jumla ya wanachama 3407 wa vyama vya ushirika 343 wamepatiwa mafunzo juu ya haki na wajibu wao.

Mhe. Mwenyekiti utafiti juu ya ongezeko la kipato cha wananchi na kupungua kwa umaskini Mijini na Vijijini, kimsingi ni jukumu la wizara inayohusika na masuala ya fedha pamoja na takwimu. Ili kupata majibu sahihi ya hali ya ongezeko la kipato kwa wananchi kupitia shughuli za uwezeshaji zinazofanywa na wizara yangu, tutawasiliana na wizara husika kuingiza maswali au viashiria hivyo, katika tafiti za matumizi ya kaya.

Hata hivyo, utafiti wa matumizi ya kaya uliofanywa mwaka 2009/2010, inaonesha kwamba kiwango cha watu wanaoishi chini ya mstari wa umaskini kimepungua, kutoka asilimia 49.1 mwaka 2005 hadi asilimia 44.4 mwaka 2010.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wizara yangu imefanya ufuatiliaji, ukaguzi na kutathmini shughuli zinazofanywa na wananchi hasa kwenye vyama vya ushirika. Ukaguzi huu umefanywa kwa lengo la kutambua hali halisi ya kifedha ya vyama vyao. Hivyo, pamoja na uendeshaji wa miradi yake. Matokeo ya upekuzi na ukaguzi hizo kiujumla yameonesha ongezeko la ukuaji wa rasilimali kwa baadhi ya vyama, ingawa bado elimu zaidi inahitajika ili kuimarisha utendaji na udhibiti wa rasilimali hizo, pamoja na kuleta tija kwenye vyama vya ushirika. Hata hivyo, bado vyama vingi havijawa na uwezo wa kuzalisha bidhaa bora zinazoweza kuhimili ushindani wa soko.

Wizara imezifanyia kazi changamoto hizi ili vyama vya ushirika viweze kuwakomboa wanachama wake kutoka katika wimbi la umaskini.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, utakubaliana na mimi katika kutoa pesa hizi za kusaidia vikundi vya ushirika katika ukumbi wa Benjamin Mkapa, kulikuwa na matatizo makubwa, waliokusudiwa kupata na wengine hawakupata na mzozo ukatokea.

a) Je, wizara yako imejipanga vipi ili mambo yale yasitokee tena.
b) Mhe. Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika ukumbi huu tulishuhudia na Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu pale katika kugawa pesa hizi, kuna wengine walipata kidogo na wengine wakapata kikubwa.

Kwa mfano, wengine walipata shilingi milioni 1.5, wengine milioni 2 na wengine mpaka milioni 3 mpaka milioni 5. Je kuna utaratibu gani wengine kupata kidogo na wengine kupata kingi, tunaomba kujua.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nitoe maelezo yafuatayo kabla sijajibu maswali yake. Wakati tunagawa fedha zile ingawa sio suala la msingi limeulizwa, lakini nitalijibu tu kwa faida ya Waheshimiwa. Kwa sababu swali la msingi lilikuwa ni kuhusu vyama vya ushirika na kazi zinazofanywa na utafiti unavyofuatiliwa, lakini ugawaji wa fedha zile zimeonekana dhahiri kwamba ziligubikwa na hali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, walichukulia kwamba wao ndio waliosimamia suala lile katika majimbo yao. Hivyo, kutaka wao lazima jambo lile walisimamie wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yangu kama Waziri ninayehusika na mambo ya uwezeshaji, nilipowashauri Waheshimiwa Wajumbe waniletee idadi ya vyama vyao vya ushirika vyote kwa Baraza hili, ili nitizame uwezekano wa kusaidia katika kila Jimbo angalau vikundi viwili au vitatu. Kwa bahati mbaya sana wengi walioleta vikundi vile ama vilivyokuwa havijasajiliwa au vililetwa vimesajiliwa lakini vimechelewa kuletwa na kuwasilishwa pale ofisini kwetu.

Kwa imani kubwa Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuchelewa huko, nikafanya bidii basi kwa kila Jimbo angalau vikundi viwili au vitatu vipatiwe pesa zile. Pale ambapo pesa zilipungua au zilionekana kidogo ni kutokana na sababu hiyo, tulimpunguza mtu ambaye alipata pengine milioni 3, tukampatia mwengine milioni 1.5 ili na yeye afaidike katika eneo lake. Kwa hivyo,

kwanza Waheshimiwa Wajumbe lile walione kuwa serikali imefanya jambo la maana na kushukuru.

Lakini kwa masikitiko makubwa, nasikitika sana kwamba wakati nikitoa fedha hizi katika maeneo mengine, Waheshimiwa Wawakilishi walikuja juu na kuvamia pale kiasi ambacho kama nilifanya dhambi kubwa ya kwenda kutoa pesa zile kwenye maeneo yale. Hata hivyo, nimejipanga kwamba makosa kama yale hayatotokezea tena. Sisemi sitowashirikisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, lakini nitashauriana nao katika maeneo yao kwamba ni vikundi vipi tuvipatie misaada ile.

Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa kuna malalamiko mengi, nakubali. Lakini kazi ile ya kufuatilia vikundi vile haikufanywa na wizara yangu, pesa zile ni za kidini kwa kupitia mfuko wa ZAKA, watu wa Wakfu na Mali ya Amana walitembelea wakatathmini. Haiwezekani mtu ambaye ana mali ya shilingi milioni 20 ukampa shilingi milioni 1 na yule ambaye ana kuku 200 ukampa shilingi milioni 1, lazima kutatofautiana, inategemeana na mradi uliokuwepo katika eneo lile. Kwa hivyo, tumejipanga vizuri na *Inshaallah* hatutegemei jambo kama hili kutokezea tena.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakumbuka kwamba yeye mwenyewe aliwaomba Wawakilishi wapeleke vikundi viwili ndani ya Jimbo lake na wamkabidhi mkononi barua ya vikundi hivyo. Sisi kwa kufuata agizo hilo tulikwenda ofisini kwake tukapeleka vikundi hivyo mkononi. Lakini kwenye ugawaji wa fedha sasa, vikundi ambavyo Wawakilishi walivipeleka kwa barua rasmi, sivyo ambavyo vilipewa fedha katika wilaya za Pemba na ndio chanzo cha kufanya vurugu. Waziri alipokea vikundi kutoka kwetu, lakini wakuu wa wilaya na maafisa wake wakapeleka fedha katika vikundi vingine, hicho ndio chanzo cha zogo hilo.

a) Swali langu. Je, Mhe. Waziri anakubaliana na mimi kwamba agizo lake lilikiukwa na Wakuu wa wilaya na maafisa wake.

b) Kama hilo ni tatizo, mara hii anatuambia nini Wawakilishi juu ya udhaifu huo ambao ulitokezea.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimthibitishie Mhe. Hija Hassan Hija kwamba zoezi lile halikuvurugwa na Wakuu wa wilaya wala Wakuu wa mikoa. Kulitokea tatizo katika Wila ya Mkoani, tatizo hili lilisababishwa na afisa anayehusika na

vyama vya ushirika na kwa bahati mbaya sana na nilimkemea pale pale wilayani wakati nikitoa fedha zile, kwamba orodha ambayo Wakfu na Mali ya Amana walipeleka kwa kushirikiana na sisi na yeye pengine kwa ushabiki wake akaongeza kikundi chake kimoja. Lakini hakuna kikundi ambacho kilitolewa, lakini ile ni awamu ya kwanza tu Waheshimiwa. Nawahakikishieni kwamba *Inshaallah* tutajitahidi katika awamu hii inayokuja baada ya mwezi mtukufu wa Ramadhani Mhe. Hija Hassan na Wajumbe wengine wote, basi na wao vikundi vya maeneo yao vitafaidika. Lakini tuchukulie tu kitu kimoja na tuelewe kwamba hazitolewi fedha hizi kwa sababu ya kutaka kumridhisha kila Mwakilishi katika jimbo lake. Tunatoa fedha hizi kutokana na vikundi vya ushirika vilivyohamasika na vilivyosajiliwa na ambavyo vinazalisha, kwa sababu kuna vikundi ambavyo huko majimboni vipo tu, lakini wakisikia pesa wanakuja.

Kwa hivyo, nawaombeni Waheshimiwa Wawakilishi tuwe karibu na vikundi vya ushirika, ili tuzidi kuwahamasisha na *Inshaallah* serikali hii imejipanga vizuri, tutachukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha vikundi vyote vinavyohusika vinapatiwa msaada. Mhe. Hija Hassan Hija nakiri kwamba kweli alikuja ofisini kwangu, lakini ndio vile vya lala salama tena.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe musiwe na wasi wasi *Inshaallah* tukija kutoa taarifa, najua mapema watakuja na tutaweza kuwasaidia *Inshaallah*. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri katika kuwasaidia wananchi wetu katika majimbo yetu kuweza kuwapa fedha katika kujikwamua na umaskini.

a) Je, Mhe. Waziri tangu ulipoanza kutoa fedha zile na mpaka sasa hivi unafika mwezi wa ngapi.

b) Je, maafisa wako wamepita lini ili kwenda kuhakikisha zile fedha zinafanya kazi kama ilivyotakiwa ili kuweza kuwaondolea umaskini hao wana vikundi waliopewa fedha hizo.

Mhe. Waziri wa Kazi Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, ni jana tu katika kamati tendaji ya wizara yangu, tumesema miezi mitatu hivi sasa imekamilika, ni wakati muafaka wa kufuatilia vikundi vile na kuona kwamba pesa zile zimetumika vizuri kwa mujibu wa utaratibu ambao umekusudiwa.

Kwa hivyo, hivi sasa kuanzia nadhani kama sikosei wiki ijayo basi maafisa wetu wa ushirika na maafisa wangu wa Wizarani pale wataanza kupita huko

kwa kushirikiana na Wakfu na Mali ya Amana kwa sababu mambo yetu tumefanya kwa pamoja, kufuatilia ili kuona kuwa fedha kama zinatumika vizuri. Hata hivyo, kuna taarifa ambazo ni lazima niziseme hapa kwamba kuna baadhi ya watu ambao tumewapa fedha zile hadi hii leo hawajafanya jambo lolote ambalo ama walililoliombea au lile ambalo lilikusudiwa wakati ule tukitoa fedha zile.

Kwa hivyo, *Inshaallah* tutajitahidi wale ambao hawajazitumia pesa zile tutawaomba wazirejeshe na wakishazirejesha wale ambao walikosa kama Mhe. Hija Hassan na Mhe. Makame Mshimba *Inshaallah* na wao tutawapelekea katika majimbo yao.

Nam. 49

Ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Amali - Mtambwe

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa na mpango wa kujenga Chuo cha Mafunzo ya Amali kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba, katika Jimbo la Mtambwe na eneo lilipatikana katika kijiji cha Bwagamoyo - (Shehia ya Piki).

(a) Ni sababu zipi zilizofanya Chuo kile kutojengwa hadi hii leo

(b) Kama azma ya ujenzi ipo pale pale ujenzi huo utaanza lini

Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 49 lenye sehemu (a) na (b). Lakini kwanza naomba kwa ruhusa yako pia nitoe maelezo ya utangulizi na baadae nijibu hayo maswali.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) ya Afrika, itajenga vituo viwili vya kazi za amali au mafunzo ya amali kwa Unguja na Pemba, kwa kupitia mradi wa Elimu Mbadala na Elimu ya Mafunzo ya Amali awamu ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mradi huu au eneo lililochaguliwa lilikuwa Daya Mtambwe na baadae likaja wazo kwamba Daya Mtambwe ni mbali, kutoka barabarani na wananchi wengi watashindwa kufika kule au wanafunzi wengi watashindwa kufika kule. Baadae likaja wazo kwamba kituo hicho kijengwe

Bwagamoyo. Tulipofanya uchunguzi kati ya maeneo hayo mawili, tukagundua eneo la Bwagamoyo lina mikarafuu mingi na haitawezekana kuikata mikarafuu kwa kujenga hicho kituo cha amali.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la pili lililotokea ni kwamba bado hatujapata Mkandarasi na msanifu wa uchoraji wa hivyo vituo, ambaye sasa tunamtafuta kwa nguvu zetu zote na hivi karibuni tutakutana naye au tutakutana nao ili kujadiliana nao ili tujue yupi mmoja wao atakayetufaa kufanya kazi hiyo. Hata hivyo, kulikuwa na pendekezo la kwamba kituo hicho sasa kijengwe Bwagamoyo. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema eneo hilo lina mikarafuu mingi, haitowezekana kabisa kukata mikarafuu tukajenga hicho kituo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumuarifu Mhe. Mwakilishi kwamba tushirikiane kulitafuta eneo jengine lililokuwa zuri litakalokuja kufaa kujenga kituo hicho. Azma ya kujenga kituo hicho katika Jimbo la Mtambwe iko pale pale, na tutaitekeleza kwa msimamo huo.

Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mjumbe maswali yake yenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Azma ya Ujenzi wa Kituo cha Amali ipo pale pale. Ujenzi wa kituo hicho haujaanza kutokana na kutompata mkandarasi atakayesimamia mjenzi na mtaalamu atakayesimamia uchoraji wa kituo hicho. Hivi sasa hatua zimeshachukuliwa za kutoa tangazo ili tuwapate huyo mkandarasi na mchoraji ili kuanza kazi ya ujenzi.

b) Ujenzi wa kituo hicho na vyengine utaanzishwa katika robo ya mwisho wa mwaka wa fedha 2013/2014, ambapo fedha zake zimeshatengwa katika bajeti yetu ya mwaka huu. Mhe. Mwenyekiti, ahsate sana.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutoa maelezo ambayo ni ya uhakika kabisa kwa asilimia 90. Lakini kwa asilimia 10 kwa bahati mbaya, kwa sababu kapewa maelezo ambayo sio sahihi kuwa eneo ni lenye mikarafuu mingi. Eneo hili nilikwenda kulitafuta mimi na kuliomba, nikamchukua Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Mkuu wa Wilaya akaliona na wote wakasema tuonane na watu wanaohusika na mazingira kwa sababu ni eneo lenye msitu mkubwa zaidi kuliko mikarafuu mmoja mmoja iliomo.

Kwa hivyo, pamoja na kuwa Mhe. Waziri katia wasi wasi, lakini kwa sababu namthibitishia kuwa liko eneo jengine ambalo nilielekezwa kama hivyo kujengwa chuo kikubwa kuliko chuo chengine katika Zanzibar hii na mpaka leo bado. Je, Mhe. Waziri atakwenda kuhakikisha kwanza kuwa hilo eneo ni safi ili baadae kusiwe tena na usumbufu, ikawa mambo haya yasiende kama yalivyokusudiwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimefurahi sana kusikia kwamba eneo jengine limeshapatikana, linafaa na linatosha. Nataka nimuahidi Mheshimiwa mara tu baada ya kikao cha bajeti nina dhamira ya kwenda Pemba na *Inshaallah* tutakwenda pamoja kwenda kulikagua hilo eneo, ili tukimaliza suala la mkandarasi na mshauri, basi tutaanza shughuli za ujenzi.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara ya elimu imejenga chuo kizuri cha amali katika eneo la Vitongoji Jimbo la Wawi Wilaya ya Chake Chake na hivi sasa inafikiria kujenga chuo chengine cha amali katika Wilaya ya Wete, kwa sababu kuna baadhi ya ufundi haujaanza kusomeshwa kwenye chuo cha amali Vitongoji.

(a) Je, Mhe. Waziri atatuhakikishia vipi katika chuo kitakachojengwa kitasomesha taaluma zote zinazohitajika na vijana wetu.

(b) Ni lini taaluma zote zitaanza kusomeshwa katika chuo cha amali Vitongoji, kama vile ufundi wa mafriji, redio na TV

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, Vitongoji ni kweli tumejenga kituo hicho na huko Mtambwe tutajenga, Unguja tumeshajenga. Shughuli za mafunzo ya amali tumezipa kipaumbele kikubwa sana kutokana na tatizo la ajira. Tutakapowasomesha wanafunzi mafunzo ya amali, wakayaelewa, wakapasi mitihani yao na tunayo *project* ambayo itawasaidia kuwapa mikopo, ili waanze kutafuta zana za kujitegemea katika kazi zao. Kwa hivyo, lengo letu ni kufanikisha shughuli zetu za mafunzo ya amali kama tulivyozipanga, hivyo basi namuomba Mhe. Mjumbe katika hili tumejitayarisha na tunaendelea kutafuta walimu wa ziada kwa ajili ya kuwafundisha watoto wetu, ili wafanikiwe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa zamani tulikuwa tukizungumzia wakati wa enzi ya

TANU tulikuwa tukizungumzia elimu ya kujitegemea na sasa tunazungumzia elimu mbadala au mambo ya mafunzo ya amali.

Vile vile kwa kuwa amekubali kwamba hichi chuo atakijenga Mtambwe na kwa sababu sehemu za Mpakanjia, Kiapaka, Nyali yaani hayo ni maeneo ya Mtambwe na ardhi yake ni yenye rutuba na wako katika *coastal plan* ya Kisiwa kile cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye vyuo vyetu vyote vilivyoanzishwa wanazungumzia mafunzo haya ya mafriji, mambo ya ushoni pamoja na mambo mengi kadhaa. Kwa kweli asilimia karibu 90 ya Wazanzibari wamejikita katika masuala ya kilimo na uvuvi. Je, Mhe. Waziri ni lini kwenye vyuo hivi vya mafunzo ya amali ataanzisha mafunzo ya *agricultural chemistry* pamoja na mambo ya *marine navigation engineering*.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni lini tutawafundisha au tutaanzisha mafunzo kwa wanafunzi wetu kuhusu masuala ya kilimo na uvuvi, kwa sababu ndio amali kubwa inayofanywa na wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tunajiandaa katika kutoa mafunzo hayo kwenye Vituo vyetu vya Mafunzo ya amali, lakini pia katika Chuo chetu Kikuu cha Taifa *SUZA*, kwamba mpango uko mbioni na unakaribia kumalizika, kuhakikisha kwamba mafunzo hayo yanatolewa na tunafufua ule utaratibu wa zamani uliokuwepo kwa kufundisha masomo ya amali ya shughuli za kilimo na uvuvi.

Kwa hivyo, tuko mbioni kuanzisha masomo hayo haraka iwezekanavyo Chuo Kikuu chetu cha Taifa cha *SUZA*, pia kwenye vituo vyetu vya amali, lakini bado hatujajiandaa vya kutosha, isipokuwa tutajiandaa na ninakubaliana na yeye sana kwamba kuna haja ya kuwafundisha wanafunzi wetu mafunzo hayo ya amali ya kilimo na uvuvi. *(Makofi)*

Nam. 6

Ulipaji Fidia Wananchi Walioathirika na Mradi wa Umeme

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa Shirika la Umeme (*ZECO*) kwa upande wa Pemba katika mwezi wa Disemba/Januari 2013 wana mpango wa kuweka umeme kuanzia Vitongoji Darajani hadi Makaani Kwareni. Katika mpango wao huo wamekata miti ya kudumu, mazao ya biashara pamoja na chakula. Kwa kuwa

shirika hilo liliendesha mpango huo bila ya kuwashirikisha wakulima wenyewe kufanya tathmini ya mazao yao, na kwa vile hadi leo hii hakuna hata mkulima mmoja ambaye amelipwa fidia ya mazao yake.

(a) Je, serikali inalifahamu hilo.

(b) Ni lini wakulima hao watalipwa fidia zao.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 6 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli suala hili alililoliuliza wizara yangu inalijua.

(b) Kwa kuwa fidia hiyo inalipwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, hivyo wizara yangu itafuatilia na kujua fidia hiyo itapatikana lini.

Mhe. Mwenyekiti, bado nasimama katika jibu ambalo nilimjibu jana wakati aliponiuliza swali la nyongeza kwamba suala hili lina utata ambao lazima mimi na yeye tukutane, kwa ajili ya kulitatua tatizo hili kwa uangalifu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze na kumsifu Mhe. Waziri kwa jinsi alivyobobea katika masuala ya *public relations (PR)*. Kwa hivyo, kwa heshima kubwa na kwa niaba ya watu wa Wawi na wapiga kura wote wa jimbo lile, tunamshukuru sana kwamba anahitaji mlahaka na watu wa Wawi kupitia Mwakilishi wao katika suala zima la kufanya majadiliano juu ya malipo ya fidia hii, kwa hili Mhe. Waziri nampongeza sana.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti, nadhani katika hili la watu kukatiwa mazao yao pale huu ni karibu mwezi wa saba, watu wamekatiwa miembe ambayo ilikuwa na embe, ambazo wangeweza kuuza na kupata riziki zao na kuweza kuishi na watoto wao na hiyo miembe mingine baada ya miezi saba ingekuwa imeshazaa tena na wanajitayarisha kwa kuvuna na kuuza tena.

Lakini katika kipindi chote hichi hawauzi wala hawavuni na mazungumzo ndiyo yanataka kuanza sasa baina ya mimi Mwakilishi wa Jimbo la Wawi na yeye Mhe. Waziri juu ya kuwapatia fidia.

(a) Hivi haoni kwamba haki za watu wa Jimbo hili la Wawi zimechelewa kutolewa na kwa msingi huo ni sawa kama hazikutolewa.

(b) Je, baada ya makubaliano yetu mimi na Waziri sijui yatachukua muda gani mpaka tufike pahala watu waliokatiwa miembe, minazi na migomba yao walipwe walipwe. Je atakuwa tayari kuweza kulipa gharama za kuchelewa kulipwa hizi haki zao, ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Umeme liliombwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupeleka umeme Kwareni Vitongoji. Katika makubaliano yao Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano walikubali kulipa fidia ya mazao na ndipo Shirika la Umeme likachukua hatua ya kupima na kupunguza ile miti ambayo ilihitajika kupunguzwa. Kwa kweli hatuna utaratibu wa kulipa fidia ya zile siku ambazo ile fidia haikulipwa kwa sababu imechelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba ninachoweza kukifanya katika wizara yangu ni kurudi tena katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kukubaliana kwamba deni hili wananchi wa Wawi walipwe, kwa sababu miti yao kweli imeathirika na hesabu zipo na wala hazikupotea mpaka leo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, vipi kuhusu pongezi pamoja na mambo ya *PR* yake na watu wa Wawi amezipokea au laa. *(Vicheko/Makofi)*
Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, unatakiwa upokee shukurani, sasa anauliza umezipokea. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru sana Mhe. Saleh Nassor Juma muasisi kwa shukurani zake alizonipa na nitashirikiana naye vizuri na atashangaa mashirikiano yangu, yaani nitakwenda kwa *speed* ya *supersonic*. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kumpisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, naomba tutambue ujumbe wa wanafunzi 40 kutoka. *Kindergarten School* inayoitwa *MUNA Kindergarten* na *Primary School* iliopo Mwembe Madema. Kwa hivyo, naomba wageni wetu musimame. *(Makofi)*

Ujumbe huo unaongozwa na walimu 6 na hao ni wageni wa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Wageni wetu karibuni sana. *(Makofi)*

Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, karibu. *(Vicheko/Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi, ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili, kuchangia na hatimaye liweze kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili tukufu, kwa ajili ya kujadili mambo muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya viongozi na watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, napenda kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuendeleza utaratibu wa kutenga sehemu ya muda wake kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli mbali mbali zinazotekelezwa kupitia taasisi zetu. *(Makofi)*

Kwa hakika hatua hii imezidisha uwezo wa taasisi wa kutayarisha mipango mizuri pamoja na kuweka kumbukumbu za utekelezaji wa kila siku. Utaratibu huu unachangia juhudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha maendeleo na huduma bora kwa wananchi zinapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuweza kusimamia vyema majukumu yake jambo linalotupelekea kuwa makini katika utendaji wetu. Pia napenda kumshukuru Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa msukumo wa kiutendaji tunaoupata kutokana na usimamizi wake mzuri wa shughuli za serikali. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia uniruhusu kukushukuru wewe binafsi. Mhe. Spika pamoja na wasaidizi wote wa Baraza kwa kazi ngumu ya kuliongoza Baraza hili tukufu, kwa hakika kazi yenu munaimudu ipasavyo. Uzoefu ulionao wa kiutendaji unachangia sana kuleta utulivu na ufanisi wa Baraza hili tukufu na kuweza kulipatia sifa kwa utendaji wake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukurani za dhati kwa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi zinazofanya kazi na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura na Kamati ya Kusimamia Hesabu za Serikali inayoongozwa na Mhe. Omar Ali Shehe, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati hizi kwa kuchaguliwa kuziongoza tena kamati hizo, bila ya shaka hii inatokana na umahiri na utendaji bora wa majukumu yao. Pia napenda kuzihakikishia kamati hizi, kwamba tunathamini sana ushauri na miongozo wanayotupa na hakika inatusaidia kutekeleza majukumu yetu vizuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi, kwa kunipa ushirikiano wa dhati tukiwa ndani na nje ya Baraza. Ni imani yangu kuwa ushirikiano wao huo umechangia kwa kiasi kikubwa kuniwezesha kupata heshima ya kutambuliwa na Ubalozi wa Marekani uliopo nchini Tanzania kuwa mmoja kati ya Wanawake wawili Majasiri hapa Tanzania kwa mwaka 2013. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Afisa Mdhamini wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwa mashirikiano makubwa wanayonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yetu. Vile vile, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wakurugenzi Watendaji, Wakurugenzi, pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa juhudi, bidii na ustahamilivu katika kutekeleza majukumu yao ya kazi na kuleta ufanisi na tija kwa taifa. *(Makofi)*

MALENGO MAKUU YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la kusimamia na kuratibu masuala ya mazingira, watu wenye ulemavu, udhibiti wa dawa za kulevya na UKIMWI. Malengo makuu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni:

1. Kuimarisha na kutetea uzingatiaji wa haki za binadamu na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu ndani ya jamii.
2. Kuongoza, kuratibu, kufuatilia na kutathmini muitikio wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI.
3. Kuimarisha usimamizi wa mazingira na matumizi endelevu ya maliasili.

4. Kuratibu na kudhibiti usafirishaji, uingizwaji, matumizi na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatekeleza majukumu yake kupitia Taasisi zifuatazo:-

1. Ofisi ya Faragha
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
4. Idara ya Mazingira
5. Idara ya Watu Wenye Ulemavu
6. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba
7. Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya na
8. Tume ya UKIMWI.

VIPAUMBELE VYA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2013/14

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia vipaumbele vifuatavyo:-

- Kujenga uwezo wa watendaji katika maeneo ya utafiti
- Kufanya tafiti na kukusanya taarifa juu ya shughuli zinazotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais
- Kukabiliana na athari za kuhimili mabadiliko ya tabianchi
- Kuandaa Mkakati wa Usimamizi wa taka ambao utatoa vipaumbele vya hatua zinazofaa kuchukuliwa
- Kupunguza uchukuaji usiofuata taratibu wa maliasili zisizorejesheka
- Kupambana na usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya
- Kuwa na mfumo uliokamilika wa taarifa(*data base*) pamoja na mahitaji kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu
- Kutoa huduma maalum kwa Watu Wenye Ulemavu
- Kuikinga jamii kwa ujumla na makundi maalum kutokana na mambukizi ya Virusi vya UKIMWI na
- Kutafuta rasilimali ili kutekeleza shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA 2012/13 NA MALENGO 2013/14

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha ina majukumu ya kutoa huduma pamoja na kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazofanywa na Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Ofisi ya Faragha ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuimarisha mazingira ya kazi katika kuleta ufanisi wa wafanyakazi.
3. Kuimarisha huduma za Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2013 Ofisi ya Faragha imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-
Mhe. Mwenyekiti, taasisi 15 zimesaidiwa katika kutimiza ahadi alizozitoa Makamu wa Kwanza wa Rais. Aidha, jumla ya wananchi 250 vikiwemo vikundi vya jamii na taasisi nyengine walifika ofisini kwa Makamu wa Kwanza wa Rais na kupatiwa huduma mbali mbali.

Jumla ya ziara tano zimefanywa na Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais katika Mikoa ya Tanzania Bara na ziara mbali mbali za kuzitembelea Ofisi za Serikali Zanzibar. Katika ziara hizo, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alipata fursa ya kushiriki katika shughuli za kijamii, kuzindua na kuweka mawe ya msingi ya miradi ya maendeleo.

Vile vile, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alifanya vikao tisa vilivyowashirikisha mawaziri na viongozi wakuu wa taasisi mbali mbali za serikali kwa lengo la kupata taarifa za utekelezaji wa maagizo aliyoyatoa kuhusiana na matatizo yanayowakabili wananchi kwenye maeneo aliyoyatembelea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha Ofisi ya Faragha vifaa mbali mbali vimenunuliwa likiwemo jenereta moja la KVA 70. Mfanyakazi mmoja amepelekwa masomoni, kwa ajili ya kusoma Diploma ya ukatibu muhtasi (angalia kiambatanisho namba 1).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ya Faragha ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 511,324,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 300,000,000/= kwa kuendeshea kazi na shilingi 211,324,000/= kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei 2013, ofisi hii imekwishatumia jumla ya shilingi 237,900,000/= sawa na asilimia 79 ya makadirio kwa kuendeshea kazi.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kuratibu shughuli zote za Makamu wa Kwanza wa Rais.
2. Kuimarisha utoaji wa huduma kwa Makamu wa Kwanza wa Rais.
3. Kuimarisha mazingira ya kazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Faragha iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, naliomba Baraza lako liidhinishe jumla ya shilingi 515,150,000/= kwa ajili ya kuendeshea kazi.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina majukumu ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kukusanya, kutunza takwimu, ufuatiliaji na tathmini pamoja na kuratibu shughuli za utafiti kwa idara zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu utayarishaji na utekelezaji wa sera, mikakati, mipango na bajeti.
2. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli mtambuka, UKIMWI, dawa za kulevya, mazingira, watu wenye ulemavu, utawala bora, jinsia na idadi ya watu.
3. Kuimarisha mazingira ya kazi na kujenga uwezo kwa watendaji.
4. Kuratibu miradi ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kusimamia utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeweza kutekeleza mambo yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Mwenyekiti, idara imeendelea na utekelezaji wake wa kawaida wa kuandaa mipango ya utekelezaji, bajeti, pamoja na kuiwakilisha ofisi katika vikao vya kitaalamu, ili kuhakikisha masuala yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais yanazingatiwa katika mipango mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira ya kazi na kujenga uwezo kwa watendaji, mtendaji mmoja amelipiwa sehemu ya gharama ya masomo ya ngazi ya shahada ya pili katika fani ya uchumi, (rejea kiambatanisho namba 1). Pia, mfanyakazi mmoja amehudhuria mafunzo ya siku tano Dar-es –salaam juu ya namna ya kuingiza masuala ya mabadiliko ya tabia nchi katika mipango.

Mhe. Mwenyekiti, Muon**g**ozo wa Uzingatiaji wa Mambo Mtambuka (UKIMWI, Watu Wenye Ulemavu na Dawa za Kulevya) yanayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais umeandaliwa. Muongozo huu unatarajiwa kuzielekeza taasisi mbali mbali juu ya namna ya kuingiza mambo mtambuka katika sera na mipango yao. Kufanya kazi kwa muongozo huu kutapelekea kuwa na juhudi za pamoja za utekelezaji wa masuala ya mtambuka.

UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iliratibu utekelezaji wa miradi 5 ya maendeleo kwa fedha za serikali na miradi 2 kwa fedha za wahisani kama ifuatayo:-

1. Mradi wa kujenga uwezo wa OMKR chini ya *UNDAP* (unaratibiwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo).
2. Mradi wa kuimarisha usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kupitia mradi wa *UNDAP*.
3. Mradi wa kuangamiza kunguru weusi.
4. Mradi wa elimu ya mazingira.
5. Mradi wa majaribio wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.
6. Mradi wa kuingiza masuala ya watu wenye ulemavu katika mipango ya maendeleo.
7. Mradi wa Kujenga Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya huko Tunguu (*Construction of Treatment and Rehabilitation Center*).

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mradi wa Kujenga Uwezo wa OMKR chini ya *UNDAP*

Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi huu ambao fedha zake hupitia Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Idara imeandaa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa kipindi cha miaka 7 (2013 - 2020). Mpango huu utakuwa ndio dira kuu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi.

Idara pia imeandaa Mpango Mkuu wa Utafiti ambao umeainisha maeneo makuu yanayohitaji kufanyiwa utafiti kwa kipindi cha miaka 7 (2013-2020). Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, OMKR ilitarajia kupata jumla ya shilingi 162,973,000/=. Hadi mwezi wa Mei 2013 idara ilikwisha kuingiziwa jumla ya shilingi 140,000,000/= sawa na asilimia 87 kwa utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia nchi

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu unaofadhiliwa na *UNDAP* na kuratibiwa na OMKR, unatekelezwa na OMKR pamoja na watekelezaji wengine wakiwemo Ofisi ya Rais, Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo, Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Idara ya Nishati, Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka na Jumuiya ya Maendeleo ya Jamii na Uhifadhi wa Mazingira Zanzibar (*Community Development and Environmental Conservation Zanzibar – CODECOZ*). *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lengo kuu la mradi huu ni kujenga uwezo kwa taasisi mbali mbali katika kuhakikisha masuala ya mabadiliko ya tabia nchi yanaingizwa katika mipango ya sekta. Aidha mradi huu utaweka mifumo mbali mbali itakayorahisisha utekelezaji wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi ikiwemo kuandaa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia nchi pamoja na mpango wa utekelezaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia nchi umo katika matayarisho, ripoti ya utangulizi imewasilishwa na mshauri elekezi "*Global Climate Adaptation Partnership*" kwa kupitiwa na wadau. Rasimu ya kwanza inatarajiwa kuwasilishwa mwezi wa Julai.

Aidha, kampuni ya "*Global Climate Adaptation Partnership*" (*GCAP*) imepewa kazi ya kuainisha mapungufu katika MKUZA II na kuweka

vipaumbele vya fursa za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Kampuni ya "*Environmental Protection and Management Services*" (*EPMS*) imepewa kazi ya kuandaa Muongozo wa Uzingatiaji wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabia nchi. Rasimu za awali tayari zimewasilishwa na kupitiwa na wadau, rasimu ya pili inatarajiwa kuwasilisha OMKR katika wiki ya nne ya mwezi wa Juni 2013 kwa mapitio ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, vikao mbali mbali vya kamati ya wataalamu na uongozi vya mabadiliko ya tabia nchi vimefanyika na kutoa ushauri juu ya namna ya kutekeleza kazi za mradi (*UNDAP*) pamoja na kujadili masuala yanayohusu mabadiliko ya tabia nchi Zanzibar. Aidha Mkutano wa siku mbili wa kujenga uwezo wa wadau walioshiriki katika mkutano wa Umoja wa Mataifa wa kumi na nane wa mabadiliko ya tabia nchi nchini Qatar na mkutano wa siku mbili wa kutafakari utekelezaji wa mambo yaliyokubalika nchini Qatar umefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 mradi huu ulitegemea kupata fedha za wahisani jumla ya shilingi 705,600,000/= hadi kufikia mei 2013 jumla ya shilingi 616,752,700/= sawa na asilimia 87.4 zilikwishapatikana. Mgao wa fedha kwa watekelezaji wa mradi huu ni kama inavyoonekana kwenye (kiambatanisho nam. 2)

Mradi wa Kuangamiza Kunguru Weusi

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mradi huu, hadi kufikia mwezi wa Mei 2013 jumla ya kunguru 10,008 wameuliwa kwa kutumia mitego na sumu. Kwa mwaka 2012/2013, jumla ya shilingi 50,000,000/= zilipangwa kutumika na hadi kufikia mwezi wa Mei 2013 shilingi 30,000,000/= sawa na asilimia 60 zilikwishapatikana.

Mambo yaliyofanyika kwa fedha hizo ni pamoja na kutengeneza mitego 6 na kusambazwa maeneo mbali mbali, kununua sumu ya kuulia kunguru kilo moja na nusu kutoka New Zealand, kununua vifaa mbalimbali vikiwemo mabeseni, ndoo, sinia, vijiko, glavu, mapanga na majembe pamoja na kununua chambo cha kutumika kwenye sumu na mitego. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kuendelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, meza mnazigonga vibaya sana, tunazihitaji kwa kipindi hichi na wengine watakaoingia pia waje kuzitumia. Mhe. Waziri endeleea. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti.

Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza mradi huu, semina sita kwa kamati sita za Polisi Jamii za Wilaya ya kati na semina nne kwa Kamati nne za Polisi Jamii za Wilaya ya Mkoani zimefanyika juu ya kuzielewa na kuzitumia sheria za mazingira.

Operesheni 4 za usafi wa Mazingira, zimefanyika na vifaa vya usafi kama vile mabero, mareki, *gloves*, na mapauro vimetolewa kwa jumuia za Mazingira. Kwa mwaka 2012/2013, jumla ya shilingi 25,000,000/= zilitarajiwa kutumika, hadi kufikia mwezi wa Mei 2013 shilingi 25,000,000/= sawa na asilimia 100 zilikwishapatikana.

Mradi wa Majaribio wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia nchi

Mhe. Mwenyekiti, katika kukamilisha utekelezaji wa mradi huu, serikali kwa mwaka 2012/2013 ilipanga kutumia shilingi 25,000,000/= kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakulima na wananchi ambao mazao na mali zao zimeathiriwa kutokana na utekelezaji wa mradi kwa kupitisha njia ya umeme pamoja na kuchimba msingi wa kulaza mabomba ya maji. Hadi kufikia Mei 2013 jumla ya shilingi 25,000,000/= sawa na asilimia 100 zilikwishapatikana na kulipwa kwa wananchi 99.

Mhe Mwenyekiti, miradi miwili ambayo ni Mradi wa Kuingiza Masuala ya Watu wenye Ulemavu katika Mipango ya Maendeleo uliopangiwa kutumia shilingi 25,000,000/= na Mradi wa Kujenga Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya huko Tunguu ulipangiwa kutumia shilingi 100,000,000/= hadi kufikia Mei 2013 miradi haikuingiziwa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kutumia shilingi 176,251,000/= kwa kazi za kawaida ambapo shilingi 115,000,000/= kwa ajili ya kuendeshea kazi na shilingi 61,251,000/= kwa ajili ya mishahara.Hadi kufikia Mei 2013 ilikwisha kuingiziwa TZS 62,500,000 sawa na asilimia 54 kwa kuendeshea kazi. Idara pia ilikadiria kutumia jumla ya TZS 255,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa serikali, hadi kufikia Mei 2013 ilikwisha kuingiziwa TZS 80,000,000 sawa na asilimia 31. Kwa upande wa fedha za wahisani, ilitarajia kutumia jumla ya TZS 705,600,000, hadi Mei 2013 ilikwisha kuingiziwa jumla ya TZS 616,752,700 sawa na asilimia 87.4.

Malengo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo**:-**

Kujenga uwezo wa watendaji na kufanya tafiti mbili. Tafiti ya kwanza ni kwa ajili ya kukusanya taarifa za awali juu ya hali halisi ya shughuli zinazotekelezwa na OMKR na ya pili ni utafiti wa kuangalia vikwazo vilivyopo kwa Watu Wenye Ulemavu katika sekta ya elimu na ajira kama Mpango Mkuu wa Utafiti wa OMKR unavyoelekeza.

1. Kusimamia na kutekeleza mambo mtambuka yanayosimamiwa na OMKR.

2. Kuratibu, kusimamia na kutekeleza mipango ya kazi na bajeti ya OMKR.

3. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Miradi ya Maendeleo Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatarajia kutekeleza miradi 2 kwa kupitia fedha za Serikali na miradi 2 kwa fedha za wahisani kama ifuatavyo:-

Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Mazingira

Mradi huu una lengo la kuendelea kutoa elimu ya mazingira kwa jamii kwa madhumuni kuongeza uelewa juu ya uhifadhi endevu wa mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 unatarajiwa kutumia fedha za serikali TZS 50,000,000

Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya huko Tunguu

Mradi huu una lengo la kujenga kituo cha kurekebisha tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya ili kuwa na jamii bora. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 unatarajia kutumia fedha za serikali TZS 100,000,000

Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi chini ya mradi wa UNDAP.

Mradi huu wa miaka 4 ulioanza kutekelezwa 2011/2012. Utaingia katika mwaka wa 3 wa utekelezaji na unategemewa kumalizika mwaka 2014/2015. Lengo lake kuu ni kujenga uwezo kwa taasisi katika kuhakikisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanaingizwa katika mipango ya sekta na kuweka mifumo mbali mbali itakayorahisisha utekelezaji wa masuala ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 mradi unategemea kutumia fedha za wahisani jumla ya TZS 800,000,000.

Mradi wa Kujenga Uwezo wa OMKR wa UNDAP unaoratibiwa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mradi huu ni wa miaka 4 na utakuwa unaingia katika mwaka wa 3 wa utekelezaji. Lengo kuu ni kuijengea uwezo OMKR kwa kuisaidia kutengeneza miongozo mbali mbali itakayosaidia katika utekelezaji wa shughuli zake. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 unatarajia kutumia fedha za wahisani jumla ya TZS 200,000,000.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 160,065,000 kwa kuendeshea kazi. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 150,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa serikali na jumla ya TZS 800,000,000 ikiwa ni mchango wa wahisani.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kusimamia rasilimali watu na utawala, kusimamia masuala ya nidhamu, uwajibikaji, mafunzo na stahiki za wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Utumishi na Uendeshaji ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia majukumu na utendaji wa wafanyakazi.
2. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.

3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.

4. Kusimamia utaratibu wa udhibiti wa matumizi ya fedha

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei, 2013 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeweza kutekeleza majukumu yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/13 OMKR imeajiri wafanyakazi 11; kwa kujaza nafasi zilizokuwa wazi, wafanyakazi 5 walistaafu kisheria na wafanyakazi 2 walifariki dunia; Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi amin.

Mheshimiwa Spika katika kusimamia majukumu ya utendaji, vikao viwili vya kamati ya uongozi vya kupitisha muongozo wa nyumba za makaazi *(sober houses)*, Waraka wa sheria ya kukinga na kudhibiti virusi vya UKIMWI pamoja na waraka wa sheria ya marekebisho ya Tume ya UKIMWI vimefanyika. Aidha, wafanyakazi wote wameshapangiwa daraja zao kwa mujibu wa muundo wa utumishi *(scheme of service).*

Mhe. Mwenyekiti, katika kujenga mazingira mazuri ya ufikiaji kwa watu wenye ulemavu, "ramp" imejengwa katika jengo la OMKR. Gharama za bili mbalimbali zimelipwa; matengenezo ya gari 3, bima ya gari pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya ofisi umefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, Wafanyakazi wawili wanaosoma katika ngazi ya Stashahada na Shahada katika fani ya Sekretari na Ugavi wamelipiwa masomo yao.Wafanyakazi wengine 3 wamesaidiwa gharama za vifaa vya kuandikia na mmoja amelipiwa posho kwa mafunzo mafupi. (Rejea kiambatanisho namba 1)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa jamii kupata taarifa juu ya mambo yanayotekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi imenunua televisheni moja na deki kwa ajili ya kutayarisha vipindi. Filamu fundishi moja ya watu wenye ulemavu wanaoishi katika mazingira magumu imeandaliwa na kuoneshwa katika siku ya kuchangia mfuko wa maendeleo kwa ajili ya Watu Wenye Ulemavu. Malipo ya huduma za mtandao, magazeti na uchapishaji zimelipiwa.

Mhe. Mwenyekiti, vikao viwili vya kamati ya ukaguzi wa hesabu za ndani vimefanyika ili kupitia ripoti za fedha. Vikao vinne vya zabuni na matumizi ya fedha vimeratibiwa kwa mujibu wa kanuni za fedha na sheria za manunuzi. Pia kikao kimoja kilichowajumuisha wahasibu, wakaguzi wa ndani, washika fedha na afisa manunuzi kimefanyika kwa madhumuni ya kusimamia vyema matumizi ya rasilimali za Ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 ilikadiria kutumia jumla ya TZS 616,444,000 kwa kazi za

kawaida. Kati ya hizo TZS 254,749,000 kwa kuendeshea kazi na TZS 361,695,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei, 2013 ilikwisha kuingiziwa kiasi cha TZS 189,372,415 sawa na asilimia 74 kwa ajili ya kuendeshea kazi.

Malengo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
2. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari
3. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.
4. Kusimamia utaratibu wa matumizi ya fedha kwa mujibu wa sheria na kanuni za fedha zilizopo.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimekuwa nikifuatilia tangu ameanza Mhe. Waziri naelewa nia yake anapotwambia kwamba malengo ni kama ilivyo katika paragrafu kadhaa na paragrafu kadhaa, lakini kwa utaratibu kwenye kitabu hichi tunapewa Wajumbe asubuhi tunapoingia hapa na tunakenda sambamba inaposomwa hotuba hii. Ikizingatiwa kwamba akimaliza yeye tu na Mwenyekiti wa Kamati wanatakiwa Wajumbe waanze kuchangia. Nadhani utaratibu huu utakuwa hautusaidii sana.

Kwa hivyo nilikuwa namuomba kwa kutusaidia awe anasoma kama wanavyosoma wenzake maelezo yote yaliyokuwemo katika kitabu chake. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri Mhe. Mjumbe ameleta ombi kwamba usome kama ilivyoandikwa kwenye kitabu cha Bajeti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hakuna tatizo nitaendelea nalo lakini nitaomba pale sauti inapokataa basi wanivumilie vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, Ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 1,615,931,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS 292, 427,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS 1,323,504,000 kwa ajili ya mishahara.

Idara ya Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira, kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango na miradi ya kimaendeleo, kufuatilia mwenendo wa hali ya kimazingira, kukabiliana na matatizo ya kimazingira, kuhamasisha wadau kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira pamoja na kutoa elimu ya mazingira kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Mazingira ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia uingizwaji wa masuala ya mazingira katika miradi ya maendeleo.

2. Kuongeza uwezo na kuimarisha muundo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

3. Kuimarisha usimamizi endelevu wa maliasili.

4. Kuongeza uwelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine.

5. Kuimarisha utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni za mazingira.

6. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2013 Idara imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya miradi 65 ya mahoteli imekaguliwa, miradi 15 ya uwekezaji imefanyiwa tathmini ya athari ya kimazingira (EIA) na kutolewa vyeti vya Mazingira na miradi 5 imefanyiwa uchunguzi wa awali wa kimazingira (*scoping*) ili kutoa hadidu rejea za kufanya tathmini za athari za kimazingira (angalia kiambatanisho nam. 3). Kiwanda cha Makonyo cha Wawi, Pemba kimefanyiwa ukaguzi wa kimazingira na ripoti ya ukaguzi huo imewasilishwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuchukuliwa hatua za utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa.
Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia utekelezaji wa mabadiliko ya tabianchi ngazi ya shehia, kamati kumi za majaribio za usimamizi wa ukanda wa pwani *(Intergrated Coastal Zone Managemant – ICZM)* zimesaidiwa kuandaa

mipango ya utekelezaji wa usimamizi wa mazingira katika maeneo yao; Unguja na Pemba. Kamati hizi zimetayarisha mipango ya utekelezaji ya usimamizi wa mazingira katika maeneo yao. Katika kuziongezea uwezo kamati hizo, mipango ya ICZM ya Shehia za Nungwi na Chwaka imesaidiwa utekelezaji kwa kununuliwa vifaa vya usafi. Aidha, mipango ya ICZM ya Shehia za Mtende na Nyamanzi imesaidiwa kwa kupatiwa miti ya aina mbali mbali ikiwemo ya matunda na misitu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hizi huwezesha Idara ya Mazingira kuwa na mawasiliano na jamii katika kusimamia masuala ya mabadiliko ya tabianchi na kuimarisha muundo wa usimamizi wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya shehia. Warsha ya siku moja ya mabadiliko ya tabianchi na Mpango wa Kupunguza Hewa Ukaa kutokana na Uharibifu wa Misitu na Ukataji Ovyo wa Miti kwa Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara zote za Serikali imefanyika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha usimamizi endelevu wa maliasili, kanuni za usimamizi endelevu wa maliasili zisizorejesheka zimeandaliwa na kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali la tarehe 15 Febuari 2013. Warsha moja ya wadau juu ya kanuni hiyo imefanyika. Usimamizi wa Kanuni hiyo kwa ajili ya kupunguza vitendo vya uchukuaji usiofuata utaratibu wa maliasili zisizorejesheka utafanyika mwaka wa fedha wa 2013/2014. Aidha, ekari 15 za eneo la uwandani Pemba lililochimbwa matofali ya mawe zimefukiwa. Jumla ya miti 2,525 imepandwa katika maeneo yaliyofukiwa, kati ya miti hiyo, 500 ni ya matunda ikiwemo michungwa, miembe na mifenesi; na miti 2,025 ni ya misitu ikiwemo mikungu, mitondoo na mivinje.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kuongeza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine, jumla ya vipindi 15 vya redio na vipindi 3 vya TV vinavyohusu usimamizi wa mazingira vimerushwa hewani, jumuiya na Kamati za Mazingira 8 zimepatiwa elimu ya Mazingira (angalia kiambatanisho 4).

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba sera, sheria na kanuni za mazingira zinatekelezwa, jumla ya operesheni 117 zimefanyika Unguja na Pemba na watu 33 wamekamatwa na kuhukumiwa kwa faini ya TZS 3,280,000 kwa jumla. Aidha, kilo 670 za mifuko ya plastiki zimeteketezwa katika eneo la Maruhubi. Aidha, sera mpya ya mazingira imeandaliwa na kuidhinishwa na serikali na mpango wa utekelezaji wa usimamizi wa Mazingira umeandaliwa kwa mujibu wa sera mpya ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi 7 wamelipiwa sehemu ya gharama za mafunzo ya ngazi za Cheti na Stashahada katika fani za utumishi wa umma (3), ukutubi (1), Kingereza (1), na ukatibu muhtasi (2), wafanyakazi 5 wamelipiwa mafunzo mafupi ya usimamizi wa Mazingira katika vyuo vya Tanzania Bara. (Rejea kiambatanisho namba 1).

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kutumia TZS 369,369,000 kwa kazi za kawaida kati ya hizo TZS 112,373,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS 257,296,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei 2013 ilikwisha kuingiziwa jumla ya TZS 68,600,000 sawa na asilimia 61 kwa kuendeshea kazi. Aidha Idara ya Mazingira ilipangiwa kukusanya jumla yaTZS 10,800,000 kutokana na huduma ya tathmini za athari za kimazingira. Hadi kufikia mwezi Mei 2013, Idara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 6,830,000 sawa na asilimia 63.

Malengo kwa Mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha usimamizi wa udhibiti wa uchafuzi wa mazingira.
2. Kuimarisha usimamizi endelevu wa maliasili.
3. Kukuza uelewa wa elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine wa mazingira
4. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi
5. Kuimarisha na kusimamia utekelezaji wa mikakati, sera, sheria na kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mazingira iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 127,884,000 kwa ajili ya kuendeshea ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira kwa mwaka wa fedha 2013/2014, imepangiwa kukusanya jumla ya TZS 10, 500,000 kutokana na ada ya hifadhi ya mazingira ikwa ni pamoja na vyeti vya mazingira.

Idara ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kuratibu masuala mbali mbali ya watu wenye ulemavu kwa mujibu wa Sheria No. 9 ya mwaka 2006.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Watu Wenye Ulemavu ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu.

2. Kuwapatia visaidizi na kuimarisha juhudi za taasisi katika kushughulikia masuala ya Watu wenye Ulemavu.

3. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za watu wenye ulemavu.

4. Kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na kujenga uwezo wa wafanyakazi katika kuleta ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2013, Idara ya watu wenye ulemavu imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Mwenyekiti, vikao vinne vya Baraza la Taifa la watu wenye ulemavu vimefanyika na kujadili mambo mbali mbali yanayowahusu watu wenye ulemavu. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa ni matayarisho ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye Ulemavu ambayo hufanyika kila ifikapo tarehe 3 Disemba. Kwa mwaka huu wa fedha maadhimisho hayo yalifanyika kisiwani Pemba ambayo yametoa muamko kwa jamii juu ya haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu. Ujumbe wa maadhimisho ya mwaka huu ni "**Ondoa vikwazo ili kujenga jamii jumuishi kwa wote"**.

Mhe. Mwenyekiti, Jumuiya 10 za Watu wenye Ulemavu zimepatiwa ruzuku ya TZs 1,700,000 kwa kila moja kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kawaida. Jumuiya hizo ni CHAVIZA, ZANAB, UWZ, JMZ, SAD'Z, JUWAUZA, ZADA, ZACDID, ZAPDD na SOZ. Utoaji wa ruzuku hizo ni miongoni mwa juhudi za serikali katika kuhakikisha jumuiya za watu wenye ulemavu zinatekeleza vyema shughuli za kuwahudumia wadau wao.

Mhe. Mwenyekiti, shughuli ya chakula cha usiku kwa ajili ya kuchangia kutunisha Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu ambao ulianzishwa kwa mujibu ya Sheria namba 9 ya mwaka 2006 ilifanyika. Mfuko huo kwa hivi sasa una jumla ya TZS 158,157,319. Idara inaendelea kuzifuatilia ahadi za michango ambayo bado haijawasiliswa. Aidha, Idara

ilipokea misaada ya visaidizi vya watu wenye ulemavu kutoka kwa Umoja wa Wazanzibari wanaoishi Canada (ZANCANA), Kampuni ya Bopar pamoja na watu wengine mmoja mmoja. Misaada hiyo iligaiwa kwa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha mazingira mazuri ya utendaji na kuleta ufanisi kazini, jumla ya wafanyakazi watatu wamechangiwa gharama za masomo, katika mafunzo ya Shahada ya pili ya Sheria, Shahada ya kwanza ya IT, na Stashahda ya uhasibu. (rejea kiambatanisho namba 1)

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya Shehia 19 za Mkoa wa Mjini Magharibi na 3 za Mkoa wa Kusini Unguja zimefanyiwa uhamasishaji, wazee wa watoto wenye ulemavu na wazee wa watoto wasio na ulemavu walishiriki katika zoezi hilo. Uhamasishaji huo ulikuwa juu ya kuinua uwelewa katika masuala ya haki za watu wenye ulemavu, Mkataba wa Kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu na Sera ya Maendeleo kwa Watu wenye Ulemavu. (angalia kiambatanisho nam 5). Vikao vinne vya maafisa waratibu wa masuala ya Watu wenye Ulemavu vimefanyika ili kufuatilia utekelezaji wa Sheria ya Haki na Fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuendeleza usajili wa watu wenye ulemavu jumla ya wilaya 9 zimefanyiwa usajili ikiwa wilaya 5 za unguja na wilaya 4 za Pemba kwa ajili ya kuweza kupata takwimu sahihi na kurahisisha upangaji wa Sera na Mipango ya Maendeleo kwa Watu wenye ulemavu (angalia kiambatanisho nam 6).

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kutumia TZS 532,562,000 kwa kazi za kawaida kati ya hizo TZS 435,570,000 kwa kuendeshea kazi na TZS 99,992,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei 2013 ilikwisha kuingiziwaTZS 391,000,000 sawa na asilimia 92.8 kwa kuendeshea kazi.

Malengo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha Mazingira ya Utendaji kazi.

2. Kutengeneza mfumo wa takwimu (data base) za watu wenye ulemavu.

3. Kusimamia haki, fursa sawa na ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Watu Wenye Ulemavu iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 396,782,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi hii ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na Kuratibu utekelezaji wa shughuli zote za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba.

2. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

3. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari.

4. Kusimamia na kuratibu udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2013 Ofisi Kuu Pemba imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba, Elimu juu ya athari za dawa za kulevya ilitolewa katika skuli za sekondari 17 ambapo jumla ya wanafunzi 1,117 (wanaume 540, wanawake 577) na walimu 49 (wanaume 40, wanawake 9) walifikiwa. (Angalia kiambatanisho nam7). Aidha, tathimini ilifanywa kwa Wateja walioingia *sober house* iliyojumuisha vijana 181. Tathmini hiyo iliangalia uhakiki wa njia za matumizi ya dawa na kutoa matokeo ambayo yalionesha wanaotumia dawa kwa njia ya kujidunga sindano (IDUs) – 108 na wanaotumia dawa kwa uvutaji unga (SUs) - 73

Mhe. Mwenyekiti, ziara ya kupitia kila Wilaya ili kuyatambua mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kupatiwa visaidizi ilifanyika, kufuatia ziara hiyo watu wenye ulemavu kutoka Shehia mbali mbali walipatiwa visaidizi ili kuwarahisishia kupata mahitaji yao. Ziara nyengine iliyofanyika ni kutembelea vikundi vya ushirika na ujasiriamali vya watu wenye ulemavu kwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Vikundi hivyo ni pamoja na kikundi cha

wasioona (ZANAB) Wete, Kikundi cha Tuimarishe cha Kianga Ole, Vikundi vya Hirimu Mfasi na Tupendane vya Micheweni pamoja na Mwanzomgumu cha Shumba mjini.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi OMKR inaendelea kufanya ufuatiliaji wa maeneo yalioathirika kutokana na uharibifu unaojitokeza, jumla ya maeneo 18 yametembelewa ili kujionea uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uingiaji wa maji chumvi na ukataji ovyo wa mikoko. (Aidha, maeneo yaliyoathirika na uharibifu wa mazingira kutokana na uchimbaji wa mchanga Kangani na ukataji matofali Mwambe yalitembelewa ili kuona ni hatua gani zinaweza kuchukuliwa kunusuru hali iliyopo. Mikutano ya kushauriana juu matokeo ya athari za uharibifu wa mazingira na migogoro iliyopo miongoni mwa wananchi imefanyika na maagizo yametolewa kwa wananchi wa maeneo husika kukubali kufanya yale yaliyo katika uwezo wao kwa hatua za awali.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira bora ya kazi shughuli mbali mbali za kiutawala na uendeshaji zimefanyika ikiwemo kulipa gharama mbali mbali za huduma, matengenezo ya gari, bima ya gari, ulipaji wa kodi ya jengo la ofisi pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya ofisi. Aidha katika kuimarisha mawasiliano ya habari, kamera 1 (*Digital*) imenunuliwa kwa ajili ya usambazaji na ufuatiliaji wa taarifa mbali mbali za utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi hii kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 ilikadiria kutumia jumla ya TZS 316,659,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS 157,774,000 kwa kuendeshea kazi na TZS 158,596,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei 2013 ilikwisha kuingiziwa kiasi cha TZS 77,189,906 sawa na asilimia 49 kwa matumizi ya kuendeshea kazi.

Malengo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi.
2. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi.
3. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba.
4. Kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 330,175,000 kwa kazi

za kawaida kati ya hizo TZS 167,575,000 kwa kuendeshea kazi na TZS 162,600,000 kwa ajili ya malipo ya mishahara.

Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Mhe. Mwenyekiti, Tume hii ina jukumu la kuratibu mapambano dhidi ya biashara, matumizi, uingizwaji na usafirishaji wa dawa za kulevya. Tume pia ina jukumu la kutoa taaluma kwa jamii pamoja na kutoa huduma za tiba na ushauri nasaha kwa watumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na kuendeleza mapambano dhidi ya uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.

2. Kuimarisha mazingira mazuri ya kazi katika kuleta ufanisi.

3. Kuongeza mwamko wa jamii juu ya athari na udhibiti wa dawa za kulevya.

4. Kuratibu na kuimarisha juhudi za taasisi katika kushughulikia mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia Mei 2013 Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Mwenyekiti, ili kuhakikisha Sheria ya Dawa ya Kulevya inatekelezeka *"Road Map"* ya utekelezaji wa sheria hiyo imeandaliwa na kuekewa makisio ya fedha zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji kwa kila mdau, Aidha mkutano wa kwanza wa Tume ya Kitaifa ya Dawa za Kulevya umefanyika ambapo uliweza kujadili mambo mbali mbali yenye lengo la kuendeleza mbele vita dhidi ya dawa za Kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi za taasisi zinazohusika na mapambano ya Dawa za Kulevya pamoja na mashirikiano kutoka kwa raia wema zinaendelea vizuri. Jumla ya watu 22 wamekamatwa kwa makosa ya dawa za Kulevya kati yao (wanaume 21 na mwanamke 1) na kesi 21 ziko mahakamani na upelelezi unaendelea. Katika kuona kwamba sheria ya Udhibiti wa dawa za kulevya inatekelezwa ipasavyo Rasimu ya kanuni ya sheria hiyo tayari imeshaandaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha jamii inapata mwamko juu ya athari na udhibiti wa dawa za kulevya, vipindi 10 vilivyolenga kuinua mwamko wa jamii juu ya athari ya dawa za kulevya vimerushwa hewani kupitia vyombo mbali mbali vya habari viliopo nchini vinavyomilikiwa na serikali na taasisi binafsi kama vile: Zenji FM, ZBC, HITS FM na Bomba FM. Aidha filamu fundishi kuhusiana na athari za dawa za kulevya imetayarishwa ambayo itatumika katika programu na vipindi vya kuhamasisha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, tume pia iliandaa ziara katika skuli za Serikali na Binafsi. Jumla ya wanafunzi 6,270 (wanawake 3,677 na wanaume 2,593) kutoka skuli 45 za Unguja wamepatiwa elimu juu ya athari za dawa za kulevya na maambukizi ya virusi vya UKIMWI. (rejea kiambatanisho namba 7). Ziara za utoaji wa elimu katika shehia mbali mbali za Unguja, kwa lengo la kuonana na kamati za ulinzi na Polisi jamii za shehia hizo ambapo jumla ya shehia 5 za Mkoa wa Mjini/Magharibi ambazo zinaonekana kuathirika zaidi na biashara ya dawa za kulevya na matumizi yake yanayochangia maongezeko ya uhalifu katika jamii zilifanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutambua mchango wa taasisi zisizo za kiserikali katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Tume tayari imeshazipatia ruzuku nyumba tisa za makaazi ya vijana wanaoacha matumizi ya dawa za kulevya *(Sober Houses)* kwa ajili ya kusaidia mahitaji mbali mbali. (Angalia kiambatanisho Nam.8).

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na kuleta ufanisi, mfanyakazi mmoja anaendelea kulipiwa masomo kwa ngazi ya Diploma ya Uhasibu katika Chuo Cha Maendeleo ya Utalii kilichopo Maruhubi–Unguja. (Rejea kiambatanisho namba1).

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kutumia TZS 247,091,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS 146,607,000 kwa kuendeshea kazi na TZS 100,684,000 kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia Mei 2013 ilikwisha ingiziwa TZS 66,435,000 sawa na asilimia 45 kwa kuendeshea kazi.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo;

1. Kupunguza matumizi ya Dawa za Kulevya.
2. Kupunguza usafirishaji, uzalishaji na usambazaji wa Dawa za Kulevya

3. Kuweka mazingira bora ya kazi na kuleta ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti ili Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 160,117,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Mwenyekiti majukumu makuu ya Tume ya UKIMWI ni kuhakikisha kwamba sera na mikakati ya taifa ya kupiga vita UKIMWI zinaandaliwa na kutekelezwa, kutafuta rasilimali zitakazotumika katika utekelezaji wa muitiko wa kitaifa wa kupambana na UKIMWI, kuimarisha uwezo wa wadau katika kufanyia kazi programu za UKIMWI na kuratibu shughuli zao, kushajihisha utoaji wa huduma za tiba na matunzo kwa watu walioathirika na kuathiriwa, kufuatilia na kutathmini umakini na ufanisi wa utekelezaji wa mikakati, sera na muitiko wa kitaifa na kutoa taarifa zote zinazohusiana na UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilijipangia malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha mazingira mazuri ya wafanyakazi wa Tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya UKIMWI.
2. Kuongeza uwezo wa programu za habari, utetezi na mawasiliano ili kuchochea mabadiliko ya tabia katika jamii na makundi maalum.
3. Kuimarisha Uratibu na Utekelezaji wa Sera na Sheria na Mkakati wa Taifa wa Pili wa kupambana na UKIMWI.
4. Kuongeza utumiaji wa taarifa zinazotokana na Ufuatiliaji, Tathmini na utafiti katika programu za UKIMWI.
5. Kusimamia utaratibu wa udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti hadi kufikia Mei 2013 Tume ya UKIMWI imeweza kutekeleza yafuatayo katika malengo iliyojipangia:-

Mhe. Mwenyekiti katika kuimarisha mazingira mazuri ya wafanyakazi wa tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya UKIMWI, stahiki za likizo kwa wafanyakazi 2 na malimbikizo ya mishahara kwa wafanyakazi 3 zimelipwa. Wafanyakazi 3 wanaosoma fani za Uhasibu (1), Uongozi (1) na Manunuzi (1) wamelipiwa gharama za masomo. Malipo ya huduma mbalimbali zikiwemo ununuzi wa mafuta kwa kurahisisha

ufuatiliaji wa kazi, matengenezo ya magari ya ofisi, malipo ya maji, ulinzi, umeme, mtandao kwa kurahisisha mawasiliano, vifaa vya kuandikia yamefanyika.

Mhe. Mwenyekiti ili kuhakikisha ufanisi katika kuongeza uwezo wa programu za habari, utetezi na mawasiliano kwa kuchochea mabadiliko ya tabia katika masuala ya UKIMWI, nyumba tano za makaazi ya vijana walioacha dawa za kulevya **(***Sober houses*) zimesaidiwa kwa kununuliwa televisheni na radio moja kila nyumba. Katika muendelezo wa kuelimisha makundi maalum kwa kuwatumia waelimishaji rika, idadi ya dada poa 307, kaka poa 38, na wanaojidunga sindano 271,wameweza kufikiwa kupitia katika mikusanyiko mbali mbali. Pia, taasisi za dini zimeweza kuhamasisha waumini wao wapatao 380 kupitia katika mikusanyiko ya kidini juu ya mbinu bora za kutumia huduma za kuzuia maambukizo ya UKIMWI, kupanua upatikanaji wa taarifa za afya ya uzazi pamoja na kuwepo kwa usawa wa kijinsia kuhusiana na elimu ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti Elimu ya UKIMWI inayohusu mpango wa kuimarisha uwezo wa jamii kupambana na UKIMWI *(Community Capacity Enhancement Programme – CCE*) imetolewa kwa shehia mbali mbali za Unguja na Pemba. Jumla ya shehia 21 zimeweza kufikiwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti jarida la JIHADHARI toleo nambari 16 limechapishwa na kusambazwa kwa wadau kwa lengo la kutoa habari kwa jamii. Maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani yamefanyika tarehe 1/12/2012 ambapo kilele chake kilifanyika Mangapwani, Wilaya ya Kaskazini B Unguja. Lengo kuu la maadhimisho hayo lilikuwa ni kuihamasisha jamii juu ya kujikinga na UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti katika kuimarisha uratibu wa shughuli za UKIMWI nchini, Tume imefanya mikutano ya uratibu kwa wadau mbalimbali ikiwemo taasisi za Serikali, taasisi zisizo za kiserikali, kamati za UKIMWI za Wilaya na Shehia, jumuiya ya wafanyabiashara, na taasisi za viongozi wa dini. Mikutano 12 (6 Unguja na 6 Pemba) imeweza kufanyika na kuhusisha watu 253. Mikutano hiyo imetusaidia kujua maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI zinazotekelezwa na taasisi hizo pamoja na changamoto zilizomo katika maeneo yao. Kwa kutambua umuhimu wa kupata taarifa kwa watu wenye mahitaji maalumu, mkakati wa mawasiliano na utetezi umechapishwa kwa lugha ya wasioona.

Mhe. Mwenyekiti katika kuendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Pili wa Taifa wa kupambana na UKIMWI, Mapitio ya Sheria ya Tume ya UKIMWI Nam. 3 ya mwaka 2002 yamefanyika na rasimu ya mswada wa marekebisho

yake yanatarajiwa kuwasilishwa kwenye kikao kinachofuata cha Baraza la Wawakilishi. Aidha, mapitio ya Sera yamefanyika, na rasimu ya Sera ya UKIMWI inaendelea kuandikwa kwa lugha nyepesi (*popular version*) ili kuifanya jamii na wadau wengine kuielewa na kuitekeleza kwa urahisi. Warsha ya siku mbili kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ilifanyika kwa lengo la kuwaongezea uelewa pamoja na kupata michango yao juu ya rasimu za sheria, sera na mkakati wa utetezi na mawasiliano. Pia, Tume imeandaa mkakati wa kutafuta rasilimali na tayari umewasilishwa kwa kamati ya wataalamu na kupatiwa maoni. Vile vile, warsha ya kuzijengea uwezo taasisi za Serikali na zisizokuwa za serikali juu ya namna ya kuingiza masuala ya UKIMWI katika mipango na kazi zao za kila siku ilifanyika, jumla ya watu 42 walishiriki katika mafunzo hayo kutoka Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti katika kuimarisha mwitiko wa jamii kupambana na UKIMWI, Tume imeweza kuzisaidia Shehia 22 kuibua mipango kazi ya UKIMWI na udhalilishaji wa jinsia kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, Tume imeendesha mafunzo ya wiki mbili kwa wakufunzi 15 juu ya programu ya kuzijengea uwezo Shehia jinsi ya kupambana na UKIMWI. Washiriki hao wametoka katika taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali na ndani ya jamii kwa ujumla. Tayari wameshaanza kazi za kuwafundisha wajumbe wa kamati za UKIMWI za shehia, Vile vile, Tume imefanya mafunzo kwa kamati za shehia 10 (6 Unguja, 4 Pemba) zinazosimamia programu za kuimarisha uwezo wa jamii kupambana na UKIMWI na udhalilishaji wa kijinsia, utetezi na haki za binadamu.

Mhe. Mwenyekiti katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia kwa vijana ikiwemo utumiaji wa dawa za kulevya, zinaa, wizi nk, Tume imetayarisha nakala rahisi ya kiongozi cha mafunzo ya mawasiliano kati ya mzazi na mtoto (*parent child communication guide)* kwa ajili ya kuwawezesha wazazi kuwa na mawasiliano na watoto wao juu ya afya ya uzazi na UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti utafiti wa mwisho uliofanywa wa HIV na Malaria umeonesha wanawake na wanaume wenye umri wa miaka 15-49 walifanyiwa uchunguzi wa damu kwa kupimwa maambukizi ya VVU na UKIMWI. Utafiti huo umeonyesha kwamba kiwango cha maambukizi ya VVU Tanzania kwa mwaka 2011/2012 kimepungua kutoka 5.7(Takwimu 2007) hadi 5.1, hii ni afadhali kidogo kwa Tanzania kwa ujumla. Lakini Kwa upande wa Zanzibar, kiwango cha maambukizi hayo kimepanda kutoka asilimia 0.6 (takwimu 2007) hadi asilimia 1, ongezeko hili kwa upande wetu ni kubwa. Hali hii inahitaji nguvu za pamoja kwa Serikali na wananchi wote kuhakikisha kwamba maambukizi zaidi yanadhibitiwa, taarifa kamili kwa mikoa yote 5. (Angalia kiambatanisho nam 9).

Mhe. Mwenyekiti jumuiya ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (ZAPHA+) ni moja kati ya taasisi za kiraia muhimu sana inayotoa mchango mkubwa katika mapambano dhidi ya UKIMWI. ZAPHA+ imejengewa uwezo juu ya mbinu za utafutaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuendeleza mbele mapambano dhidi ya UKIMWI. Kupitia Tume ya UKIMWI, ZAPHA+ wamepatiwa jumla ya TZS 551,471,765 na wahisani kwa kufanya shughuli zao za uratibu.

Mhe. Mwenyekiti ziara za ukaguzi wa ndani wa hesabu zimefanyika kuwatembelea wadau mbali mbali Unguja na Pemba kufuatilia na kufanya uhakiki wa mahesabu kwa wadau wanaopata fedha kupitia Tume ya UKIMWI Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilikadiriwa kutumia TZS 739,000,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo TZS 500,838,000 kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS 238,162,000 kwa ajili ya kulipia mishahara. Hadi kufikia Mei 2013 Tume ilikwisha kuingiziwa TZS 280,035,552 sawa na asilimia 56 kwa ajili ya kuendeshea kazi**.** Aidha, Tume iliidhinishiwa TZS 50,000,000 kwa kazi za maendeleo kutokana na mchango wa Serikali. Hadi kufikia Mei 2013, ilikwisha ingiziwa TZS 15,000,000 sawa na asilimia **30**. Kwa upande wa fedha za wahisani Tume ilikadiriwa kupatiwaTZS 893,760,000**.** Hata hivyo kutokana na kupata fedha zaidi kutoka kwa wahisani baada ya bajeti ilitarajia kupata 1,604,700,000**.** Hadi kufikia Mei 2013, jumla ya TZS 1,187,016,000 sawa na asilimia 74 zilikwisha kupatikana. (Angalia kiambatanisho namba 10).

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2013/14 imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuongoza, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mkakati wa Pili wa Kitaifa wa UKIMWI kwa wadau wote.
2. Kuimarisha ubora wa taarifa zinazokusanywa pamoja na kufuatilia matumizi ya taarifa zinazotokana na ufuatiliaji, tathmini na utafiti wa programu za UKIMWI.
3. Kutoa miongozo na kuratibu masuala ya habari, utetezi na mawasiliano kuhusu UKIMWI ili kuchochea mabadiliko ya tabia katika jamii na makundi maalum.
4. Kuongoza pamoja na kuimarisha mazingira mazuri ya kazi na wafanyakazi wa Tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu wa masuala ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti ili Tume ya UKIMWI iweze kutekeleza malengo iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 768,000,000 kwa kazi za kawaida, kati ya hizo TZS 510,714,700 kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS 257,285,300 kwa ajili ya mishahara. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya TZS 50,000,000 kwa kazi za maendeleo kutokana na mchango wa Serikali na TZS 1,719,000,000 kutoka kwa wahisani (rejea kiambatanisho namba 10).

SHUKURANI

Mhe. Mwenyekiti naomba niwashukuru kwa dhati kabisa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kuwa wasikivu na wastahamilivu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu. Ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wataendelea kushirikiana na Ofisi yetu katika kutoa michango mbali mbali ambayo itaiwezesha kutatua matatizo yanayoikabili jamii. Ofisi yetu itaipokea na kuifanyia kazi michango yote itakayotolewa na Wajumbe wa Baraza hili kwa maslahi ya Jamii na Taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti napenda kutoa shukrani zangu za kwa nchi marafiki, mashirika ya Kimataifa na watu binafsi kwa kuendelea kutusaidia kuendeleza shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nchi hizo ni pamoja na Marekani, Finland, Norway, Uingereza, Uholanzi, China, India, Qatar, Oman na Falme za nchi za Kiarabu. Pia mashirika ya kimataifa yakiwemo UNDP, UNICEF, UNFPA, UNAIDS, UNEP, UNODC, UNFCCC, WHO, World Bank, Taasisi ya Maendeleo ya Kimataifa ya Serikali ya Uingereza (DFID), AIHA, CDC, ICAP, *Save the Children* na nchi na mashirika mengine ambayo sikuyataja, lakini kwa njia moja au nyengine yanatuunga mkono katika shughuli zetu za maendeleo. Michango yao tunaijali na kuithamini.

Mhe. Mwenyekiti natoa shukurani za dhati kwa Taasisi mbali mbali za Serikali zikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama na taasisi zisizo za kiserikali zinazojishughulisha na masuala ya UKIMWI, mapambano dhidi ya dawa za kulevya, utunzaji na uhifadhi wa mazingira na kutetea haki na fursa za watu wenye ulemavu. Nawaomba waendelee kutupa mashirikiano kwa lengo la kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kufikia lengo kuu la kukuza uchumi na kupunguza umasikini. Aidha, napenda kuvishukuru sana vyombo vyote vya habari kwa kushirikiana nasi katika kuielimisha jamii juu ya athari za uharibifu wa mazingira, matumizi ya dawa za kulevya, namna ya kujikinga na VVU na UKIMWI na umuhimu wa kuwahudumia watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti napenda kutoa shukurani za pekee kwa watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Ofisi kwa mwaka 2012/2013 kama yalivyobainishwa katika hotuba hii. Napenda kumshukuru Makamu wa Kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, akiwa ndio kiongozi wa Ofisi yetu, kwa maelekezo yake kwangu na kwa watendaji na kuifanya Ofisi yetu iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa. Pia napenda kuwashukuru sana Katibu Mkuu, Dk. Omar Dadi Shajak, Naibu Katibu Mkuu, Dk. Islam Seif Salum, Afisa Mdhamini, Fatma Mohammed Omar, Wakurugenzi Watendaji na Wakurugenzi wa Idara na Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Watendaji wote kwa ushirikiano na kazi kubwa walioifanya katika kuandaa mpango na bajeti hii kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti mwisho napenda kuwashukuru wananchi wote kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu. Napenda kutoa wito kwa wananchi wote na waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kulinda mazingira na kujikinga na athari za mabadiliko ya tabianchi, kutetea na kulinda haki za watu wenye ulemavu, kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya na kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI inazingatiwa na inaendelea kupewa kipaumbele kwa manufaa ya Taifa letu na kizazi kijacho.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti kwa heshima nachukua nafasi hii kuwaomba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, watushauri, watuelekeze na hatimae kuidhinisha matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ya jumla ya shilingi Bilioni tatu na milioni ishirini (TZS 3,020,000,000) kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kati ya fedha hizo, TZS Bilioni moja milioni mia nane ishirini na moja (TZS 1,821,000,000) kwa ajili kuendeshea kazi na shilingi Bilioni moja milioni mia moja tisini na tisa (TZS 1,199,000,000) kwa ajili ya mishahara. Aidha naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya TZS Milioni mia moja na hamsini (TZS 150,000,000) kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali na **TZS** Milioni mianane **(**TZS 800,000,000) ikiwa ni mchango wa wahisani (angalia kiambatanisho namba 11).

Mhe. Mwenyekiti aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishie Tume ya UKIMWI matumizi ya jumla ya TZS Milioni mia saba sitini na nane (TZS 768,000,000) kwa kazi za kawaida, ambapo shilingi Milioni mia tano na kumi laki saba na kumi na nne na mia saba (TZS 510,714,700) kwa ajili ya kuendeshea kazi na TZS Milioni mia mbili hamsini na saba laki mbili na thamanini na tano na miatatu (TZS **257,285,300**) kwa ajili ya mishahara.

Aidha, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya shilingi Milioni hamsini (TZS **50,000,000**) kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali na TZS Bilioni moja milioni mia saba kumi na tisa (TZS 1,719,000,000) ikiwa ni mchango wa wahisani (rejea kiambatanisho Namba 11).

Aidha naliomba Baraza lako Tukufu likubali mchango wa jumla ya TZS 10,800,000 ikiwa ni mapato yaliokadiriwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu) Mhe. Mwenyekiti awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kukutana asubuhi ya leo katika Baraza letu hili Tukufu la wananchi wa Zanzibar ambao wametutuma kuja kuwatumikia.

Mhe. Mwenyekiti aidha nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya mwanzo baada ya Mhe. Waziri kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti naomba pia uniruhusu nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao ya dhati wanayoipa Kamati yangu wakati wote tunapotekeleza majukumu yetu kimsingi. Vile vile napenda kuishukuru Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuwasilisha mbele ya Kamati yetu pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2013/2014 ili yapate Baraka za Wajumbe wako watoe michango yao na baadae waipitishe kwa maslahi ya kuwatumikia wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti na sisi kamati yetu tunaungana na Mheshimiwa Waziri kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na wasaidizi wake wakuu Makamu wa Kwanza Maalim Seif Sharif Hamad pamoja na Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa uvumilivu wao na busara zao katika kuliongoza Taifa letu lenye mgawanyiko wa kambi mbili kubwa za kisiasa lakini kwa sasa wameweka mbele maslahi ya Taifa letu na kusahau tofauti zao za kisiasa, hili ni jambo la kuigwa kwa

kila mmoja wetu kwani wakati huu tunahitaji uzalendo na mshikamano mkubwa kuliko wakati mwengine wowote, kwani Taifa letu linapita katika mkondo mkubwa wa mabadiliko makubwa ya kisiasa na kimfumo wa kiutawala. Kwa hiyo, sisi kama viongozi tuliokula kiapo kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi wetu basi tumebeba dhima kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Hivyo, nawaomba wenzangu sote kwa pamoja na wananchi wetu tunaowaongoza kushikamana na kuwaunganisha wananchi wetu katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti lakini pia sitosahau kuwashukuru kwa dhati kabisa Wajumbe wa Kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya kazi zetu, na pia kwa wakati wote wa kupitia Bajeti hii kwa umahiri wameweza kufanya kazi kubwa na leo ndio tunawasilisha hapa Barazani maoni ya Kamati yetu, naomba niwatambue Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hamza Hassan Juma — Mwenyekiti
2. Mhe. Saleh Nassor Juma — Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Mzee Ali — Mjumbe
4. Mhe. Ashura Sharif Ali — Mjumbe
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk — Mjumbe
6. Mhe. Subeit Khamis Faki — Mjumbe
7. Mhe. Shadya Mohd Suleiman — Mjumbe
8. Nd. Rahma Kombo Mgeni — Katibu
9. Nd. Makame Salim Ali — Katibu

Mhe. Mwenyekiti baada ya Utangulizi huo, sasa kwa niaba ya Kamati yetu naomba uniruhusu tuwasilishe maoni yetu juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

OFISI YA FARAGHA:

Mhe. Mwenyekiti kiujumla Kamati yangu inaipongeza Wizara kwa kufanikisha vyema utekelezaji wa majukumu ya Mhe Makamu wa Kwanza wa Rais mbali na hali ngumu ya upatikanaji wa fedha inayoikabili nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti Pia Kamati inawataka Wahusika wote kuhakikisha kuwa ahadi zinazotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais kutekelezwa kwani kutotekeleza ahadi hizo pamoja na maagizo wanayoyatoa ni kuwadharaulisha mbele ya jamii viongozi wetu hao.

Pamoja na kusimamia ahadi za Makamu wa Kwanza wa Rais, kamati yangu inaishauri Ofisi kufuatilia ahadi na makubaliano yanayofikiwa baina ya Makamu wa Kwanza na viongozi, taasisi au mashirika mbali mbali pale wanapokwenda nje ya Nchi, au pia wanapojiwa na wageni katika ofisi yao.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Mwenyekiti Idara hii ina majukumu ya kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera na mipango ya maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kukusanya, kutunza takwimu, ufuatiliaji na tathmini ikiwa ni pamoja na kuratibu shughuli za utafiti kwa idara zote zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti tunaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa jitihada ilizozifikia katika kuandaa Mpango Mkakati wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kipindi cha miaka saba (2013 hadi 2020). Hili ni suala zuri na tunaiomba ofisi ya Makamo wa Kwanza kuhakikisha hiyo mipango ya miaka saba pia ipangiwe muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu na pia utekelezaji wake uende kwa malengo ya kipindi fulani ikiwa mradi umepangwa kufanyika kwa kipindi cha mwaka mmoja na ikiwa haukukamilika basi zitolewe sababu za msingi kwa nini haukukamilika hapo ndipo tutaweza kutekeleza majukumu yetu kwa kasi kubwa. Kwa hiyo tunataka tusikie je mpango wa kukimaliza kituo cha kurekebisha tabia kwa watumiaji wa madawa ya kulevya pale Tunguu kitamalizika lini?

Mhe. Mwenyekiti pia tunapongeza Mpango Mkuu wa Utafiti ambao umeainisha maeneo makuu yanayohitaji kufanyiwa utafiti katika kipindi cha miaka saba kuanzia 2013 hadi 2020.

Aidha Mhe.Spika, tunaipongeza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa jitihada ilizozichukua na mafanikio waliyoyapata katika suala la kutokomeza kunguru weusi ambao wamekuwa ni chanzo kikubwa cha uchafuzi na uharibifu wa mazingira katika nchi yetu. Tunaiomba Ofisi ya Makamo wa Kwanza Wa Rais kuendelea na jitihada za kuwatokomeza ndege hawa ili kuondokana na changamoto zao.

Mhe. Mwenyekiti Kamati imefarajika na jitihada ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kufanikiwa kutekeleza mradi wa elimu ya mazingira. Kamati yangu inapenda kusisitiza katika mradi huu kwamba umakini mkubwa unahitajika katika kuieleimisha jamii juu ya njia na mbinu za kuhifadhi mazingira. Changamoto iliyopo ni kuwaonesha njia nyengine mbadala katika kuhifadhi mazingira.

Miradi mingine Mheshimiwa Mwenyekiti ni pamoja na mradi wa majaribio wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, mradi wa kuingiza masuala ya watu wenye ulemavu katika mipango ya maendeleo, mradi wa Kujenga kituo cha Tiba na Marekebisho ya tabia kwa watumiaji wa dawa za kulevya huko

Tunguu ambapo kwa masikitiko makubwa mradi huu ulishindwa kuingiziwa fedha za kutosha katika mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti Vile vile kupitia idara hii Kamati inaiomba Serikali kuisaidia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais fedha za safari ambazo kwa sasa ni changamoto kwao na huwapelekea kukosa kuhudhuria vikao na mikutano mbali mbali nje ya nchi kwa kutokuwa na uwezo wa kusafiri jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada katika ufanisi wa kazi.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI:
Mhe. Mwenyekiti tunapongeza jitihada zinazochukuliwa na Idara katika kutekeleza majukumu yake vizuri ikiwemo suala la kuimarisha mawasiliano ya habari na kusimamia uratibu na udhibiti wa matumizi ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti licha ya majukumu makubwa ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuwapatia maslahi yao wanayostahiki, pia kukuza na kuimarisha mawasiliano ya habari, tunatoa pongezi maalum kwa kitengo hiki cha mawasiliano ya habari kwa kuandaa filamu fundishi ya watu wenye Ulemevu wanaoishi katika mazingira magumu. Filamu hii ambayo Mhe. Mwenyekiti ilioneshwa siku ya kuchangia Mfuko wa Maendeleo ya walemavu.

Mhe. Mwenyekiti kwa upande wa kusimamia utaratibu na udhibiti wa matumizi ya fedha. Mheshimiwa hii ni changamoto kubwa inayoikabili si Idara hii tu bali ni kwa Idara zote za serikali nzima, hivyo tunaitaka Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kutupia jicho la kipekee katika sehemu hii ili yasitokezee yale ambayo yalitokezea katika maeneo mengine hasa Mhe. Mwenyekiti kwenye miradi inayofadhiliwa na wafadhili au wahisani wa nje.

IDARA YA MAZINGIRA:
Mhe. Mwenyekiti pamoja na majukumu makubwa waliyopewa Idara hii na nchi ya kuhakikisha mazingira katika nchi yetu yanahifadhiwa lakini bado kuna mapungufu mengi ya kisheria yanayokwamisha jitihada za Idara husika katika kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na hatimaye kuikosesha Idara na Serikali kwa ujumla mapato. Bado Idara hii Mheshimiwa Spika inashindwa kuchukua hatua za kisheria za kumuadhibu yule anayeharibu mazingira iwe kwa makusudi au kwa bahati mbaya.

Mhe. Mwenyekiti kwa ufupi Idara hii haina nguvu za kisheria katika kufanikisha kazi zake. Kwa hiyo inabidi yapatikane mashirikiano na idara nyingine kwa yale maeneo ambayo kuna uharibifu wa mazingira ili kuangalia ni sheria gani ya kudhibiti itumike ili kuzuia kuendelea na uharibifu wa mazingira, na kuepuka kila mmoja kukwepa lawama na huku tunaharibikiwa.

Hivyo, tunaiagiza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuwasilisha haraka iwezekanavyo hapa Barazani Marekebisho ya Sheria ya Mazingira ili kuipa nguvu Idara kuweza kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaokiuka sheria hizo. Aidha tunaiagiza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kupitia Idara ya Ardhi ili kuhakikisha kuwa sheria zao zinafanya kazi ipasavyo kwa lengo la kwenda sambamba na utunzaji wa mazingira.Mhe. Mwenyekiti, tunalitaja hili kwa sababu ardhi na mazingira ni watoto pacha na mmoja akienda kinyume na mwenziwe basi hali huwa ndivyo sivyo.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati yangu bado inaisisitiza serikali kupitia Idara hii kuhakikisha kuwa hairuhusu utekelezaji wa mradi wowote kabla ya kufanyiwa tathmini ya kimazingira na kupewa kibali na Idara hii. Pia tunaishauri serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na mawasiliano ambayo inaongoza kwa kuharibu mazingira kwa kuchimba mashimo makubwa wakati wa ujenzi wa barabara, hatukatai wasichimbe mashimo lakini yawe na kiasi, lakini vile wafuate ushauri wa maazingira, kwani sote tunaelewa umuhimu wa barabara lakini pia tuelewe mara mbili zaidi umuhimu wa kuhifadhi mazingira ya nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii wapatiwe asilimia kumi (10%) ya kufidia uharibifu huo wa mazingira kutoka Wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti**,** Kamati inaunga mkono hatua zinzochukuliwa na Idara katika kuandaa rasimu ya kanuni ya kupiga marufuku uingizwaji na udhibiti wa bidhaa chakavu za umeme kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa mazingira. Kukamilika kwa rasimu hii itakuwa ni mwanga mzuri wa nchi juu ya suala hili. Aidha wazo la kuweka viwango mbali mbali badala ya kupiga marufuku moja kwa moja sio baya, lakini Idara iwe makini sana na suala hili kwa sababu hapa kwetu Zanzibar ni wazuri sana wa mipango lakini kwa bahati mbaya ni wabovu mno na wazito kwenye utekelezaji wa mipango yetu. Tunapenda kutahadharisha kwamba tusipokuwa makini na waangalifu basi Zanzibar itakuwa jaa la kila kila mwenye makachara yake kuja nayo kuyatupa kwetu. Kamati yetu inaishauri Idara kuharakisha kanuni hiyo na pia kabla ya kuchapwa basi ni busara kuzitambulisha japo kwa kamati yako ambayo inasimamia sekta hii ya Baraza la Wawakilishi, Kamati ya Ofisi ya Kusimamia Watendaji Wakuu wa Kitaifa na kuiongzea nyama au kutoa ushauri wao kwani kanuni hizo ndizo zinazotoa miongozo na tafsiri nyepesi katika utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaridhishwa na Idara ya Mazingira kwa kudhibiti suala la uingizwaji na matumizi ya mifuko ya Plastiki hapa Zanzibar, lakini bado tusibweteke kwani bado kuna watu wanaojaribu kuiingiza kwa siri ambao wanaweza kurudisha nyuma jitihada za Idara hii.

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati aidha inaipongeza Idara hii kwa kusimamia uingizwaji wa masuala ya mazingira katika miradi ya maendeleo ambapo jumla ya miradi 65 ya hoteli imekaguliwa, miradi 15 ya uwekezaji imefanyiwa tathmini ya athari za kimazingira na kutolewa vyeti vya kimazingira na miradi 5 imefanyiwa uchunguzi wa awali wa kimazingira ili kutoa hadidu rejea za kufanya tathmini za athari za kimazingira. hapa tunapenda kukumbushia kwamba haitoshi tu kufanya tathmini ya mazingira bali kuhakikisha ripoti hizo zinafanyiwa kazi kuingana na matokeo yatakavyojionesha.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaikumbusha Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kuipatia vitendea kazi vya kutosha Idara ya mazingira hususan suala la usafiri wa kutosha kwa ajili ya kufuatilia masuala ya uharibifu wa mazingira. Aidha kamati yetu itaendelea kushauri na inaona kabisa kuna haja kubwa kwa idara hii kujengewa jengo la kisasa linaloendana na Idara yenyewe na umuhimu wake katika suala zima la kutunza mazingira. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Idara ya Mazingira iliopo Maruhubi kwa kweli hailingani na Idara hii na majukumu yake.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU:

Mhe. Mwenyekiti**,** kamati inaipongeza serikali kwa kutambua umuhimu wa watu wenye Ulemavu pamoja na changamoto zinazowakabili. Kamati kwa upande wake pia inazikumbusha taasisi zote za serikali ikiwemo Baraza la Wawakilishi pamoja na taasisi binafsi kuitekeleza sheria inayowahusu watu wenye ulemavu kwa kujenga au kuyafanyia marekebisho majengo yao ili yawe na mazingira mazuri na rafiki wa kuweza kutumika na watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti**,** masuala ya watu wenye Ulemavu yanamgusa kila mmoja wetu na hasa ikizingatiwa kwamba kila mmoja wetu wakati wowote ule anaweza kupata ulemavu kutokana na sababu mbali mbali. Hivyo ni vyema kwa serikali kuhakikisha kuwa sheria zinazopitishwa na Baraza pamoja na ile mikataba ya Kimataifa kuhusu watu wenye Ulemavu inatekelezwa kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la udhalilishaji kwa watu wenye ulemavu bado ni changamoto kubwa katika nchi yetu. Kuna baadhi ya watu huwabaka kwa makusudi watu wenye ulemavu na kesi zinapofikishwa kunakohusika huambiwa hakuna ushahidi au ushahidi hucheleweshwa kwa makusudi kwa lengo la kuharibu kesi. Mhe. Mwenyekiti, hali hiyo hupelekea jamii kukata tamaa kwa wabakaji kuendelea kutamba mitaani na kuendelea kuwabaka watu wenye ulemavu na kuongeza mzigo katika familia na jamii za watu hao wenye ulemavu. Kwa upande mwengine familia inayoathiriwa kwa kubakwa

mtoto wao, kutokana na kupoteza imani kwa vyombo vya sheria, huchukua hatua mikononi mwao kwa kulipiza kisasi cha aina yoyote ile ilimradi familia hiyo ijiridhishe kutokana na ovu alotendewa mtoto wao.

Mheshimiwa Spika**,** kamati yetu inaiagiza Idara ya Watu wenye ulemavu pamoja na Jumuia ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar kushirikiana na taasisi zinazohusika na masuala ya sheria pamoja na Tume ya Haki za Binaadamu ili zipatiwe msaada wa kisheria na haki za Wenye Ulemavu pale inapohitajika.

Mheshimiwa Spika, kamati pia kwa mara nyengine inaitaka serikali kuchukua hatua za haraka kwa kununua vifaa vya kupimia DNA kwa lengo la kuondosha kero za ucheleweshwaji wa majibu hasa pale inapotokezea kesi za ubakaji kwa watu wenye ulemavu na kupunguza sababu ya kukosekana kwa ushahidi.

Mheshimiwa Spika kamati inaona kuna haja ya kuangaliwa upya sheria zinazowahusu watu wenye Ulemavu hususan katika vitendo vya udhalilishaji na ubakaji ili kuhakikisha kuwa sheria zinawabana zaidi wabakaji na wale wote wanaoharibu ushahidi katika kesi za udhalilishaji na ubakaji kwa watu wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kamati yangu inaipongeza kwa dhati kabisa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kufanikiwa kuanzisha mfuko maalum wa watu wenye ulemavu. Hata hivyo kuna haja ya kuendelea na kuuendeleza mfuko wenyewe ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufikiwa.Aidha tunaishauri Ofisi husika kuhakikisha na kusimamia vyema fedha hizo ili ziweze kuwanufaisha walengwa waliokusudiwa.

TUME YA KURATIBU NA KUDHIBITI DAWA ZA KULEVYA:

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza Tume hii kwa kazi kubwa na ngumu wanayoifanya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kupambana na kuzuia dawa za kulevya. Pamoja na jitihada hizo bado kuna changamoto nyingi zinazoikabili Tume hii pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuwa na uhaba wa vitendea kazi, pesa za mafuta pamoja na mafunzo. Hivyo Kamati yangu inaiomba Serikali kuiwezesha Idara hii pamoja na Jeshi la Polisi kwa kuzipatia vitendea kazi vya kutosha yakiwemo magari na fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, tunawapongeza wale wote waliojitolea katika kuanzisha nyumba za kurekebisha tabia *sober houses* kwa lengo la kuwasaidia kuwarejesha kwenye hali ya kawaida wale waliojiingiza kwenye janga hili la utumiaji wa madawa za kulevya. Aidha kwa mara nengine tena tunaipongeza

Serikali kwa kuandaa muongozo wa kuanzisha na kuzisimamia *sober houses* hizo hapa Zanzibar. Lakini katika hili Mhe. Mwenyekiti, bado kuna tatizo kwani fedha wanazoingiziwa za shilingi milioni moja na nusu kwa mwaka ni chache mno. Hivyo tunaiomba serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuliangalia kwa upana zaidi suala hili la kuwasaid hawa wananchi walioanzisha hizi *sober houses.*

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inatoa tahadhari kwa serikali na jamii kwa ujumla kwani kiwango cha watumiaji wa dawa za kulevya kimekuwa kikiongezeka siku hadi siku. Hali hii si nzuri kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu na ustawi wa jamii kwa ujumla. Hivyo tunatoa wito kwa serikali nzima pamoja na jamii kwa ujumla kulichukulia suala hili kwa umakini zaidi na kulipa umuhimu unaostahiki kwa kuwafichua wale wote wanaojihusisha kwa njia moja ama nyengine katika biashara hii haramu ya madawa ya kulevya.

Kamati yangu inalisema hili kwa kutambua ukweli kwamba *fimbo moja haiui nyoka*. Hivyo ni wajibu wetu sote kushirikiana na taasisi husika katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Elimu bado inahitajika kutolewa zaidi ili kuona kwamba kila mmoja wetu anaelewa ukubwa wa tatizo hili lilivyo ili aweze kushiriki kikamilifu katika mapambano haya.

TUME YA UKIMWI:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada zinazochukuliwa na Tume hii katika kupambana na suala hili la Ukimwi. Jitihada hizo zimesaidia kudhibiti ongezeko la maambukizi mapya.Hata hivyo,tunaiombaTume kuendelea kushirikiana na jumuia zote zinazohusika na masaula ya Ukimwi ikiwemo ZAPHA+ kwa malengo yale yale ya kuzisaidia kwa hali na mali katika harakati zao za kujiendeleza kiuchumi na kijamii lakini pia katika kupamba na maambukizi mapya ya ukimwi. Aidha tunapenda kutoa wito kwa Serikali kusaidia miradi mbali mbali iliyo chini ya jumuia hizi hasa jumuia ya ZAPHA+ ili kuweza kuwajengea uwezo. Mhe. Mwenyekiti, pia tunamuomba Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuwatembelea kadiri itakavyowezekana kwa lengo la kuwahamasisha na kuwajali katika harakati zao za kujiendeleza kiuchumi. Mhe. Mwenyekiti, hapa tunatoa pongezi zetu za dhati kwa sababu kazi hiyo tunaiona Mhe. Waziri, pamoja na Mhe. Makamo wa Kwanza wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, pia tunaiomba serikali kutenga fedha maalum kwa ajili ya mapambano dhidi ya maambukizi ya Ukimwi kwani wafadhili wanaochangia masuala haya ya Ukimwi si wa kuwategemea sana, na katika hili Mheshimiwa Spika waswahili wanasema *Abebwaye hujikaza*! Hivyo basi tunatoa wito kwa Serikali kuanza kuweka mipango ya kujitegemea ili

wafadhili watakapotuacha mkono tuweze kuendesha mambo yetu sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Aidha kamati yangu inashauri na kutilia mkazo juu ya suala la kutoa elimu kwa wananchi juu ya maradhi haya ya Ukimwi. Wala tusiridhike na kuona kuwa kila mtu anaelewa ukimwi unapatikana vipina unapatikana wapi, bali mkazo uelekezwe kwenye kutoa takwimu zinazoendana na wakati kwa kuzingatia usahihi wake ili wananchi waweze kujua hali halisi ya maradhi yalivyo kama alivyokutoa Mhe. Waziri, muda mchache uliopita. Takwimu ambazo bila ya shaka yoyote zitasaidia katika kutoa dira si kwa jamii tu bali pia kwa Serikali juu ya nini cha kufanywa na mkazo uelekezwe wapi.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia majukumu makubwa ya Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo ni kupambana na uharibifu wa mazingira, suala la dawa za kulevya na mapambano yake, na suala la maradhi haya ya UKIMWI basi ni vyema kabisa kwa serikali kuhakikisha tunafanya kila jitihada inawaongezea bajeti ya Wizara hii kila hali inaporuhusu na kuwaingizia fedha zao kwa wakati ili malengo yao yaliyokabidhiwa Ofisi hii yaweze kutekelezeka kwa ufanisi. Kinyumme chake itakuwa ni sawa na *kutamani keki huku tunaogopa kuvunja mayai!*

Mhe. Mwenyekiti**,** kwa kumalizia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais inakabiliwa na tatizo kubwa la ufinyu wa nafasi katika Idara na Ofisi mbali mbali za Ofisi hii kwa upande wa Unguja na Pemba hali ambayo ni changamoto kubwa kwao katika mazingira ya kazi. Hivyo, tunaiomba Serikali kuliona hili kwa kuwatengea fedha zitakazosaidia kutatua tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijamaliza hotuba yangu hii nilikuwa naomba na mimi nikiwa kama Muwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura kwambanitoe mchango wangu wa mawazo kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti, nimezungumzia sana suala la mazingira katika hotuba yangu, lakini bado inaonekana kuna baadhi ya wawekezaji wanaendelea kuvunja na kukiuka sheria za mazingira. Sasa ninamuomba sana Mhe. Waziri, pamoja kwamba sheria yetu ya mazingira ina ufinyu katika maeneo mbali mbali na mmo katika kufanya marekebisho mbali mbali, kwa hivyo tunakuomba sana Mhe. Waziri, Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwako tunamuomba sana kushirikiana na Waziri mwengine yeyote ambaye ana sheria katika Idara zake mbali mbali ambazo anaweza akazitumia katika kuhifadhi na kulinda mazingira yetu, lakini vile vile kuwabana wale watu ambao wanaoharibu mazingira kwa makusudi.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu kamati ambayo iliyopita kabla hii kamati mpya, tuliwahi kutembelea Skuli ya Kisiwandui pale, kwa bahati Mhe. Mwenyekiti, Skuli ile wanasoma watoto wenye ulemavu na wenye ulemavu wa akili na viungo na ulemavu wa aina mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe ulikuwa shuhuda tulipokwenda pale kwa kweli unapoingia katika Skuli ile imani kwa kweli itakujia imani kubwa kwa sababu watoto wanaosoma pale ni wadogo sana na wengine umri wa kati na wengine ni wakubwa. Lakini kutokana na ulemavu wao Skuli ile wakati wa mvua na hasa mvua za masika, skuli ile ile kwa kweli inajaa maji.

Kwa hiyo ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, ashirikiane na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Baraza la Manispaa, kuweza kuliangalia eneo lile la Skuli ya Kisiwandui. Kwa sababu tatizo lililokuwepo pale wale watoto wenye ulemavu wa akili, wenye ulemavu wa viungo, watoto wadogo, skuli wakati wa mvua inapojaa maji kuna hatari ya kuja kutumbukia katika maji wakaja wakapoteza maisha. Sasa nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri hawa waitembelee Skuli ile waonane na walimu wale mimi naamini katika hii miradi yetu basi naamini tunaweza tukaangalia uwezekano wa kuweka njia ya kuweza kuyatoa maji kwa haraka hasa wakati wa mvua zinaponyesha katika eneo lile.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa namalizia katika eneo la madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, tulitembelea China hivi karibuni, China ina watu karibu 1,400,000,000, sisi tulifikia katika mji ambao una wakaazi hawapungui 10,000,000. Lakini kwa bahati tulipokuwa tukitembea mjini na tulijitahidi sana kutembea mjini tena kwa miguu, lakini hatukukutana na watu wanaosinzia wakatoka udenda kwa ajili ya madawa ya kulevya. Sasa hii inatokana na nini?

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu tunawajua hawana masihara katika utekelezaji wa sheria. Tumetunga sheria hapa ya mihadarati na mambo mengine yanayohusiana na madawa ya kulevya na katika sheria tuliyoitunga Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu kinachosema mtu yeyote atakayekamatwa na madawa ya kulevya basi anafilisiwa mpaka kile kitu ambacho kama mfano gari, yaani kitu chochote ambacho alichokutikana nacho pamoja na ule mtaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na orodha yote inayotajwa watu waliokamatwa na madawa ya kulevya lakini bado hatujasikia mtu akafilisiwa, bila ya kufuata sheria tunazozitunga hapa Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya tutaendelea kuimba nyimbo lakini yataendelea kuletwa. Kwa hivyo naomba sana Mhe.

Mwenyekiti, suala hili lisiwe la Waziri peke yake au la Serikali peke yake, wananchi tuweze kutoa taarifa kuweza kuisaidia Serikali, lakini vile vile kama kuna viongozi au kama kuna watendaji katika jeshi la polisi wanashirikiana na hawa wanaoleta madawa ya kulevya basi waweze kufichuliwa ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa ili tuweze kuliondoa tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wanaathirika na madawa ya kulevya, vijana wa kutegemewa sasa hivi wamekuwa hawana akili, wanasinzia wanatoka udenda ovyo kwa kweli suala hili inabidi tulipige vita kwa pamoja.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, ninaomba sasa kuwaomba Wajumbe waichangie hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais na waweze kutoa michango yao na mawazo, wakosoe pale pa kukosoa, washauri pa kushauri lakini baadae tuipitishe kwa pamoja ili tumpe nafasi Mhe. Waziri, mwanamke jasiri aweze kutekeleza majukumu yake aliyokabidhiwa na Mhe. Rais.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja naomba ninywe maji.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi hii asubuhi hii leo kutia barka Wizara hii ambayo inaongozwa na mama mwenyewe, kwa hivyo niitakie baraka kwanza kabla sijaanza kuchangia katika michango yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikisifu sana hichi kitabu chake kimepangika vizuri na inavyoonesha amejipanga vizuri hasa na hawa wataalamu wake aliokuwa nao, na hasa mama mwenyewe kuwa *smart*, kina mama wamekupeni hongera sana, ujasiri aliokuwa nao mama huyu na kuonesha ufanisi wake mkubwa sana kusoma hotuba bila ya kuterereka.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchangia katika ukurasa wa 7, katika Ofisi ya Faragha. Ninaomba kidogo Mhe. Waziri, anisaidie hapa kichwa kinanigonga kuwa Ofisi ya Faragha hii ya Makamu wa Kwanza na wa Pili kwa nini yake yeye imekuwa na wakati yule ni mtendaji, kidogo naomba hapa anisaidie kunifafanulia. Inavyoonesha ananitolea macho hajanisikia. Naeleza hivi Mhe. Mwenyekiti, nikisema sana mtu anakuwa hasikii leo ninasema kwa sauti ya chini ya upole sana.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kuwa hii Ofisi ya Faragha imechanganywa na Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili kuwa Makamu wa Pili na yeye ameekwa ndogo kuliko yake imekuwa kubwa kidogo anisaidie maarifa hapa ili akili yangu ikae sawa, nafikiri atakuwa ameshanielewa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini niulize zaidi ningemuomba kidogo anisaidie *data* hizi za Makamu wa Kwanza jinsi ambavyo anavyosafiri nje katika vipindi vingapi na katika vipindi hivi kipi kilichotupa faida katika utekelezaje wake wa kazi na sasa hivi ninasikia yuko nje sasa sijui kenda kiserikali au kwa matibabu atakuja kunieleza hilo. Mwenzangu mmoja aliuliza katika Ofisi ya Makamu wa Pili yeye hakupewa jibu, sasa mimi ninaomba hili nipewe jibu ya kuwa viongozi wetu wanapokwenda hii *cost* yao wanatumia kiasi gani na faida yao tuone kiasi tunanufaika wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia ukurasa wa 17, kuhusu habari ya mradi wa ujenzi wa kituo cha tiba kurekebisha tabia na utumiaji wa madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kituo hichi kiweze kuharakishwa kwa nguvu zote kwa sababu hali halisi iliyokuwepo kama alivyosema Mwenyekiti wangu vijana wanatupotea kabisa, na kuna tatizo kubwa sasa hivi utakuta mtu akikosa kete moja basi anakwenda kumuua mtu au kumnyang'anya au kumfanya lolote ili aweze kupata kete, hilo nalo moja linatupa tabu sana sana. Naomba sana Mhe. Waziri, ujenzi huu wa kituo ajitahidi sana na Mhe. Waziri wa Fedha, ajitahidi kumuongezea fedha ili aweze kutumia hizi fedha kwa wakati unaotakiwa ili kuweza kufikisha ujumbe wangu niliokusudia.Hapa mimi sitakuwa na mkazo mkubwa isipokuwa nasema Serikali iangalie zaidi kuhusu suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, naingia ukurasa wa 22, suala la mazingira. Suala la mazingira mimi sina utata nalo mkubwa sana, lakini ningeomba sana Mhe. Waziri, aangalie sheria haraka sana za kuwasaidia watu wa mazingira, kwa sababu kuna mambo ambayo yanafanyika anashindwa yeye Mkurugenzi kuchukua hatua za kisheria kwa sababu huwa bado sheria haijampa meno ya kuweza kutafuna yale mambo ambayo anayaona yanaharibika lakini sheria haimpi *power*, hili ningeomba sana Mhe. Waziri, simamia mjasiri mama, simamia Waziri wetu ili sheria haraka haraka iwepo.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana hawa wataalamu wake ambae ni Mkurugenzi mwenyewe pamoja na wataalamu wake wamejaribu kupitapita sana katika sehemu, kama hizo sehemu za fukwe lakini sheria zinawabana, na hawawezi masikini ya Mungu kusema kweli, wanaona sehemu michanga inachimbwa lakini hamna kitu kinachopatikana, pengine labda ushirikishwaji wao ni mdogo sana katika haya maamuzi, sasa hawa kwa kweli tunawapa unyonge sana wakati hawa ni wataalamu ambao ni wataalamu hasa waliosomea jinsi gani ya mazingira na kuyatengeneza na kuyaboresha. Kwa kweli hili suala linatia unyonge sana. Na ningependa sana Mhe. Waziri, sasa tungekuwa na wigo au tungekuwa na *special program* tungekuwa tunapita katika Shehia zetu au katika majimbo yetu wataalamu au kwa kila katika

Wilaya kama wapo au hawapo ningeomba hawa Maafisa washushwe pale kiwilaya au kimkoa ili wao wana-*rotate* ya kuweza kupita kule katika maeneo yetu, kwa sababu kuna wengine wapo *very interested* na masuala ya mazingira, lakini kinachokosa ni wataalamu wa kuwapata ili kuwaweza kuwajengea uhai wa kujua mazingira nini maana ya mazingira na sheria zinasemaje katika mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala lingewezekana na linawezekana hasa likitiwa msititizo kwa sababu siku hadi siku mambo yanazidi kuharibika yanazidi kuchafuka, tunakosa kutokana na taaluma hizo, wananchi tunaambiwa wajikusanye kwa misingi hiyo ya kuweka mazingira lakini hatimae inakuwa *nothing* kwa sababu hawapati usaidizi uliokuwa mzuri wa kitaalamu. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri, tusiwe na tabia ya kuwaondoa Kusini tukawapaleka Kaskazini, mimi naomba sana tuwe na wigo hawa au tuwapeleke nchi za aidha nchi hizi za *West African* hapo tuwapeleke tuwaangalie wa-*quote* ni jinsi gani wenzetu wanavyozuia uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mwenzetu hapa ameeleza kwamba amekwenda China. Mhe. Mwenyekiti, China mi sijaenda lakini nasema kuwa suala la mazingira limepewa kipaumbele mkubwa sana, ni kosa kubwa sana kama utaharibu mazingira, mjiti mmoja nasikia ukiukata basi mara wanaku-*kill*, kwa sababu gani ufuate sheria ya ukataji na ule mjiti unapoukata unatakiwa uusimamie mpaka ukue ushike, lakini sisi leo hatuna sheria hizo. Sasa nikisema Mhe. Mwenyekiti, hata na mimi nimekwenda katika nchi moja hapo jirani Austria hapo wana sheria zao nao vile vile jinsi ya kuhifadhi misitu yao au miti yao kutokatwa ovyo ovyo, sasa haya mazingira kama haya vipindi vyetu tungekuwa tunavitoa nje.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na bajeti yake finyu Mhe.Waziri, lakini ninamuomba aombe na namuomba sana awe na *special fund* yeye kutafuta kwa *donars* aombe kwa kuwatoa wanavikundi katika majimbo yetu kuwapeleka nje ili kuweza kufanikisha masuala haya, vyengine vyovyote itawekwa sheria itakuwa ni bure tu. Nazihurumia sana fedha za Serikali kuharibika bure bila ya kupatikana mafanikio. Ninaomba sana Mhe. Waziri, kwa hili ujitahidi sana ili tuweke katika mazingira mazuri, kwa sababu mazingira ni suala kubwa sana katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kuna masuala haya ya kuwa jinsi gani wananchi tunaweza tukawa-*plan* kutokata kuni ili kwa kuingizia suala ambalo litaweza kuweza kupata jiko lenye manufaa ili kuni isitumike tena kwenda kukata nalo hilo tulione sana. Mhe. Mwenyekiti, kuna wawekezaji, hawa wawekezaji hivi sasa katika nchi yetu kisiwa chetu kizuri sana na ndio maana

wawekezaji wengi wanakuja kutaka kutuletea maendeleo, lakini bado Waheshimiwa wakubwa hamjaliona hilo suala, kuna muwekezaji anataka kuweka mambo ya gesi itakuwa *very cheaper* kabisa, ili ingeweza huyu mkata kuni ataweza kuimiliki ile gesi, ninaomba sana Mhe. Waziri, muwekezaji huyu mumpokee na mumpigie debe apate *land* ambayo kwa mujibu wa sheria ile iwe karibu na pwani, ili iwezekane kwa sababu watu wanatandika mabomba, mabomba yale yanatoka kwenye bahari yanaingia kwenye kiwanda chenyewe moja kwa moja na kuweza ku-*dilute* na kufanya mambo ambayo yanatakiwa nalo hili litatusaidia mambo matatu makuu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza itatusaidia kupata pato kubwa katika Serikali, la pili kupata ajira kwa wananchi lakini la tatu tunaweka mazingira mazuri watu msitu hawatoukata tena. Mambo kama haya Mhe. Waziri, ninamuomba sana awe mbunifu, ili anikubalie kabisa aweze kulisimamia hili suala liwe ni moja katika ujasiri ataonesha, kwa sababu kina mama ndio wengi sana wanakimbilia kukata miti kwa ajili ya kuni. Sasa ujasiri wake Mhe. Waziri, awa-*control* wale kina mama kwa kuwatafutia kitu ambacho watafurahika nacho, watakijali, watakipenda na watakipokea na wala wasijisikie unyonge, kwa sababu mambo inawapunguzia masafa ya kwenda mwituni, mwituni unajua siku hizi kuna watu wanabaka, kuna mijiti ambayo unaweza ukajikwaruza, unaweza ukakuta nyoka, sasa hii ni njia moja ya kuondoa matatizo haya kwa kuleta viwanda ambavyo vitakavyoweza kuleta gesi asilia uipigie debe hiyo tuweze kuchimba gesi yetu asilia kama wenzetu Bara wanavyochimba, nayo ni moja hiyo uwe na *plan* Mhe. Waziri, basi upigie debe hiyo na sisi tuweze kumiliki gesi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tunaweza tukaanzia viwanda kwa sababu uchimbaji wa gesi si masihara kwa leo na kesho inaweza ikachukua maika 10 mimi na wewe hatujaweza kwenda kuchimba isipokuwa ni mwanzo vifunguliwe hivi viwanda, baadae ikishakuwa tayari kuchimba itakuwa kwake ni rahisi viwanda ushakuwa navyo tena hutafuti tena viwanda kwa sababu tayari umeshakuwa navyo. Ninaomba sana Mhe. Waziri, hili ulifanyie kazi kwa uangalifu sana ili tuweze kupata manufaa yetu katika nchi yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, niingie katika Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mimi ninajaribu sana mpaka sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, nimo katika kutafuta lugha fasaha ambayo nisitamke neno la walemavu bado Mhe. Mwenyekiti, sijaipata hiyo lugha lakini *Inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu naweza kuipata. Kwa sababu naona shida sana jambo la Mwenyezi Mungu kumpa mtu mapungufu ya viungo labda niseme hivyo, lakini nikisema mtu mlemavu ninahisi vibaya sana. Sasa naomba Mhe. Waziri hilo moja anitafutie njia hiyo ili tuweze kuweka sana na kuweza kuwasaidia hawa.

Lakini niseme pia Mhe. Mwenyekiti, nia yetu kwa ukweli niseme sina, maana yake unajua kuna lugha ukizisema unaambiwa aaa, Mhe. Makame Mshimba mchochezi na nini hata kama ni kweli lakini mtu anaigeuza ile lugha. Kwa sababu anaona ukisema ukweli unamu-*affect* yeye yule ambaye unamwambia. Lakini kinyume chake atafanya angalau watu waone kuwa Mjumbe kuwa nimeipotosha na kumbe si kweli, wenyewe wananchi wanajua, wanaona, Mhe. Mwenyekiti, walemavu bado hatujawatendea haki.

Walemavu bado hatujawatendea haki kwenye maeneo mengi, ukija kwenye ajira takwimu yao itakuwa ni ndogo sana na watu waliokamilika viungo. Sasa hilo nasema Mhe. Mwenyekiti, kwamba hata majengo yetu ni machache mno ambayo tunawarahisishia njia za kuweza kupita wao. Nalo hili tulione.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, twende kwenye ujasiriamali, utakuta na wao hatujawawekea hasa *fund* ambazo zinaweza kuwasaidia na kuwagomboa kutokana na hali yao ya upungufu wa viungo ili kufanya mambo yale wanayoweza kuliko kutaabika. Halafu isitoshe kuna wengine wanakwenda ovyo, sijui serikali ina mpango fani kwa wale wanaokwenda ovyo, tutawalinda vipi wale kitaaluma, pengine wana tatizo la akili au wengine kutokana na ukali wa maisha anaona bora atembee tu mara kwa mara au vipi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha mwaka jana tulipitisha fungu la shilingi milioni mia tatu, pesa hizo kama nitakosea Mhe. Waziri kwa upole kabisa naomba uje unijibu kwa utaratibu hasa mimi nilivyoizowea Mhe. Waziri wizara yako hiyo naipenda sana na mko wazi na hasa wewe mwenyewe Waziri uko wazi katika utendaji.

Mhe. Mwenyekiti, tulipitisha fungu la shilingi milioni tatu lakini la kushangaza mpaka leo hii Mheshimiwa tumeambiwa *tender* imeshatolewa, ningefurahi sana leo Mhe. Waziri ningemsikia kunieleza kuwa *tender* ile kama tulivyoeleza kwenye ripoti yetu ya Kamati imeshatolewa na sasa imefikia asilimia 60 hivi au 70 ya kuwa vifaa vya walemavu kuwa tayari.

Samahani sana Mheshimiwa sitaki kwenda moja kwa moja nitie kitu kinaitwa *yaumu shaka*, kwa sababu kitu kilichokuwa kina mashaka mashaka mtu nafsi yake hata kama mimi inanilinda. Kwa sababu *yaumu shaka* ni kitu ambacho sitaki kusema pasi na kuwa na uhakika utanisaidia wewe.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme pesa zimetumika hasa shilingi 16 milioni kununulia vifaa, na vifaa hivyo mnaviitaje sijui, dawa zimeshapelekwa sijui kama kweli au vipi, lakini dawa zimekuwa *very expensive* kutokana na hali halisi ya wakati tulionao, *three hundred* na kuna *one thousand five hundred*.

Sasa sijui ipi sahihi katika hizo. Mhe. Mwenyekiti, naomba hii *expensive* sijui kikoje hiki kitu.

Mhe. Mwenyekiti, hebu aje kunambia hapa Mhe. Waziri sitaki nimzuilie fungu akinipa maneno mazuri, sina historia nayo mbaya Mhe. Waziri kumjibu maneno ya ufedhuli hilo niseme ukweli, mtu haki yake mpeni wala simpi kutokana labda na alivyo aa. Kutokana na hali halisi ilivyo ni lazima niseme ukweli kwa sababu bado anawajali hawa walemavu, lakini bado kuna watu ambao bado wakorofi watakuwa ndani ya miongoni mwao watu hawa wanataka kuwadhalilisha walemavu hawa. Mheshimiwa naomba sana nieleweshwe pesa zilizobakia zimefanyiwa shughuli gani mpaka hivi sasa hata leo tuweze kuwatafutia fungu jengine. Mhe. Mwenyekiti, hilo ningeomba sana.

Lakini nikiingia katika ukurasa wa 28 ametuonesha Mhe. Waziri jinsi anavyojali Jumuiya za Walemavu. Mheshimiwa bado hizi fedha ni ndogo hazitoshelezi kabisa, kumpa mtu fedha hizi shilingi milioni moja laki saba kutokana na hali yao haihalisi. Mhe. Waziri hii mimi sikubaliani nayo hata kidogo, hawa wenzetu wana upungufu wa viungo, tayari hawa kidole kimoja tu hapa katika vitano kikitoka keshakuwa na kasoro na huna uwezo wowote wa nguvu za kufanya kazi kwa nini tuwape pesa kidogo. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, nitarudi sana hapa lazima hawa watu waongezewe ili fungu liweze kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, siku nilitembea *Sober House* wale wanapewa shilingi milioni moja sijui na laki tano. Hata na wale Mhe. Waziri naomba sana waongezwe kutokana na kuwa nao wanasaidia ukuaji wa madawa ya kulevya. Hivi leo tuangalie Mhe. Mwenyekiti, tunakupa shida lakini usione shida kutokana na hali halisi.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika maeneo haya ambayo nitoe nguvu zangu zote hata wananchi wa Jimbo la Kitope wanakubaliana na suala hili. Kwa sababu mle wapo wengine wanakula unga, wengine walemavu nao hawa nimeona niwasemee ili kutilia mkazo ili wafanikiwe.

Mhe. Mwenyekiti usiwashe taa, kwa hiari yangu nasema kuwa sitoiunga mkono mpaka nitakapopata maelezo mazuri yatakayoniwezesha mimi niwe na nguvu kuweza kuunga mkono. Ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote napenda nitumie fursa hii haraka haraka kukushukuru wewe kunipatia hii nafasi ya kuweza kutoa mawazo yangu katika Baraza letu hili katika hoja

iliyopo mbele yetu. Kwa hivyo, mimi binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi nashukuru sana kunipatia hii nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika kutoa pongezi tu kwa Waziri kwa hotuba yake nzuri na ameieleza kiutaalamu kabisa na tumefahamu. Aidha, nitumie fursa hii nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Wenyeviti ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi wa Kitaifa na yeye kuwa makini, sio tu katika kupinga au kuiweka vizuri ile ripoti yetu, lakini katika kuiwasilisha naamini kila mtu amefahamu. Kwa hivyo, nampongeza sana Mheshimiwa.

Baada ya dibaji hiyo ndogo Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa katika hili uniruhusu dakika moja nitoe *introductory statement* ya huu mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, hili Baraza la Wawakilishi la Zanzibar hili ndio Bunge letu, hili kwa bahati ni miongoni mwa Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Mhe. Mwenyekiti, katika hili sasa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanatakiwa wawe makini katika kuliweka Baraza hili kuwa ni miongoni mwa Mabunge ya Jumuiya ya Madola.

Mhe. Mwenyekiti, katika hili nadhani kazi yetu sisi humu ni kujadili mambo pamoja na hii miswada tunayoletewa, kwa hivyo Mjumbe yoyote wa Baraza la Wawakilishi anatakiwa kwa kiasi kikubwa awe anajadili mambo. Sasa kama atatokea Mwakilishi yoyote humu ndani kumuona anamjadili mtu huyu atakuwa ana *simple mind* jambo ambalo hatolipa hadhi Baraza hili ambalo ni Bunge la Jumuiya ya Madola.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe tumia zaidi lugha ya Kiswahili ili ueleweke vizuri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa maelekezo yako Kiti. Mhe. Mwenyekiti, akili za kawaida mara nyingi zinajadili mtu, akili za katikati zinajadili matukio na hizi akili kubwa zinajadili *issues*. Sasa Mheshimiwa katika hili ndio nikasema kwamba hili ni Bunge la Jumuiya ya Madola kwa vile Wawakilishi ni Wabunge wa Jumuiya ya Madola mnatakiwa mliweke katika hadhi Bunge hili ndani ya Baraza letu la Wawakilishi, utakapokuja hapa kusema Saleh Nassor hivi, Mhe. Mwinyihaji hivi, kusema Rashid Seif hivi, una-*discuss* watu ambapo ile *simple minded* sio kwamba unajidhalilisha wewe tu lakini unalidhalilisha hata hili Bunge letu Baraza la Wawakilishi kwamba bado ni tatizo.
Mimi nawaombeni sana Waheshimiwa kwa hili tulipeni hadhi Baraza letu la Wawakilishi kwa kuwa na akili kubwa ili tuweze kujadili mambo na sio

kujadili watu. Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa naomba sasa niende moja kwa moja katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Idara ya Mazingira ambayo Mhe. Waziri aliizungumza katika ukurasa wa 22, kwenye Ibara ya 59. Naomba ninukuu kidogo hii ibara ya 59 kwamba, "Jumla ya miradi ya hoteli 65 imekaguliwa na miradi 15 ya uwekezaji imefanyiwa tathmini (*EIA*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani suala la mazingira halitaki mchezo katika nchi hasa nchi kama Zanzibar, ambayo kwa kiasi kikubwa inategemea kilimo kwa ajili ya maendeleo, sio kwa wananchi lakini hata hili taifa letu kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha sana pamoja na kwamba miradi 65 imefanyiwa upuuzi, lakini kuna matatizo ya uharibifu wa mazingira kupitia hii miradi ya mahoteli. Hili ni kutokana na udhaifu kwamba hii Idara ya Mazingira katika Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais haina meno hiyo kazi yake ni kusimamia tu, lakini haina meno wala haina sheria inayowafanya kuwatia watu hatiani jambo ambalo ni tatizo sana.

Kitendo hiki Idara hii ya mazingira hata hivi juzi juzi tu Kaskazini huko kulikuwa na ujenzi wa hoteli mtu kazuia sehemu ya wavuvi wasiende kuvua kajenga kuta watu wasiende, hawawezi kupita, wakapewa *stop order* kwamba wewe usijenge hapa nauvunja ukuta wako. Kwa kiburi, jeuri na kejeli ya muwekezaji yule aliendelea kujenga ukuta bila ya kujali hii amri ya Idara yetu ya Mazingira jambo ambalo tatizo sana Mhe. Mwenyekiti, katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kuna haja hii idara kupewa meno. Waziri huyu kwa kushirikiana na Waziri anayehusiana na mambo ya sheria na Katibu watuletee sheria hapa Barazani ili tuwape meno hawa wenzetu, bila hivi mazingira yataendelea kuchafuliwa na kuchafuliwa kila siku huku wanaochafua mazingira hayo wakiwa na jeuri na kiburi jambo ambalo ni tatizo sana.

Mhe. Mwenyekiti, hii miradi 15 nadhani ni pamoja na uwekezaji unaofanyiwa hiyo *EIA* pamoja na ujenzi huu wa barabara. Mheshimiwa hivi ninavyokwambia maeneo ya Micheweni, maeneo ya kwao huyu mama sehemu za Kandwi huko, maeneo ya Vitongoji Umangani pale mpaka Makaani huko yameathirika sana pamoja na kwamba hii miradi imefanyiwa *EIA* lakini mashimo yaliyoko ni hatari. Sisi hatuna tena pa kulima, tulikuwa tunategemea ardhi ile ya Makaani kule kwa ajili ya kufanya kilimo na kupata rizki, tulikuwa tukilima nyanya, tungule, mahindi ili kupata chochote kuweza kutuendeleza katika maisha yetu. Lakini imekuja hii miradi ambayo imefanyiwa tathmini ya kimazingira ikaja ikakoroga sio kuharibu tu, lakini kukoroga mazingira ardhi ile haifai tena wala sisi wakulima hatujaambiwa

kwamba badala ya kulima tushaiharibu ardhi yenu hii basi hizo kampuni zilizopo zikatuwezesha, ina maana kuuza tonge kwa tonge pale Chake Chake ili kupata rizki tumeachiwa tu. Sasa hili ni tatizo la kimazingira na ni tatizo la kimaisha kwa sisi maskini wa Mungu.

Kwa sababu walipoiharibu ardhi ya Makaani haifai kwa kilimo, hamna kilimo wala hatuna mitaji ya kufanyia biashara tukaweza kujiendeleza sisi na familia yetu. Sasa katika hili Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze kwa kina ni kwa kisi gani watu walioathiriwa na makampuni ya ujenzi kama vile *H. YOUNG* kwa maana watu wa Vitongoji/Makaani ambao mashamba yao yamekorogwa yote kwa kuchimba kifusi wao wamewekwa wapi na mashamba yale hayarudishiki tena, wenyewe wakafanye kazi gani na wakija huku wataambiwa ni wazururaji. Mnatusaidia nini katika hilo, au wapige makaa na wakipiga makaa mtawaambia kuwa wanakata miti kuharibu mazingira mnawaweka ndani, hili ni tatizo mtueleze hatujui wapi pa kwenda.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira ya uwekezaji, naomba nizungumzie suala hili la mazingira ya uwekezaji. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kumekuwa na tatizo sana la mambo haya. Hivi juzi sisi tulipitisha sheria ya kuweka *ZBS*, ili bidhaa zitakazoingia katika nchi kudhibiti bidhaa. Jambo la kufurahisha leo nilikuwa nasikiliza kwa wenzetu Tanzania Bara wao kulikuwa na *discussion Star TV* pale asubuhi kwamba *tbs* wamezungumza kuingiza nguo za ndani hizi za mitumba za akina baba na akinamama, hawa *tbs* wamekataza kwa sababu zinasababisha mambo ya maradhi, nguo nyingi tu za ndani naona tabu kuzitaja lakini zimetajwa pale kwamba hizi si ruhusa kuingizwa, nahofia kuja kukiuka kanuni Mhe. Mwenyekiti.

Sasa *ZBS* (*Zanzibar Bureau of Standard)* wao wanatwambia nini, nguo za ndani hapa zinaingizwa. Hivi juzi kulikuwa na ugonjwa kule Pemba mtu anafanya majibu akijitumbua linatoka funza, yalitokezea maradhi haya kule Pemba na mpaka juzi juzi tu, anafanya uvimbe akijitumbua anatoka mafunza. Hili si jambo la kubahatisha na kama serikali inataka ushahidi mimi nitawapeleka na wako waliotoa mafunza katika majibu yao wanapatikana. Sasa mambo kama haya, mambo yanaingia bila viwango sidiria hizi ambapo sidiria sio kama ataathirika yule anayevaa tu, lakini hata sisi tunaokaribia mambo hayo na watoto wanaonyonya. Mimi nadhani *ZBS* ina haja ya kuwa makini sana katika hili ili wasiweze kuwapatisha maradhi hawa akinamama ambao wanatuliwaza sana, watoto wetu wanaonyonya na wao wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala zima la uingizwaji wa bidhaa nyengine hizi za mambo ya *electronic.* Mheshimiwa kuna mambo yanakwama yamechoka sana, lakini huku yanakuja wengine wanasema tunafanywa kama jaa na ukiangalia kweli. Mimi sitaki niseme mitumba isije, ile kwa sababu

ndio inayo-*import,* lakini iwe na viwango. Nataka Mhe. Mwenyekiti Baraza lako linielewe na wananchi wa Zanzibar wanielewe wasije wakaja wakaninunia mimi sikatazi masuala ya mitumba kuja hapa laa hasha! Lakini hiyo mitumba iwe *standard* katika hali nzuri.

Wewe unakuta TV hata hazijauzwa zishabomoka bomoka pale Bandarini mkawa mnachukua vile vyombo huyu anatia huku, makompyuta chombo hiki anatia huku ndio wanakuja kuuziwa, cha huku anatia huku yale makachara mengine yaliyokuwa hayafai yanatupwa katika vyanzo vya maji.

Mhe. Mwenyekiti ni tatizo, ni tatizo kubwa kwa sababu katika haya mambo alakiniki kuna kitu kinaitwa *mercury* mle, sijui kwa Kiswahili inaitwaje, *Zebaki***.** Hii *Zebaki* ikiingia katika maji na haya madude yanatupwa katika vyanzo vya mkaji mambo ya *electronic* yanayotoka Ulaya, yakishaingia katika vyanzo vya maji haya hii *Zebaki* ikitumika na maji ya kunywa na maji ya kutumia ya kukogea basi yanaharibu ubongo. Sasa unakuta siku hizi vijana wetu tunasema wanavuta unga kumbe wakati mwengine inawezekana *Zebaki* imekuwa nyingi katika maji wala si unga wengine. Sasa hapa nilikuwa ndio nazungumza kwamba umuhimu wa *ZBS* kuwa makini kuingiza mitumba iliyokuwa na viwango sio jaa hili.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, katika hizo hizo bidhaa hatuko makini serikali inaharibu mazingira. Kwa mfano, hivi sasa utakuta mafriji *used* ambayo yashaoza, ndani yake mna mende wale wadogo wadogo, vimende vya nchi za nje huko tunaanza kuvileta huku. Sasa kama hatukudhibiti wale mende mbona kunguru mnawaua, mbona hamtumii pesa kuua wale mende ambao wanaingia kwa *speed* kubwa sasa, kwenye mafriza yale yanayotoka Uingereza kazi yenu ni kuua kunguru tu shilingi milioni mia tatu. Sasa mimi nasema katika hili sijui Waziri atakuja kunijibu nini, idadi ya mende kutoka nje inakuwa kubwa na hatujui madhara yake mende hawa. Mimi ni mtu mtaalamu katika masuala ya viumbe hawa wakija wakiingia wakizidi katika *ecosystem* mende wageni waka-*disturb* na ile *bilogical equilibrium* katika *ecosystem* haitopatikana. Tusiendekeze kuua kunguru tu hawa mende je!.

Mhe. Waziri mimi nazungumza kwa uchungu sana kwa sababu mimi ni taaluma yangu, mimi ukija ukizungumza sheria sitasema sana nitapiga piga tu, lakini ukizungumza mambo haya mimi ni mtaalamu katika masuala haya, japo si mtaalamu niliyebobea lakini nina taaluma ya kutosha katika mambo haya ya viumbe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naona tatizo hilo na naomba sana sasa Waziri aje atueleze kwa nini katumia shilingi milioni mia tatu kuua kunguru ambao nimeshamwambia ukitafuta makoho mia mbili ukiweka Unguja na mia moja

tukiyapeleka Pemba kwa mia tatu hawa yakawamaliza kunguru wote bila ya kutumia dawa, akanidharau mimi kama mwana taaluma. Sasa katika hili aje anieleze sasa, na tena baya zaidi wanatumia sumu iliyo ghali sana, kama mtaalamu mimi napata tatizo kwa sababu tungekaa tunatumia *DDT* sisi hapa kama hujui *toxoid* serikali iliingilia kati tusitumie *DDT,* leo mnatuletea sumu kuua kunguru ambayo inakuwa *wash* ndoo za maji inaingia katika vyanzo vya maji, tuwaelewe vipi wanasiasa sisi wataalamu tuwaeleweje? Msifikiri kwamba humu hamna watu wenye *profession* zao hizo, msifikiri sote ni wanasiasa sisi wengine tuna *profession* humu ndani mnapoambiwa hamkubali, hatukubali kabisa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti nadhani aje anieleweshe sasa kwa kina Mhe. Waziri, kwa nini anaacha kutumia makoho kula kunguru wale. Halafu hasara nyengine itakayotokea kwa kutumia sumu nyinyi mnaua kunguru weusi lakini mpaka kunguru vibaka wanakula na wanakufa. Kwa hivyo, ile *existing species* katika *ecosystem* nayo tutai-*weed* out kwamba bado ni tatizo kitaalamu. Ninapomaliza kusema nzige, panzi, nyevule wakaongezeka ambao watakwenda kushambulia mipunga yetu na kukosa mavuno hili ndio tatizo Mhe. Mwenyekiti.

Sasa jengine nije katika mambo ya mazingira ya upandaji wa miti. Mimi nilieleza zamani hapa kwamba nyinyi hamfanyi tafiti za kina, katika kupanda hiyo miti mnayotaka tupande hamfanyi tafiti za kina mnatwambia tu tupande miti. Siku moja nilimuuliza Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili kuhusu tatizo la mivinje Mungu bariki sasa hivi hayupo nataka apate siku aje humu tena Mwenyezi Mungu amjaalie. Waziri wa Kilimo alinambia bwana mivinje haina tatizo, kwa sababu mivinje ina *root nodules* ambayo inafyonza *nitrogen* wakati hayo si kweli, kama utaangalia *hansard* zimo, mti pekee uliojaaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na *root nodules* na kuweza kuzi-*fix nitrogen from the air* na kuwa na *maitroles* ni hii *leguminous plants* ambayo ni kunde tu ndio Mwenyezi Mungu kazijaalia hivyo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba mnafanya tafiti? Kwa sababu mvinje kwa mujibu wa taaluma ya mambo ya viumbe una *high transpiration rate,* una uwezo wa kufyonza *access water from the soil* kupitia katika mizizi nyuzi na kuja zake katika *lenticels* na kutoa maji katika hewa na kuyapoteza maji yaliyoko katika ardhi kwa njia inayoitwa *transpiration*. *Removering water from the soil to the atmosphere* hiyo ndiyo *transpiration***.** Sasa unaponambia kwamba mvinje unakuwa na *high transpiration rate* kwa sababu una hizi *lenticels* nyingi ambao unafanya *lenticular transpiration* ndio tukasema inaweza kuwa *high transpiration rate.*

Nilisema juzi nikaambiwa mvinje hauna majani, hauna majani lakini una *lenticels* nyingi na ndio maana huu mvinje unausikia unavuma mmm kwa sababu ya maji mengi kwenye ardhi, leo mnatwambia mvinje hauna tatizo, fanyeni utafiti mje mtueleze hapa. Kwa sababu Vitongoji hakufanyiki kitu kwa vile mivinje ishakuwa mingi maji ardhini hayamo, vipando haviwi tena, ardhi inachimbwa mawe hatujui tuelekee wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu kwa watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu ni miongoni mwa Watanzania na kwa mujibu wa ibara ya 21 ya Katiba ya Zanzibar, niruhusu Mhe. Mwenyekiti, ninukuu. Na wala sio kama nazungumzia mambo ya walemavu labda jirani yangu hapa ni mlemavu laa, nazungumzia watu wenye ulemavu in *general*.

Kifungu cha 21(i) cha Katiba ya Zanzibar kinasema kwamba:

"Uhuru wa kushiriki shughuli za umma haki na kufanya kazi kupata ujira"

Kifungu cha 21 (ii) kinasema kwamba:

> "Kila Mzanzibari anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye maisha yake au yanayolihusu Taifa".

Mhe. Mwenyekiti, sisi wakati huu tunazungumzia suala la utawala bora na demokrasia, inasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba Zanzibar tunazungumza *verbal statement* hakuna *practicality***,** sioni pahala popote palipowekwa watu wenye ulemavu. Baraza la Mawaziri nimeliangalia mle mawaziri wote sijaona mlemavu hata mmoja humu ndani, huku ni kuwanyanyapaa walemavu! Nimekuja nikaangalia safu ya Makatibu Wakuu nikaitizama sijaona mlemavu, nimeona Mkurugenzi mmoja tu alietoka katika Ofisi hii tunayoijadili leo ni mlemavu *ratio* yake *one to 1: 99* ni unyanyapaa! Sasa mimi nadhani Mhe. Waziri anayehusika na mambo haya shirikiana na Mhe. Waziri anayeshughulikia mambo ya Sheria na Katiba mueke *proportionality* katika masuala haya na haya yana haki. Tunazungumzia haki za binaadamu Mhe. Mwenyekiti, kwa uchungu mkubwa sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe malizia.

Mhe. Saleh Nassor Juma: (anaendelea) nataka sana nimalizie lakini hili limeniuma sana. Kwa kuwanyanyapaa walemavu wakati wana uwezo mkubwa sana na wao. Hivi sasa kuna walemavu wana *PhD* mimi nawajua wana digirii sijui za nini ambazo mimi sinazo, wana *Master* hawa walemavu mimi sinayo. Lakini Serikali haiwapi nafasi inawanyanyapaa.

Basi la kusikitisha zaidi Mhe. Mwenyekiti, si hili Baraza letu limejengwa juzi juzi hili si mmeshindwa hata kuweka *ramp* ya kuweza kufika yule mlemavu hapa akapata fedha jamani si kuwanyanyapaa huko? Kweli mnafikiri Mhe. Raya Suleiman Hamad anafika pale hilo jengine.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, nataka tu nimalizie kwa suala hili la Madawa ya Kulevya na Ukimwi sitopata kuchangia maana umeshanambia nimalizie. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Serikali iwe makini kwa sababu hizi *Sober houses* wanazianzisha wenyewe wananchi wewe hata ukipeleka unapeleka kitu kidogo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Baada ya maelezo haya Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu sana, naunga mkono hoja na nitazidi kuunga mkono hoja hii pale Mhe. Waziri akija kunifafanulia kuhusiana na suala zima la hawa kunguru wanaotumia dawa katika kuuliwa na dawa hii haina madhara kwa binaadamu au vipi? Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa dhati kabisa kunipa nafasi hii ya kuchangia Makadirio Ofisi ya Makamu wa Kwaza wa Rais.
Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuanza lolote na mimi kama binaadamu wengine nipitishe uungwana wangu kumshukuru Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Mhe Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Pia nichukue fursa hii adhimu kuwashukuru watendaji wa Ofisi hii kupitia Katibu mahiri Shajak pamoja na kurugenzi zake zote ikiwemo ya Mazingira inayoongozwa na Ndugu Sheha Mjaja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mambo mawili, matatu madogo sana. Sitoichangia sana Wizara hii kwa sababu tendaji za kuregenzi hizi mimi ninazifahamu vya kutosha hasa katibu Mkuu ni mwalimu wangu wa siasa, Wakurugenzi wake nimefanya nao kazi kwa muda mrefu kabla kuingia katika Ofisi hii nawajua uwezo wao na nawajua fahamu zao na nawajua utendaji wao. Jitihada zinaonekana na Mwenyezi Mungu awape nguvu katika utendaji wa kila siku wa shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuzungumzia ukurasa wa 14 kifungu cha 36 ambacho Profesa hapa amemalizia katika suala zima la mradi wa kunguru. Mimi sina wasi wasi mkubwa katika suala hili niseme napongeza jitihada za

kutokomeza kunguru katika maafa ambayo wanayasababisha katika nchi hii. Lakini tatizo langu linakuja dogo sana tu.

Kwanza niwaombe tu kuna mapungufu madogo madogo yanajitokeza katika ile mitego ambayo wameiweka, wakati ilipowekwa ile mitego katika hatua za awali jitihada zilikuwa nzuri za kupitia ile mitego na kuwaondosha wale kunguru ambao wameshafariki. Lakini kadri siku zinavyoendelea lile zoezi la kufuatilia ile mitego kidogo ilikuwa linasuasua.

Sasa sijui kama mapungufu ya pesa yalikuwa wamepungua au gharama za kutumia mafuta kufuatilia ile mitego zimepungua. Na baadhi ya mitego mingine imewekwa karibu na mazingira ya vijijini yaani iko mitaani kabisa. Naweza kutoa mfano mtego ambao umewekwa Bwejuu uko chini ya nyumba za watu sawa unapochukua muda mrefu basi na kuondosha ile mizoga ya kunguru ambao tayari wameshafariki basi wananchi wale wanakuwa wanaishi katika mazingira magumu ya kupata harufu ya mizoga ya kunguru ile ambayo imewekwa.

Sasa niombe kabisa hii mitego ambayo imewekwa katika maaeneo ya karibu basi taasisi inayohusika kuwa wepesi kama walivyoanza jitihada za mwanzo kuweza kufuatilia na kuondosha mizoga ile ili kuondosha kero kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kabisa hivi karibuni amepata Nishani ya Mwanawake Jasiri. Sasa atumie ujasiri wake Mhe. Mwenyekiti, katika kutuonesha utendaji wa kazi, naamini uwezo anao lakini baada ya kupata ile *promotion* basi na yale mambo yaonekane. Kama tunavyomuona mama yetu Anna Tibaijuka anavyofanya shughuli zake katika taasisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, tumetumia gharama kubwa sana katika mradi wa kunguru. Lakini tunaacha kutumia gharama kubwa sana katika kuwasaidia wanaadamu ambao wana mapungufu na hususan ndugu zetu walemavu. Nimuombe Mhe. Waziri kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti wakati alipokuwa akiwasilisha hotuba yake hapa alizungumzia suala la Skuli ya Kisiwandui. Mhe. Mwenyekiti, Skuli ya Kisiwandui kwa bahati ziara ile tuliifanya katika Kamati iliyopita na wewe mwenyewe ulikuwa shahidi. Jinsi ya wanafunzi wa Skuli ile wanavyoteseka, ahadi zilikuwa za muda mrefu maneno mengi tumejitahidi na tumo mbioni lakini hatimae wanaadamu wanateseka na wanaumia kutokana na mapungufu ambayo Mwenyezi Mungu amewajaalia.

Sasa kama tumetumia tumeweza ku-*create* jambo tukaweza kupata mafungu ya fedha tukatokomeza kunguru. Kwa nini tushindwe ku-*create* mambo kuweza kuwasaidia binaadamu ambao Mwenyezi Mungu kawapa ulemavu. Sasa nimuombe Mhe. Waziri atumie jitihada zake, atumie maarifa yake kwa namna yoyote ile kadhia wanayoipata walemavu, wanafunzi ambao wana mapungufu ya aina mbali mbali katika Skuli ya Kisiwandui. Kupitia bajeti hii Mhe. Waziri ufanye maarifa yako yoyote wale wanafunzi wanaonekana wana matatizo. Mhe. Mwenyekiti, kama utakwenda katika Skuli ile utalia, ile ni skuli moja lakini tunazo nyingi, tuna Mwanakwereke pia wapo kama wale.

Hali ya watoto wetu ambao wana matatizo kama yale inatisha, mtoto haoni anaingia kwenye dimbwi la maji atafute mlango ulipo. Wewe unayeona siku za mvua mashaka seuze yule ambaye haoni. Sasa Mhe. Mwenyekiti, imani yangu Mhe. Waziri hili atalichukua na kulifanyia kazi.

Kwa haraha haraka Mhe. Mwenyekiti, kwa ku-s*ave* muda wako. Basi nije katika suala la mazingira. Mhe. Mwenyekiti, kamati iliyopita ilifanya kazi kubwa sana na ikaona mapungufu ya mahoteli jinsi wanavyojenga kiholela mpaka katika fukwe za bahari. Basi nilijaribu kuiomba Taasisi ya Mazingira ikajaribu kuchukua jitihada za kutia *notice* lakini kwa heshima kubwa tumshukuru ndugu yetu wa hoteli ya *Zanzibar Ocean view* peke yake ndiye aliyetii amri ya agizo la Serikali katika kupambana na masuala ya mazingira.

Lakini waliobakia wote hakuna ambaye alitekeleza hili agizo, na wengine si kutekeleza wanakaidi zaidi na kwenda mbele kufikia hiyo bahari siku hadi hadi. Sasa nimuombe Mhe. Waziri pamoja na kuambiwa kuwa hana meno lakini mimi naamini meno anayo kwa sababu kuna taasisi nyengine zina sheria, ashirikiane na taasisi ambazo zina sheria kwa kuweza kuwabana hawa watu ambao wanachafua mazingira. Kuna sheria mbali mbali ambazo wenzetu wizara nyengine wanazo.

Sasa hii ni hatua ya awali kwa sababu tunajiandaa na kusubiri miswada lakini kuweza kuvuta nguvu katika kupeleka sheria hii Ofisi yetu ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, najaribu kwenda mbio kwa sababu muda unakimbia sana na mimi nitakuwa mmaliziaji.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika kilio ambacho siku zote mara zote nitakuwa napiga kelele lakini nikiachia kupiga kelele nitakuwa napewa vi -*notice* vya siri siri kumpelekea mama yangu katika suala zima la kupambana na dawa za kulevya.
Mhe. Mwenyekiti, sisi tunazeeka na tegemeo la nchi hii ni vijana ambao tunategemea rika wakue ili watusaidie katika masuala mazima ya nguvu kazi kesho baadae. Mhe. Mwenyekiti, vijana wanateketea na siku kila zikiendelea

suala la madawa ya kulevya basi linakuwa ni tishio katika nchi yetu. Nimesema mwanzo kuwa Mhe. Waziri umetunukiwa nishani ya ujasiri tumia *power* Mwenyezi Mungu aliyokujaalia ya kupata hii heshima. Tumia ujasiri wako katika kuhakikisha suala la madawa ya kulevya katika nchi hii linamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema hivyo nna ushahidi wa baadhi ya mambo ambayo Wizara hii ilijaribu kujitahidi kuyafanyia kazi na yamepungua kwa kasi sasa kama katika suala la madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano katika masula mazima ya kutokomeza misumeno ya moto. Tunaona jitihada ya misumeno inakamatwa inachomwa moto, iwe Zanzibar iwe Tanzania Bara, Bangi inakamatwa magunia kwa magunia yanachomwa moto, tunaona katika nchi yetu hii hii marobota ya mifuko la plastiki inakamatwa inaangimizwa na wahusika wanafikishwa Mahakamani.

Lakini hatujaona Mhe. Mwenyekiti, hata siku moja kuoneshwa katika *television* kama kuna kesi hii ya dawa za kulevya na dawa zilizokamatwa zimeangamizwa hatujaona. Kuna nini Mhe. Mwenyekiti, najua hiyo ni sehemu moja.

Lakini sehemu ya pili na wao pia salamu zitawafikia. Kwamba tatueni hatua za dawa za kulevya, tunaambiwa kila siku tu kesi mia tatu hizi kesi zinakuwa zinaongezeka tu. Lakini umalizaji wa kesi hatuujui. Sasa mimi nilikuwa nina mashaka Mhe. Mwenyekiti, katika kile kitabu chetu cha Bajeti ukurasa wa 84, kifungu 0601 Tume ya Taifa ya Utaribu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya (*National Commission for Coordination and Control of Drug Abuses*).

Mhe. Mwenyekiti, katika fungu dogo la 220404 gharama za mafuta. Mimi Mhe. Mwenyekiti hapa kidogo nimepata mashaka sana. Sisi tunahitaji mafuta tufike mitaani tukapambane na masuala ya dawa za kulevya, tunazipata habari za mtu ambaye ana mzigo wa dawa za kulevya tumfukuze ili tumkamate. Sasa baada ya kuongeza gharama na kuzidisha matumizi ya kupata fedha zaidi za mafuta hili fungu limepunguziwa mafuta.

Mwaka jana lilikuwa milioni tano laki tano lakini mwaka huu lina milioni tano laki mbili. Sasa niseme kwamba hii kazi ilifanyika vizuri hatuna haja ya kuwafikia au kuwatafuta hao watu kuhangaika kufanya kazi katika suala zima la kuwadhibiti. Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba akija Mhe. Waziri anisaidie nini sababu za kupunguza mafuta katika suala zima la dawa za kulevya anambie sababu gani za kupunguzwa fungu hili.

Lakini kinachonisikitisha zaidi katika masuala ya mafuta ilikuwa wafikie na kupambana na watu wa dawa za kulevya hili limepunguzwa. Lakini katika masuala ya kutafuna tafuna na kunywa mafungu yameongezwa. Sasa hapa kidogo Mhe. Mwenyekiti, nakuwa napata mashaka. Kwa nini huku kunako matumaini labda kwa utendaji kazi mzuri kunapungua lakini kule kwengine kunako mambo ambayo hayana msingi ya kutafuna na kunywakunywa kumeongezwa?

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie pia katika kifungu 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti fungu dogo 220200 vibudurishaji, 2012/2013 ilipangiwa kutumia shilingi laki saba na hamsini elfu. Lakini mwaka huu imepangiwa shilingi milioni thalathini na moja laki tatu hamsini na tatu elfu na mia tano mara nne zaidi ya bajeti iliyopita.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo muda umemalizika mimi sina tatizo na Ofisi hii. Baada ya maelezo mazuri *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu basi tutaunga mkono hotuba hii ili kuwapa fursa Mawaziri kuzungumza na watendaji kwenda kufanya kazi kwa ajili ya kuiletea nchi yetu mafanikio. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe muda uliobakia ni mchache sana kwa kweli kwa kuweza Mjumbe kuchangia. Kwa hiyo, natamka rasmi kwamba tunaakhirisha kikao hadi leo jioni saa 11:00 kamili. Nawashukuru kwa michangio yenu na ushirikiano wenu ahsanteni.

(Saa 6: 45 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa mujibu wa list yangu ambayo nimeandika hapa ya wachangiaji, ni wachangiaji kama wajumbe 12. Sasa Waheshimiwa Wajumbe, nilikuwa naomba sana tuangalie muda kwa maana ya kwamba tuzungumzie hii bajeti tu na pia tusirudie yale ambayo tayari yameshazungumzwa. Nafikiri mmenifahamu vizuri.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii jioni ya leo kuwa mtu wa mwanzo katika kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa shukrani zangu kwako, nimshukuru Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, niwashukuru watendaji wa ofisi yake kwa kuandaa hotuba hii ya bajeti ambayo leo imewasilishwa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwenye mafungu moja kwa moja kwanza, ili muda wako tusiupoteze ambapo mimi nahisi kidogo yanahitaji ufafanuzi kabla sijaingia kwenye kitabu cha hotuba.

Mhe. Mwenyekiti, naanza na 0301 Ofisi Kuu Pemba, nilikuwa nataka ufafanuzi kwenye fungu dogo 211200 mishahara isiyokuwa ya fedha taslim, kwenye fungu 211208. Naomba ufafanuzi katika hili Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kidogo, maana yake mwaka jana, mwaka juzi na mwaka juzi yake hapana kitu hapa, lakini mwaka huu naona zimeingizwa milioni 5,400,000 sijui ni kwa ajili ya nini hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea mbele nije kwenye suala la gharama za mafuta na vilainisho 220400, fungu dogo pale la 220404. Mhe. Mwenyekiti, jana pia nilijaribu kuonesha mawazo yangu katika hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais, kuonesha kuwa fungu hili sioni mimi umuhimu wake kuwepo, kwa sababu tayari huku chini kuna mafungu ya kufanyia *service* hayo magari na kuna fungu la kununulia spea. Sasa hivi vilainishi mimi nina wasi wasi vimewekwa vya kazi gani wakati unapokwenda kufanyiwa *service* hizi *oil* na grisi unawekewa katika gari lako. Ingawa Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendele alijaribu kujibu, sikupewa nafasi ya kuweza kutoa maelezo yangu ya ziada. Kwa hivyo, bado narudia tena na hoja yangu ile ili kupata maelezo ya ziada leo hii.

Nikiendelea mbele Mhe. Mwenyekiti, kwenye fungu la 311200 ununuzi wa mashine na dhana, niende kwenye kifungu kidogo pale cha 311202 ununuzi wa gari. Mwaka jana Pemba inaonekana gari lilinunuliwa, lakini na mara hii zimetengwa fedha nyengine milioni 50, mwaka jana zilikuwa milioni 25 na mara hii milioni 50. Sasa nilikuwa nataka kujua tu kwamba halikuwahi kununuliwa kwamba ilikuwa ni fedha ndogo zinatakiwa ziongezwe nyengine, au la.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie kwenye fungu la 0401 Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Nianze kwenye fungu la mishahara ya fedha taslim 211100 nishuke kwenye kifungu kidogo cha mwisho pale, 211116 posho, vikao na kamati kuna milioni 17 hapa. Sasa nilikuwa nataka nipatiwe ufafanuzi wake katika hivi. Baadae nishuke kwenye 220200 viburudishaji. Halafu nishuke kwenye kifungu kidogo cha 220201 chakula na vinywaji milioni 31. Mwaka juzi kulikuwa kuna milioni 3,150,000, mwaka jana kukawa kuna 750,000, lakini mwaka huu naona kuna milioni 31. Nilikuwa naomba maelezo katika hili, Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie maana hili fungu limetononoka mno, maana tulikuwa tunataka kujua kuna tatizo gani hapa.

Mhe. Mwenyekiti, nikisogea mbele niende kwenye vifaa na huduma 220500 kwenye ada ya ushauri, kifungu kidogo cha 220509, ada ya ushauri nilikuwa nahitaji ufafanuzi ni ushauri wa namna gani unaotolewa katika kifungu hiki, kiasi cha kutengwa fedha kiasi hicho.

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, naingia kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi 0501. Fungu hili Mhe. Mwenyekiti, mimi ninapata mashaka kidogo hasa kwenye mishahara ya fedha taslim. Ukiangalia kwenye kifungu cha 211101 mishahara na waajiriwa wa kudumu wa serikali, mwaka jana kulikuwa na milioni 235,159,000, lakini mwaka huu anaomba milioni 663. Hebu Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie hapa kulikoni na atakapokuja aje na data zilizokamilika. Kama ni kuajiri umeajiri watu wangapi wa ziada kiasi hiki, kiasi cha kwamba mshahara utoke milioni 200 mpaka milioni 600.

Mhe. Mwenyekiti, nikiteremka tena chini hapo nakuja kwenye 211108 malipo ya kujikimu na malazi *Per diem*. Mwaka jana hukuwa na chochote hapa, mwaka juzi ulikuwa na kidogo, lakini mara hii una milioni 14 unaziomba. Sasa na hizo nilikuwa nahitaji maelezo yake, nikiridhika sina tatizo.

Lakini nishuke chini yake kidogo kwenye posho maalum 211110. Mwaka jana uliomba milioni 107 na uliidhinishiwa hizi, lakini mwaka huu naona unahitaji milioni 307. Hebu kidogo utakapokuja Mhe. Waziri na hili utusaidie ufafanuzi wake, kama patakuwa pana kuridhika mimi sina hoja nitakuruhusu, lakini kwa sasa nitazuwia mpaka utakapotoa maelezo ya kutosha katika mafungu haya na haya mengine ninayokuja nayo kidogo. Namalizia kwa haraka Mhe. Mwenyekiti, najali muda wako.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye gharama za mafuta na vilainisho nilishalizungumzia hili na hapa limejitokeza tena kwenye idara ya uendeshaji na utumishi, lakini kwenye kifungu 220500 vifaa na huduma za ofisi vile vile kwenye fungu dogo la 220504 na 220505 navyo pia nilikuwa nahitaji nipate ufafanuzi wake na kwenye fungu la matengenezo madogo ya ofisi, maana unaonekana kila mwaka una matengenezo ya ofisi. Sasa mimi nafikiria ni vyema ungejenga kabisa, kuliko kuwa kila mwaka unaingiza mafungu ya namna hii kuomba matengenezo.

Nikimaliza hapo Mhe. Mwenyekiti, nitaingia kwenye idara ya faragha, *private offices* 2102, hapa kidogo nilikuwa naomba maelezo kwenye 211200 mishahara isiyokuwa ya fedha. Tushuke chini kidogo hapo na 211201 kodi ya nyumba. Mwaka jana ulipatiwa milioni 24, lakini mwaka huu unaomba 98 milioni. Sasa nilikuwa nataka kujua kutoka 24 milioni hadi 98 milioni, labda umeongeza kukodi nyumba zimekuwa tatu ama imekuwaje. Naomba maelezo

katika fungu hili. Nikipata ufafanuzi hapo, basi naweza nikakuachia lakini kwa sasa nitazuwia bajeti yako hii sijaiunga mkono.

Naendelea Mhe. Mwenyekiti, nije katika kitabu cha Mhe.Waziri, kitabu ambacho ametuletea hapa. Nikisogea kwenye ukurasa wa 19 Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, kwenye idara hii Mhe. Waziri mwisho kabisa kwenye kifungu cha 55, anasema Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kujipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, analiomba Baraza liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 1,615,931,000 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo milioni 292,427,000 kwa ajili ya kuendesha kazi na bilioni 1,323,504,000 kwa ajili ya mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia hesabu hii au maombi ambayo anayaomba kwenye kitabu hiki na ukiangalia kwenye buku kubwa huku zinatofautiana sana. Huku kwenye buku kubwa jumla ya fungu hili la idara hii ya uendeshaji na utumishi ni bilioni 1,329,827,000. Sasa huku kwenye kitabu kikubwa anaomba hivi na huku kwenye kitabu chake anaomba tumuidhinishie bilioni 1,600,000,000, naona kuna tofauti kubwa kidogo, sasa sijui kipi anachokitaka Mhe. Waziri tumuidhinishie kipi. Tuangalie kitabu hiki kikubwa au tuangalie kwenye kitabu hiki ambacho hii hotuba umeisoma. Naomba utakapokuja Mhe. Waziri hebu tupe ufafanuzi katika hili liweze kukaa sawa.

Mhe. Waziri, utakapokuja ikiwa unachokiomba ni hiyo 1.6 bilioni, basi nilikuwa naomba maelezo ya ziada sana na hasa idadi ya hao wafanyakazi ambao umewaajiri wapya labda na namna mishahara hii utakavyoigawa, kwa sababu hizi fedha ni za mishahara unazoonesha. Sasa nahitaji maelezo ya ziada katika hili ili niweze kukupitishia bajeti yako hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisogee kwenye ukurasa wa 22 kwenye idara ya mazingira. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu chake cha hotuba Mhe. Waziri ametuonesha hapo kwenye kifungu cha 59 anasema jumla ya miradi 65 ya mahoteli imekaguliwa, miradi 15 ya uwekezaji imefanyiwa tathmini ya athari ya mazingira na kutolewa vyeti vya mazingira na miradi mitano imefanyiwa uchunguzi wa awali wa kimazingira, ili kutoa hadidu rejea za kufanya tathmini za athari za kimazingira na akatushauri twende kwanye kiambatanisho nambari 3 ambako nimekwenda nimeona.

Lakini mimi nilikuwa nataka maelezo zaidi, jumla ya miradi 65 ya mahoteli imekaguliwa, kukagua umekagua, je matokeo ya ukaguzi huo ni yepi. Je, imepasi, imefeli au imekuwaje. Kwa hivyo, utakapokuja kwenye miradi hii ingeomba utufafanulie zaidi ili tuweze kujua baada ya ukaguzi matokeo ya ukaguzi ni nini sasa, maana kukagua umeshakagua, lakini sasa matokeo

hukutuambia. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja atueleze.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kuna kiwanda cha makonyo cha Wawi Pemba kimefanyiwa ukaguzi wa kimazingira na ripoti ya ukaguzi huo imewasilishwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa ajili ya kuchukuliwa hatua za utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa. Mimi nilikuwa nauliza ni mapendekezo gani ambayo yalitolewa katika kiwanda hicho. Nafikiria hiki ni chombo cha wananchi, hivyo ni vyema basi utatuletea taarifa hii ya hayo mapendelezo ambayo mmeyapeleka tukaweza kujua. Je, ni yepi mapendekezo hayo.

Kwa hapa Mhe. Mwenyekiti, naachia hapo nisogee kwenye ukurasa wa 33, kuhusu Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu cha Mhe. Waziri kwenye kifungu cha 92, Mhe. Waziri anajaribu kutuelezea anasema;

Kifungu cha 92

"Tume hii inajukumu la kuratibu mapambano dhidi ya biashara, matumizi, uingizwaji na usafirishaji wa dawa za kulevya".

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kazi ambayo wamepewa tume hii, lakini ukiangalia na bajeti ambayo wamepewa. Mimi Mhe. Mwenyekiti, siafiki hata kidogo. Juzi nilipokuwa nachangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hapa nililigusia sana suala hili la madawa ya kulevya, namna vijana wetu wanavyoathirika na nikaiuliza serikali kwamba kama kweli serikali iko tayari kuhakikisha kwamba hizi dawa haziingii hapa nchini, kweli ina nia hiyo. Maana kila nikiitizama naona kama iko katika kufanya mchezo. Lakini bahati nzuri Mhe.Waziri alipokuja kujibu alisema tumsubiri waziri husika atakuja kutusaidia.

Sasa leo waziri husika ndio umeshawasilisha hotuba yako hapa, kwa hivyo ningeomba uje utusaidie ili tuone ile *seriousness* ya serikali katika hili, maana yake tukiiangalia hii bajeti mwaka jana waliomba 247, kuwapa kwenyewe mpaka Machi wamepata asilimia 45 ya hiyo 247 waliyoiomba. Mwaka huu imeshuka zaidi wanaomba 160, hivi mimi niulize hiyo kazi ndio itafanyika katika hali kama hii. Maana hapa nina hakika inawezekana walileta maombi mengi, lakini katika kukata kata mkaona fungu hili ndio linaloweza kupunguzwa zaidi, maana halina kazi. Tumekuwa na wasi wasi na serikali kama kweli iko *serious* katika kulifanyia kazi suala hili, kwa sababu wauzaji wa madawa wapo, wavutaji, walaji wa huo unga wapo.
Mhe. Waziri kesi umetuambia ziko 21 mahakamani kama maelezo yako yalivyosema. Lakini kama tutazifuatilia zaidi zote hizo zitakuwa ni za wale

wanaokula. Hawa wanaoleta na wanaouuza hebu tuambie Mhe. Waziri hasa una kesi ngapi za hawa, utuletee takwimu hapa ili tuone ni namna gani mnavyojitahidi katika suala hili kama kweli mko *serious*. Maana bado mimi siamini, kila nikitizama na hii bajeti mlioleta ndio imenishitua zaidi, ikiwa mwaka jana 247 na kazi yenyewe ndio hii ambayo tunaiona kama hakukufanyika chochote. Lakini leo mnawakadiria 160 wataweza kufanyakazi kweli hawa. Mimi nafikiria katika suala hili Mhe. Mwenyekiti, serikali bado haijaonesha umakini wake katika kulifanyiakazi.

Kwa hivyo, ninavyotaka Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba sana Mhe.Waziri hebu akija atupe takwimu hasa za hawa waletaji ni wangapi nyinyi mmeshawakamata, wangapi wamehukumiwa na kama kuna kesi mahakamani ziko ngapi. Waletaji, wauzaji, sio mtupe hadithi za walaji. Hawa walaji akishakuwa mtu na shilingi zake 500 atakwenda kuununua kama upo, lakini kama mtahakikisha kwamba hauingii hapa, basi nina hakika huyo mlaji atakuwa hawezi kuula kwa sababu haupati.

Sasa Mhe. Waziri mimi nitaizuwia bajeti yako hii, kama sikupata maelezo ya kina katika kuona *seriousness* ya serikali juu ya suala hili la madawa ya kulevya. Kwa kweli Mhe. Waziri katika hili sina masihara, hapaji kutosha hapa. Ukawafuate watendaji wako vizuri wakupe utuletee, tukiridhika fahuwa, kama hatukuridhika Mhe. Waziri utanisamehe.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nisipoteze muda wako niwapishe na wenzangu nao waendelee. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Siungi mkono hoja *(Makofi).*

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi jioni hii kupata nafasi ya kutoa machache kuhusu ofisi hii ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha jioni hii kufika hapa na kuendelea na shughuli zetu za Baraza kama kawaida yetu.

Pia nitowe shukrani kwako kwa kutuongoza tokea asubuhi hadi jioni hii. Vile vile nimshukuru na nimpongeze waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na hii inatokana na matokeo mazuri aliyofanyiwa na watendaji wake katika ofisi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe pongezi za dhati kabisa kwa mkuu wa ofisi yao, yaani Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kutekeleza ahadi katika jimbo langu. Hivi juzi tarehe 14 Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais alikwenda Pemba, aliombwa kuweka jiwe la msingi katika skuli iliyojengwa katika Shehia yangu ya Mkungu eneo la Mahdus. Kwenye uwekaji wa jiwe la

msingi huo, aliombwa na yeye aliahidi kuchangia. Siku tano baadae yaani tarehe 19 mimi niliitwa katika ofisi yake na kukabidhiwa kile alichoahidi, yaani ndani ya siku tano baada ya kuahidi alitekeleza ahadi yake. Kwa hivyo, nampongeza sana sana. Ningewaomba na wengine wafuate mfano huu.

Mhe. Mwenyekiti, katika jimbo langu hilo hilo la Mtambile Mhe. Rais tuliyekuwa naye hivi sasa, wakati akiwa Makamu wa Rais wa Tanzania aliahidi katika Skuli ya Kengeja kupeleka kompyuta, lakini bahati mbaya haikufika. Kadhalika Rais mstaafu wa awamu iliyopita Mhe. Aman Abeid Aman Karume na yeye alitoa ahadi kama hiyo ya kupeleka kompyuta na *printer* katika Skuli ya Kengeja, lakini bahati mbaya nayo kadhalika mpaka leo haikufika.

Kwa hivyo, ningewaomba wahusika wa ofisi hizi wasiwadhalilishe hawa viongozi, kompyuta ni kitu kidogo sana. Sasa kwa Rais kuweka ahadi ya kompyuta halafu isifike, huko ni kumdogosha kweli kweli.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, niliwasiliana na waziri aliyekuwepo sasa katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi vizuri, lakini mawaziri wakati wa bajeti wanakuwa laini, lakini bajeti ikishakupita eehe! Lakini hivi sasa hata kunitizama hanitizami tena, kwa sababu bajeti yake imeshapita na ombi langu pia limepita. Lakini nawashauri mambo madogo madogo kama haya wasiyapige chenga kwa sababu yanatekelezeka, ni utendaji wa ghafla ambao unaweza kufanyika, kwa sababu ni pesa kidogo sana. Sijui kwa nini mambo kama haya madogo madogo watendaji mnayafanya makubwa ambapo ni ahadi za wakubwa wetu, wakubwa tusiwadogoshe kiasi hicho *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mhe. Waziri kazungumzia mambo kadhaa na ofisi hii kwa kweli nahisi idara zake zote zina matatizo. Kidogo idara ambayo ni nzuri na haina matatizo ni hii ya mazingira, lakini nyengine zote. Ukimwi, madawa ya kulevya, watu wenye ulemavu. Ilimradi yale matatizo yote yamewekwa katika wizara moja. Kwa bahati mbaya ofisi hii ndio yenye bajeti ndogo kuliko nadhani wizara nyengine zote. Mambo yake magumu, lakini fedha za kufanyia kazi ni kidogo sana, sijui serikali inaipima katika vigezo gani ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii katika idara yake ya mipango sera na utafiti katika kitabu chake hiki kuanzia ukurasa wa 9 hadi wa 18 ilikuwa wanaelezea utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Lakini niwasifu hawa ni watu wazuri kweli kweli, kwa sababu kitabu hiki cha mwaka huu na kitabu hiki cha mwaka jana, mambo ndio yale yale, lakini kama ingekuwa ni wanafunzi basi

wangekuwa ni wanafunzi mahodari sana, kwa sababu anakopia mwalimu hajui kama mwanafunzi huyu kamkopia mwanafunzi mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, maneno yaliyoandikwa humu mradi wa kuimarisha usimamizi wa mazingira na mengineyo. Maneno haya yameandikwa na yakawekwa vyengine ambapo pia hayapotezi maana yake. Kwa kweli nakushukuru una wataalamu wazuri sana wanaoweza kukibingirisha Kiswahili wakakiweka vyema na wakakitumia na msomaji akaridhika na vile ambavyo Kiswahili kimeelekezwa.

Sasa katika miradi hii, mimi nataka nigusie miradi michache sana. Mradi wa kwanza nitakaozungumzia ni mradi wa kuimarisha usimamizi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa kweli suala hili ni muhimu sana, mabadiliko ya tabia nchi ni jambo ambalo limetukumba katika dunia hii. Sasa ni vipi ambavyo tutaweza kukabiliana nayo, wakati ambao kila siku, kila dakika tunachafua na kuharibu mazingira sana, upo uharibifu wa maumbile na ule unaosababishwa na mwanadamu, kukata miti na mengineyo ndio tunasababisha sisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hali hii tunayokwenda nayo tunaharibu vyanzo vya maji, tunaharibu maeneo ya kilimo mbali mbali, hatimaye nchi baada ya muda mfupi huenda ikawa nusu jangwa kutokana na uharibifu tunaosababisha sisi wanadamu. Kwa hivyo, ofisi yako Mhe. Mwenyekiti, ina kazi kubwa na ngumu ya kuweza kukabiliana na matukio haya makubwa yanayotukabili.

Mhe. Mwenyekiti, mradi mwengine kidogo nitakaouzungumzia ni huu mradi wa kuangamiza kunguru weusi. Hawa kunguru inaelekea kuwa ni tatizo, ndio maana serikali kwa makusudi tena kwa wizara mbili tofauti kukamata bunduki, yaani sikusudii bunduki kama bunduki, yaani kutafuta njia ya kuwaangamiza ili kuwapunguza. Kwa vyovyote serikali imefanya utafiti na wamejua athari wanazoleta katika nchi ama za mazingira au vyenginevyo na ndio maana ikaamua kuwaangamiza hawa ndege. Mhe. Mwenyekiti, kama ndege hawa wangelikuwa wana asili ya Zanzibar, basi mimi nisingelikubali kuwa waangamizwe lakini hawa ndege ni wakuja, wapi walikotokea sijui, lakini hawa ndege kama wangelikuwa ni watu basi wasingelipewa Uzanzibari Ukaazi, kwa sababu si pao hapa.

Kwa hivyo, kwa kuwa ni ndege wageni na pengine wanatuharibia ndege wetu basi ndio maana serikali ikachukua zoezi la makusudi la kuwangamiza na inatumia fedha nyingi kidogo kwa ajili ya kufanya zoezi hili. Lengo sijui ni kuwangamiza wangapi, kwa sababu kitabu kimeonesha wangapi wameshaangamizwa na lengo ni wangapi na leo likifikiwa itakuwa tumetumi kiasi gani?

Mhe. Mwenyekiti, ukiacha hawa kunguru ambao hawana bahati hapa Zanzibar hakuna ndege wengine waharibifu ambao serikali imewabaini. Kwa mfano, kuna panya ambao ni waharibifu wa mazao mashamba na hata majumbani na wanyama au ndege wengine kadhaa, lakini hawa bado hakuna na mkakati wowote wa kiserikali kwa ajili ya kuwachukulia hatua za kinidhamu kama tulivyowachulikia hawa kunguru. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu mradi wa kuendeleza elimu ya mazingira. Kwa kweli hili ni jambo muhimu sana, kwa sababu mazingira yameharibika, yanaharibika, tunayaharibu na tutaendelea kuyaharibu. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mwenyekiti, wananchi pamoja na jamii kwa jumla wanapaswa wapatiwe elimu ya kutosha ili waweze kudhibiti huu uharibifu wa mazingira tusiendelee, kwa sababu tukiendelea iko siku hata maeneo ya kupata maji tutakosa. Kwa mfano, Mhe. Mwenyekiti, kuna baadhi ya wakulima wanaolima kando kando ya miti ambavyo ni vyanzo vya maji wanakata miti na badala yake wanayatupa ndani ya ule mto.

Kwanza kukata mti unaharibu mazingira, majani pamoja na matawi ya ule mti kuyatupa mtoni inakuwa mto anaufukia. Kwa hivyo, baada ya muda mfupi mito mingi itapotea. Mhe. Mwenyekiti, ardhi itakuja juu na kupoteza rutba yake, mvua zimekuwa adimu sana, basi tutakuja kujikuta tupo pahala ambapo hatukutegemea kuwa tufike hapo. Kwa hivyo, Idara hii ya Mazingira inayo kazi kubwa tena ngumu ya kutuelimisha sisi wananchi, ili tuweze kufuata sheria na kanuni za mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, mradi mwengine ni kuhusu ujenzi wa Chuo cha Kurekebisha Tabia za Watu Wanaotumia Dawa za Kulevya. Kwa kweli chuo hichi ni muhimu sana na kinahitaji kisimamiwe ili kimalizike kwa lengo la wale watumiaji wawepo pale kwa ajili ya kuelimishwa na huenda baadhi yao wakaelekea.

Lakini kujenga chuo na kuwaweka waathirika bila ya kutafuta njia za kudhibiti uingiaji, uuzaji na utumiaji wa madawa itakuwa tunatwanga maji ndani ya kinu na wala maji hayatwangiki. Kwa maana hiyo, lazima tutafute njia ya kudhibiti uingiaji, uuzaji pamoja na utumiaji ili hawa ambao tayari wameathirika basi tuweze kuwarekebisha na ongezeko lipungue mwaka hadi mwaka na hatimaye janga hili liondoke. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa kwenye kamati tulikwenda kwenye vituo mbali mbali vya vijana hawa walioathirika na wengine wanakwambia mimi nimetumia miaka 15, wengine ikipita ndege wanasema ndege ya kwangu. Sasa tubadilishe lugha hizi na vipi tutabadilika? Kwa hiyo, lazima

kama alivyotangulia msemaji aliyeondoka kwamba serikali iwe na juhudi za makusudi kama alivyosema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk mara nyingi kuwa serikali lazima iwe *serious*, kwa lengo la kuokoa taifa na janga hili, kwa sababu taifa ni vijana na sisi wengine tuko kama saa hizi, yaani zaidi ya *hidaashara* na *thinaashara* tena.

Kwa kweli hii *generation* inayochipua sio ipite ndege aseme ile ndege ya kwangu au ipite meli aseme meli ya kwangu. Kwa maana hiyo, lazima serikali ijenge utamaduni wa kuweza kuyabadilisha mambo haya na watoto wetu waepukane na majanga haya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika 5.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, mimi mungelinionea huruma kwa sababu *art* yangu ya kusema ni pole pole, yaani neno moja nikisema basi la pili mpaka nilitafute. Lakini kwa kuwa umeshaniambia hivyo basi naomba nimalizie kwa haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, natoa pongezi maalum na dhati kabisa kwa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu Chama cha Mapinduzi ni chama makini na chenye mtazamo mzuri kweli katika taasisi hii tuliomo imetuingizia makada wazuri sana na hawa tungeomba tuwalee, tuwalinde pamoja na kuwapigia debe, ili wazidi kuwa makada wazuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilivutika sana na nilipata fahari ya aina fulani kuona kijana mwenye asili ya kwetu Kengeja jinsi alivyokuwa makini kwenye michango yake jana. Halikadhalika Mhe. Mwenyekiti, dada yangu, rafiki yangu *schoolmate* wangu Mhe. Asha Bakari Makame. Kwa kweli watu wawili hawa walitupa funzo la kutosha na ikiwezekana hotuba zao basi zichukuliwe, kwa ajili ya kuzisambaza na kuelimisha wengine namna ya kuzungumza katika vyombo kama hivi. *(Makofi)*

Mhe. mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakushukuru sana na anayefuatia ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadaye anafuatia Mhe. Marina Joel Thomas.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru muumba wangu Mwenyezi Mungu Mtukufu Azza Wajalla, kwa kunidiriki uhai na uzima wa afya na mimi kusimama hapa tena mara hii nikitoa mchango wangu katika bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe pia kwa kuniona kwenye kiti chako kikubwa huko ukanipa fursa na mimi nichangie.

Tatu Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye ni dada yangu na mpiga kura wangu Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake, hata pale nilipomuomba aisome yote kwa ukamilifu na wasi wasi kutokana na hali yake, lakini aliweza kuimudu kuimaliza vizuri kabisa na sauti haikutetereka hata kidogo. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani na pongezi hizo naomba sasa niingie kwenye mchango wangu. Awali kabisa Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyofanya siku ya Ijumaa katika kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, naomba uniruhusu kwamba badala ya kwenda kwenye fungu moja moja nahofia nitamaliza muda wangu wote. Lakini kwa sababu Kanuni za Kibunge haziruhusu kumshurutisha mtu, Kanuni za Kibunge kwani Baraza la Wawakilishi ni Bunge Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba nitaje yale maeneo ambayo atayarishe maelezo mazuri tu wakati wa kuja kupitisha vifungu kesho tukijaalia, ili tuweze kuja kupata maelezo ya kina na tusije tukamsumbua na iwe mambo yake mwanana kama yalivyokuwa jana katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Katika mambo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba vifungu vifuatavyo. Kwanza posho maalum, takriban katika maeneo yote na katika hili nikumbushe tu serikali kwamba jana tulipopitisha Ofisi ya Makamu wa Pili tuliomba na tukaahidiwa na wala wasije wakadhani tumesahau, kwamba tuliomba kupata *breakdown*, yaani ule undani wa kilichomo katika posho maalum analipwa nani na kwa mtiririko gani. Sasa leo tumeahidiwa tutapewa lakini inakaribia kumalizika siku bado hatujapewa, nakumbusha Mhe. Mwenyekiti, tunalihitaji ili lituongoze kwa bajeti zilizobakia.

Vile vile kuhusu posho, vikao na kamati, matengenezo ya zana hasa vifaa vya magari, gharama za vifaa na huduma hasa gharama za vifaa vya uchapaji, viburudishaji, gharama za safari, gharama za mafuta na vilainisho, vifaa na huduma za ofisi, gharama za kukodishwa ukumbi, huduma za mtandao, matengenezo ya nyumba na ofisi, gharama za mafunzo.

Vifungu vyengine ni misaada ya kijamii na hili hasa naliulizia kwa mnasaba wa Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na kodi ya nyumba, na hii hasa niseme kama alivyosema Mhe. Mbarouk Wadi Mussa nimeshtuka kama mwaka jana kwenye kodi ya nyumba bajeti ilikuwa ni milioni 24, lakini mwaka huu 98,150,000/= kwenye ukurasa wa 93 wa kitabu cha makadirio ya mapato na matumizi ningeomba maelezo.
Mhe. Mwenyekiti, pia katika mafungu haya yanayohusu hesabu niseme kwamba bado napata tabu kuielewa serikali yetu, kwamba vipi serikali moja

inayoongozwa na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika kuandaa bajeti ikiwa ni ofisi moja inakuwaje ama inatoa au inakubali utaratibu tofauti wa kupanga bajeti kwa wizara tofauti za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni serikali moja. Nalisema hilo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika ofisi hii nilichokigundua fungu la mishahara kwa idara zote limewekwa chini ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji, kwa hivyo inakuwa tabu kupima ule mtiririko wa kila mwaka, lakini jana tulipopitisha Ofisi ya Makamu wa Pili tumeona kila idara imeekewa fungu lake. *(Makofi).*

Sasa najiuliza huu muongozo ni tofauti? Kama muongozo ni mmoja vipi wizara zinaachiwa kila mmoja kupanga vyake kwa sababu wakisharejesha hawa lile jukumu la kutayarisha kitabu hiki kikubwa ni Wizara ya Fedha, sasa vipi inakubali? Mhe. Mwenyekiti, hali hii haioneshi picha ya serikali makini kwamba haina mtiririko unaofanana katika kupanga bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwenye mafungu kwa kuzungumzia fungu moja makhsusi nimtahadharishe Mhe. Waziri kwamba hesabu zake zina matatizo na kama zina matatizo basi na wajumbe tunaweza kuwa na matatizo wakati wa kupitisha. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba bajeti ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji katika kitabu hiki kikubwa cha mahesabu ya bajeti jumla yake imewekwa ni bilioni 1,329,827,000/= na bajeti hiyo au nambari hizo unazikuta kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri katika kiambatisho Nam. 11 kilichopo ukurasa wa 68 Idara ya Uendeshaji na Utumishi unazikuta fedha zinazowiana na hizi ambazo nimezisoma hapa.

Lakini kitabu hicho ambacho linalo fungu linalowiana na hili ukisoma kwenye maelezo katika Idara ya Utumishi wa Uendeshaji, Mhe. Waziri wakati alipokuwa akituomba hapa ameomba ukurasa wa 22 wa kitabu chake, Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Ukurasa wa 22 wa kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, unaeleza hivi:-

> “Naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi bilioni 1,615,931,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 292,427,000/= kwa ajili ya kuendesha kazi na shilingi bilioni 1,323,504,000/= kwa ajili ya mishahara”.

Mhe. Mwenyekiti, hazioani kwa sababu huku kuna bilioni 1.3 na kule kuna bilioni 1.6, yaani hazioani hata ndani ya kitabu chenyewe baina ya maelezo yaliomo ndani ya hotuba na kiambatanisho chake ambacho nimekisoma Nam.

11. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho atupe ufafanuzi wa hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya nambari sasa naomba niende kwenye hotuba. Naomba nianze kwenye Ofisi ya Faragha kwenye ukurasa wa 8 wa hotuba yake Mhe. Waziri ametuambia kwamba *paragraph* ya 17 Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu.

Kitabu cha hotuba *paragraph* ya 17 inaeleza hivi:-

> "Katika kuimarisha Ofisi ya Faragha vifaa mbali mbali vimenunuliwa likiwemo jenereta moja la *KVA* 70".

Sasa kwenye bajeti ambayo tunayoiomba mwaka huu pia kuna fungu la jenereta. Kwa hivyo, hapa naomba Mhe. Waziri anisaidie tunalo deni au jenereta lililonunuliwa halijatosha ama linahudumia shughuli tofauti. Vile vile jambo jengine ambalo nataka nizungumzie suala moja la kutowiana baina ya fedha tunazotumia katika shughuli mbali mbali na matokeo ya kazi Mhe. Mwenyekiti, na huo ndio msingi hasa wa hoja yangu.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepewa jukumu la kusimamia shughuli ambazo zinaingia kila pahala na mimi neno Mtambuka silitumii, maana yake sijui nini na wala sijui limetokea wapi. Lakini nasema imepangiwa shughuli na majukumu ambayo yameenea na katika kila sekta ya maisha na zinaingia katika wizara na afisi zote za serikali. Kwa hivyo zina umuhimu wake. Sasa ukiangalia matumizi yanavyokwenda Mhe. Mwenyekiti, yanaoana na katika hili naomba nianze na suala zima la UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya UKIMWI kila mwaka imekuwa ikiletewa maombi na tukiidhinishia mabilioni ya fedha, lakini tija ya kazi yake haiendani na fedha zinazoidhinishwa. *(Makofi)*

Mwaka huu katika bajeti ya maendeleo kumetengwa shilingi bilioni 1,769,000,000/= ambazo katika hizo bilioni 1,719,000,000/= ni fedha za wahisani na milioni 50,000,000/= ni mchango wa SMZ. Mhe. Mwenyekiti, fedha hiyo ukichanganya na milioni 768,000,000/= ya mishahara na shughuli za uendeshaji kwa maana ya *OC*, inakupa jumla ya bilioni 2,537,000,000/= zilizoombwa kwa mwaka huu.

Vile vile tukiangalia mwaka jana fedha zinazolingana na hizo ziliidhinishwa Mhe. Mwenyekiti, lakini katika hotuba yake Mhe. Waziri mwenyewe anatuambia kwamba UKIMWI katika utafiti uliofanywa umeonekana

kuongezeka Zanzibar kutoka asilimia 0.6 kuja asilimia 1 na hilo ni ongezeko la asilimia 0.4.

Sasa ukiichukua kwa idadi ilivyokua maana yake kwa ujumla wake, lakini ukiigawa kiasilimia maana yake kiwango cha kuongezeka kwa UKIMWI kimepanda kwa asilimia kama 66 yaani ukiuchukua 0.6 kama ndio *base* yako halafu pakaongezeka 0.4 katika 0.6 ni asilimia 66 ongezeko Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, ninajiuliza kwamba fedha hizi zote zinazoidhinishwa mbona tija yake inaonekana ni kuongezeka UKIMWI badala ya kupungua? *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, bila ya kupoteza wakati na hili nawaomba wajumbe wenzangu wakati ukifika mimi kabisa natumia Kanuni ya 98(6) kutangaza kwamba naondosha shilingi katika matumizi ya fungu hili. *Vote* ya 12 ya Tume ya UKIMWI mimi Mhe. Mwenyekiti, nitaikata na ninawaomba wenzangu waniridhie kwamba hawa tuwakatie fedha, kwa sababu fedha hizi hazionekani tija yake Mhe. Mwenyekiti, isipokuwa ikiwa Mhe. Waziri atakuja kunitosheleza kwa maelezo yake ya kina kwamba nione tija yake, lakini mimi kwa takwimu zake sioni tija yake.

Jambo hili linazungumzwa sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba katika tume hii kumekuwa na utaratibu wa matumizi ya fedha yako ovyo katika mambo ya shughuli za semina, makongamano, warsha na imekuwa ndio mtindo, lakini ukitizama kama ninavyosema *output* au tija ama matokeo yake ni haya kwamba UKIMWI kiwango chake kinaongezeka Zanzibar, sasa faida yake nini Mhe. Mwenyekiti, naomba kupata maelezo. Kwa hivyo, kwa nini tuidhinishe fungu hili la bilioni 2,537,000,000/=, ambazo kuna fungu la fedha za miradi ya maendeleo pamoja na zile za uendeshaji ambalo limekuwa kubwa kiasi hichi. Hilo moja Mhe. Mwenyekiti.

Pili Mhe. Mwenyekiti, ninakuja katika suala zima la mazingira, vile vile tumeombwa fedha humu. Katika suala hili mimi zaidi nataka nisaidie Mhe. Mwenyekiti, na wala sizungumzii uchafuzi na uharibifu wa mazingira ambao tumeuzoea isipokuwa nazungumzia hapa kwa sababu ameizungumzia pia.

Katika kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri kwenye ukurasa wa 6 ametuelezea vipaumbele vya ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Miongoni mwa vipaumbele hivyo ni pamoja na:

1. Kuandaa mkakati wa usimamizi wa taka ambao utatoa vipaumbele vya hatua zinazofaa kuchukuliwa.
2. Kupunguza uchufuzi usiofuata utaratibu wa maliasili zisizorejesheka na

3. Kukabiliana na athari za kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna moja nataka niipongeze Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Katika kukabiliana na athari za kuhimili mabadiliko ya tabianchi, nataka niwapongeze sana na katika kitabu hichi nimefurahi kuna kielelezo katika mradi mzima wa kuwapatia maji safi na salama wananchi wa Nungwi.

Kwa kweli ilikuwa ni tatizo kubwa sana kwa wananchi wa pale na mimi nakumbuka miaka mingi sana kila ukenda pale tatizo ni kubwa sana, lakini tatizo hili limemalizwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika mradi huu mkubwa walioupeleka hili napongeza. *(Makofi).*

Lakini nazungumza upande mwengine haya Mhe. Mwenyekiti, yanayohusu kupunguza uchufuzi usiofuata utaratibu wa maliasili zisizorejesheka. Mhe. Mwenyekiti, kila mwaka tukija hapa tunazungumza kwamba tatizo hili linaongezeka. Sasa mimi hujiuliza Idara ya Mazingira inakwazwa na nini katika kuzuia hili. Vile vile kwenye suala la taka na wala sitaki kwenda mbali Mji Mkongwe tu jimbo langu Mhe. Mwenyekiti, ni ushahidi tosha jinsi gani serikali ilivyoshindwa kukabiliana na suala la uzoaji taka na usafishaji wa mji.

Kwa hivyo, hapa namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho aje anisaidie maelezo kinachokwaza ni kipi ni kwamba tunazo mamlaka nyingi zinazohusika, kwa sababu Idara ya Mazingira ndio idara ya msimamizi mkuu na kama nilivyosema mwanzo kwamba inasimamia *cross cutting issue*, yaani shughuli ambayo inaingia kila pahala, hivi imekosa mamlaka ya kuwasimamia wengine katika kuhakikisha usafi wa mji na uzoaji wa taka ambazo zimezagaa kila pahala.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo yanatia kinyaa tena aibu katika mji wetu. Sasa inawezekana kwa mfano kwa mjini Baraza la Manispaa halifanyi kazi yake. Lakini najuiliza nini wajibu au *role* ya Idara ya Mazingira katika kusimamia hilo? Sasa kama hawa mamlaka ya usimamizi kwa idara nyengine au kazi nyengine za serikali, basi haina faida ya kuambiwa kwamba idara hii ni *cross cutting* kwamba ina uwezo wa kuingia kila pahala na kuweza kufanya maamuzi yake, kama ni hivyo basi tuiondoe tu.

Kwa maana hiyo, hili linakuja kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sisi wengine tunazungumza na watendaji wake Mhe. Waziri na wanatuambia kwamba unakuta wao wanalalamika kama tunavyolalamika sisi, kwamba wanaandika mapendekezo wanatoa ripoti na halafu katika utekelezaji hakuna hatua inayochukuliwa. Sasa tatizo liko wapi na katika hili Mhe. Waziri awe wazi ili tusimbebeshe yeye mzigo na awe wazi atuambie hapa. Mhe. Mwenyekiti,

ikiwa wizara nyengine hazitekelezi maelekezo yao basi tujue faida yake nini kuwa wasisimamizi wa suala hili la mazingira na katika hili naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli mimi naamini wakitaka wanaweza katika hili la mazingira Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ile mifuko ya *plastic* kwa kiasi kikubwa wameliweza na leo Zanzibar inapigiwa mfano katika nchi ambayo imejitahidi kudhibiti masuala ya matumizi ya mifuko ya *plastic* na kwa hili nawapongeza sana. *(Makofi).*

Lakini kama wameliweza hilo kwa nini haya mengine yashindwe, hivi kwa nini uchafu wa taka zilizozagaa kila pahala ushinde? Kwa nini makaro mabovu yanayomwaga maji machafu kila pahala lishindikane? Kwa nini kuchukua maliasili zisizorejesheka imekuwa ndio mtindo wa kawaida bila ya hatua zozote za kurekebisha? Sasa wameliweza suala la mifuko ya *plastic* na haya kwa nini washindwe, tunaomba maelezo Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi).*

Nikiendelea na mchango wangu sasa nataka nizungumzie kuhusu suala la watu wenye ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nikijiuliza hapa kwamba kwenye hotuba hii kuna vikundi hivi ambavyo vimesaidiwa na nadhani kwenye ukurasa wa 28 *paragraph* ya 74 Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Ukurasa wa 28 *paragraph* ya 74 unaeleza hivi:-

“Jumuia 10 za watu wenye ulemavu zimepatiwa ruzuku ya shilingi 1,700,000/= kwa kila mmoja kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kawaida. Jumuia hizo ni CHAVIZA, ZANAB, UWZ, JMZ, SADZ, JUWAUZA, ZADA, ZACDID, ZAPDD na SOZ.”

Hizi jumuia 10 Mhe. Mwenyekiti, zimesaidiwa shilingi 1,700,000/= kwa kila moja. Najiuliza hivyo shilingi 1,700,000/= kwa mwaka mzima kwa jumuiya kama hii wakati hakuna njia nyengine ya kuwafanya hawa wakaendesha shughuli zao. Inatoa tija gani na kama ambavyo nitakuja katika dawa za kulevya liko lile lile la *sober house* kusaidia shilingi 1,700,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, unakuta ndani ya sera kwamba matokeo ya kazi hayalingani na yenye gharama kubwa ya uendeshaji wa shughuli yenyewe. Unakuta bajeti kubwa ya serikali yetu kwenye wizara zake imekuwa ikijikita katika gharama za uendeshaji tu ili uhalalishwe kwamba unatumia, kwa mfano milioni mia tano za uendeshaji lakini tija yenyewe inapowafika wale walengwa ni shilingi 1,700,000/=. Mhe. Mwenyekiti, inahalalisha hiyo kweli kutumia fedha hiyo ya uendeshaji kwa sababu anayetakiwa ahudumie haipati tija yake.

Kwa hivyo suala hili mimi Mhe. Mwenyekiti, linanipa shida sana ndio maana tunasema kwamba mara nyingi tunakwenda katika ofisi za serikali, kazi kubwa imekuwa ni kazi ya kukaa ofisini kuandika ripoti na kufanya utafiti lakini tija katika kubadilisha maisha wale wanaohudumiwa ikiwa ni walemavu, ikiwa ni watu wenye kula dawa za kulevya, ikiwa ni waathirika wa kimazingira, hazionekani tija yake. Hili kusema kweli sasa hivi tunaijadili hili lipo takriban katika kila wizara, sekta za maisha, utakuja kuona kila wizara ikifika hapa. Kwa hivyo nilikuwa nataka akija anieleze Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika sehemu ya walemavu, kuna suala la majengo ya serikali. Katika sera yao ukirudi kule kule kwenye ukurasa wa 5 kwenye malengo au vipaumbele vya ofisi ni pamoja na kuweka mazingira ambavyo vinapelekea huduma kwa watu wenye ulemavu ziwe rahisi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, najiuliza hili ni kosa la usimamizi, achilia mbali kusimamia taasisi za binafsi. Taasisi za serikali zenyewe haziweki mazingira mazuri ya watu wenye ulemavu kuweza kuwafikia na kuweza kutumia hudumia zake.

Mimi najiuliza kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza inafanya shughuli gani ikiwa hata majengo haya yanayojengwa na mengine hata ya zamani bado ujenzi wake unaruhusu kuweka angalau kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma asubuhi leo, kwamba angalau kuweka ramani za kuweza kuwafikia, inashughulika na kitu gani. Hayo majengo mengine ambayo ujenzi wake unaruhusu kuwekwa *lift* na kuwasaidia watu wenye ulemavu kuweza kufika hapa. Yeye mwenyewe Mhe. Waziri shahidi Mkurugenzi akija hapa anavyopata shida ya kufika juu na jengo ni hili hili la Baraza la Wawakilishi. Sasa najiuliza tunafanya shughuli gani katika kusimamia kutoa huduma hizi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumze la ukimwi na limezungumzwa katika kuzungumzia bajeti. Tume hii tunaitengea mabilioni ya fedha lakini ukitizama mara nyengine huduma za waathirika wa ukimwi. Mimi nategemea Tume ya Ukimwi inafanya kazi mbili, moja ni kupambana au kuendesha kampeni ya kujaribu kuelimisha watu wasije wakaathirika.

Lakini la pili ni kuwasaidia wale ambao tayari ni waathirika. Katika jimbo langu la Mji Mkongwe kuna jumuiya ambayo Mhe. Waziri katika hotuba yake kaitaja *ZAPHA+*. Ukitizame pale inahemewa kwa sababu imekuwa na jukumu kubwa la kuwahudumia wale waathirika pale. Ukiwakuta walivyojipanga foleni pale ya kwenda kutafuta misaada ya kuwawezesha kumudu hali zao, kwa sababu yale madawa wanayotumia zinawapelekea kupata lishe ya kutosha na nzuri. Lakini wanashindwa kwa sababu wengi kutokana na hali ya ugonjwa inawafanya wamedhoofika hata kufanya kazi hawawezi na wengine wana familia. Ndio maana nikasema kwa nini fedha

hizi zisiende kuwasaidia hawa zikawa zinatumika sehemu kubwa katika masemina, makongamano na gharama za uendeshaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea naomba nipate maelezo kwa Mhe. Waziri katika masuala ya vipaumbele vyao na masuala mazima yanayohusu utekelezaji wa shughuli mbali mbali za ofisi hii. Moja nimezungumza ni dawa za kulevya. Tuliletewa katika Baraza hili hili marekebisho ya sheria ya kupambana na dawa za kulevya ambayo moja katika malengo yake ilikuwa ni kujenga upya Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mimi naomba Waziri akija anisaidie kwamba tume ile katika kitabu chake imesema imefanya kikao kimoja tu na ile ndio inayojumuisha watu mbali mbali kutoka katika taasisi mbali mbali ambazo zinatakiwa zishirikiane katika kupambana na dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, hili ni muhimu sana aje atwambie kwa nini kumekuwa na tatizo hili na kwa bajeti yake imekuwa hata haifikii vizuri ukilinganishwa na mgao uliokuwa kwenye ile hotuba yake mwenyewe.

Mimi napongeza moja katika kusaidia kupambana na watumiaji kiasi kikubwa hali inaonekana kuna mabadiliko hata katika mitaa yetu tukipita kuna unafuu. Kuna maeneo ilikuwa ukipita imekuwa ni kawaida kukuta watu wamekaa wanasubiri pale, sasa hivi ukipita sehemu kubwa maeneo kwa mfano Kwahajitumbo, maeneo mbali mbali ya Mji Mkongwe, unaona tofauti, sesime masuala mengine ambayo kuwa siyajui. Huo ni upande mmoja wa mahitaji, ukiweza kukubaliana na wanayoyatumia utaweza kudhibiti vizuri lakini upande wa uingizaji atwambie tatizo liko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna moja la kila siku kupambana na kuwaokoa vijana kwa kuwapeleka katika *Sober House,* lakini ikiwa *supply* itaendelea kuwepo njia za kuvutia wateja, ndio kawaida ya biashara yoyote, sasa hili tutakabiliana nalo vipi. Leo nimechapa hapa kutoka kwenye mtandao, makala mbali mbali katika magazeti ya kimataifa na mengine ya nyumbani hapa yanavyoichora taswira ya Zanzibar inatisha na inatia aibu kwa nchi yetu.

Hapa Mhe. Mwenyekitik nina magazeti mbali mbali ya nje ya nchi na ya ndani ya nchi yana yanayosema kwamba,

Telegraph la Uingereza: Biashara ya dawa ya kulevya sasa imechukua nafasi ya uchumi kwa Zanzibar.

Voice of America: Zanzibar imegeuka kuwa muathirika wa biashara ya kimataifa ya dawa za kulevya.

BBC : Zanzibar imegeuka kuwa ni pepo iliyokuwa inachochewa na upata matumizi mazuri ya dawa za kulevya.

This Day: Wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya wanastawi katika kisiwa cha Zanzibar.

Daily News: Utumiaji wa dawa za kulevya kwa vijana unaongezeka Zanzibar.

Katika makala haya, inamnukuu Mkuu wa Kanisa Katoliki Zanzibar Dokta Shao akisema kwamba wanajulikana waingizaji wa dawa za kulevya. Sasa mimi nafikiri watu kama hawa wakisema bila ya shaka wanazo sababu zao. Je, tumewafuata tukawauliza wakatusaidia majina haya tukaanza kukabiliana nao.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni lilitokeza suala la *Maritime Forces*, wana maji Wacanada na Wa-Australia wanavyosema, sina uhakika kwa kushirikiana na vyombo vyetu vya ulinzi hapa kunasa dawa za kulevya zenye thamani ya dola milioni mia moja na nne. Sasa hili linakizungumkuti, alisema katika bahari karibu na Zanzibar, hatujui ndani ya mipaka ya Zanzibar au nje ya mipaka ya bahari ya Zanzibar. Kimataifa linachafu jina la Zanzibar kwa sababu kila pahali imeandikwa kwamba ni Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nasema kwamba kama hiyo *sober house* naipongeza na naisifu Ofisi ya Makamu wa Kwanza, katika suala la kupambana huku ndani, kiasi kikubwa tunaona katika baadhi ya mitaa tuliyokuwa tunaijua. Lakini katika hili suala la uingizaji panashindwa nini? Juzi tu Mhe. Mwenyekiti, tumesoma kuna mwanamke mmoja kakamatwa Misri, kaambiwa anakaa Dar-es-Salaam, lakini kwa watu wa Zanzibar kwa vile tunajuana wanasema kwamba anatoka katika maeneo ya Mji Mkongwe anakaa katika mji wa Zanzibar.

Kakamatwa na kiasi si kidogo. Mhe. Mwenyekiti, tunajiuliza kwamba hawa watu wanatajwa sio mara moja katika Baraza hili. Tunapata tatizo kwamba wananchi wetu wanavunjika moyo kwamba wanatoa taarifa mtu anakamatwa, lakini halafu baada ya siku mbili tatu anaonekana yupo mitaani tena. Tatizo liko wapi? Nini kinachokwamisha kupatikana kwa ushahidi Mhe. Mwenyekiti, hebu tuambiwe watu hawa wapo. Namuomba Waziri katika hili awe wazi atwambie.

Hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana tulitoa hoja hapa kwamba hizi *sober houses* nyumba za kusaidia vijana nyingi zinaendeshwa na watu binafsi kama si zote. Tukasema kwamba serikali lini itajenga kituo chake kwa sababu hizi nyumba za kawaida za kuishi zinageuzwa kuwa ni nyumba za kuwasaidia

vijana hawa. Lakini zile huduma zake haziwi ipasavyo tukaambiwa kwamba gharama yake ni kubwa lakini ikaambiwa angalau itajengwa kwa kuanzia mwaka jana bajeti ingetengwa milioni mia moja.

Hili sio suala la Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, mtamuonea bure. Bahati mbaya Mhe. Waziri wa Fedha hayupo. Tunaambiwa katika kuripoti Waziri kwamba hawakuingiziwa hata senti moja katika mradi ule. Tulipopambana mwaka jana hapa Waziri akatuhakikishia kwamba tunatoa hizi waanze kwanza. Mwaka mzima wa fedha umekwisha hakuna kitu. Mwaka huu zimeingizwa tena milioni mia moja, mie siamini kwamba mwaka jana hazikuingizwa kwa sababu wengi hawakuamini kwamba mwaka huu zitaingizwa.

Inaonekana zile hotuba na kauli Mhe. Mwenyekiti, za serikali ni ya kufurahisha watu lakini utekelezaji haupewi vipaumbele katika kupanga bajeti na kutoa fedha katika serikali. Sasa matokeo yake ndio, maana serikali inaishia kuwagaia *sober house* milioni moja na nusu kila mmoja wakitegemea hiyo ihudumie kwa mwaka mzima. Wengi wanaokwenda pale wanatoka katika familia za masikini wameshazimaliza familia zao kwa kung'oa mpaka milango na madirisha ya nyumba, halafu mzazi huyo anategemewa ataweza kumuhudumia mwanawe angalau laki moja kwa mwezi kuweza kumuhudumia katika *sober house*. Serikali lini itakamilisha haya, nataka maelezo ya kina juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho kabisa namtaka Mhe. Waziri akija anieleze haya kwamba mwanzo nimeeleza wasi wasi wangu juu ya mafungu haya, nikitoa mfano maalum wa Tume ya Ukimwi, nataka maelezo juu ya matumizi haya Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho haiko mbali tutakuja kuona katika kupitisha vifungu hapa, kwamba maisha hakuna maelezo. Mawaziri mara hii tunamwambia wasibebe mzigo uliokuwa si wao, waliokuwa wakipanga haya hawajui wameficha nini na wameficha wapi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka maelezo ninazo taarifa zimeandikwa mpaka kwenye mitandao kwamba katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, karibuni imekwenda kutoa msaada kwa hospitali ya wagonjwa wa akili. Msaada huu uliambiwa ati dawa zake zenye thamani ya shilingi thamanini milioni. Lakini inavyosemekana tulivyosoma katika mitandao kwamba baada ya kufuatiliwa dawa zile zimenunuliwa dukani kwa Shamsu pale Empire na baada ya kufanyiwa usaini mkubwa imeonekana kwamba thamani yake ni milioni 16, haidhuru pengine kasema milioni 10. Baada ya kutiwa kishindo inasemekana kwamba wahusika wakasema hizi pesa zilikuwa hazijatumika mpaka mwisho wa mwaka na ikifika tarehe 30 Juni zinakunjwa kunjwa zinarejeshwa Hazina. Tukaona tuzifanyie mpango zisirudi.

Sasa katika hili nataka kumpongeza, mimi taarifa nilizozisoma katika mtandao ni kwamba Waziri mwenyewe kafuatilia, katika hilo nampongeza na Katibu Mkuu Dokta Shajak kafuatilia na nimeambiwa kwake kenda kapiga picha kujiridhisha kwamba thamani yake hailingani na fedha ambazo kuwa zimetajwa. Sasa tunavyoambia kwamba wahusika ni Bodi ya Zabuni, tunapata mashaka kweli kweli Mhe. Mwenyekiti. Aje anithibitishie ukweli huo na kama ikifika Bodi za Zabuni za Wizara zetu ndio zilizoshiriki katika wizi na utafunaji wa pesa za wananchi masikini ya Mungu ambao ndio walipa kodi wa Zanzibar, tutamuamini nani Mhe. Mwenyekiti. Kwa hiyo nataka hili akija Waziri anipe maelezo ya kina ili nisije nikakwamisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio mambo yanayopatikana tukaonekana akina Jussa wakorofi tukisema tunapitisha vifungu ni kwa sababu tunasema kwamba humu kuna vichaka vinavyofichwa watu wakifika mwisho wa mwaka wanajua kukomba. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nasema tena kwamba nataka maelezo juu ya hilo na kama nilivyosema ile bajeti ya Tume ya Ukimwi naiondoshea shilingi na nitawaomba Wajumbe wenzangu katika hili tusiipitishe na kama kuna fedha za wahisani, wao watazisimamia wenyewe lakini zile zetu ambazo zinatolewa na Hazina ya Zanzibar, fedha za walipa kodi za wananchi wa Zanzibar nafikiri ni mia saba na sitini na nane milioni ambazo zinajumuisha mishahara na *OC*, mimi nitasema tuzuie. Kwa nini tuendelee kila mwaka kuchukua mabilioni huku ukimwi ukiwa unaongeza kasi.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nasema nazuia bajeti hii kwa upande wangu kuiidhinisha, siungi mkono hoja mpaka nitakapokuja kupata maelezo ya kina katika shughuli mbali mbali nilizozieleza.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuchangia kwanza nampongeza Waziri kwa ajili ya kuandaa hotuba hii pamoja na watendaji wake wote.

Mimi nitachangia katika Idara ya Mazingira, Idara ya Walemavu na Idara ya Madawa ya Kulevya. Najua wenzangu wameshachangia lakini nitakwenda kwa kifupi sana ili niwape nafasi na wao wenzangu waendelee kuchangia. Nitaanza na Idara ya Mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira ina majukumu ya kukusanya na kuhifadhi taarifa za kimazingira kama:

- Kutoa taarifa za kimazingira ili ziweze kusaidia katika kutayarisha na kutekeleza mipango na miradi ya kimaendeleo,

- Kufuatilia mwenendo wa hali ya mazingira,

- Kukabiliana na matatizo ya kimazingira,

- Kuhamasisha wadau kuchukua hatua za kuhifadhi mazingira na

- Pamoja na kutoa elimu ya mazingira kwa jamii.

Mhe. Mwenyekiti, mazingira, Ukimwi ni masuala Mtambuka. Masuala ambayo yameingia katika sekta na kila wizara. Hapa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na ushauri. Kwa vile wizara hii ni husika na mazingira, nilikuwa naiomba ichague eneo maalum. Kwa mfano lile la Kaskazini 'A' au Kaskazini 'B' ili iwe kama *pilot area* ambayo kuweza kuhifadhi haya mazingira katika kila nyanja. Kufanya hivyo itasaidia kwanza kuonekana ufanisi wa ile wizara, kwa sababu wakishughulikia eneo moja ina maana *allocation* au *resources* zitaingia hapo, wataalamu wata-*base* hapo. Ina maana itafanyika kazi ambayo itakuwa kama ni ya kihistoria. Historia ambayo itakuwa hata wale wengine wa sehemu nyengine watakuja kujifunza kutokana na eneo hilo.

Pia itasaidia katika kuendeleza maeneo mengine kirahisi zaidi wakati huku itakuwa ishaonesha ufanisi wake, kuliko kuliacha tu kwamba wizara hii imefanya kazi kidogo, wizara hii imefanya kazi kidogo lakini ikitizama eneo moja pale itachukua eneo moja la Wilaya, nguvu zake zitatupwa hapo, ina maana itakuwa inaweza ikasaidia.

Mhe. Mwenyekiti, inasemekana kuna baadhi ya maeneo hasa kwa yale maeneo ya mipunga mara nyingi maji ya chumvi yalikuwa yameshaingia katika maeneo hayo. Mfano labda Mkokotoni, hapa nilikuwa nina swali tu nimuulize Mhe. Waziri la ardhi juu ya ukubwa gani imeshaliwa na bahari kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Hapo naomba Mhe. Waziri anieleze.

Katika suala la watu wenye ulemavu. Idara ya Watu wenye Ulemavu ina jukumu la kuratibu masuala mbali mbali ya watu wenye ulemavu. Labda nataka kujua Mhe. Waziri anieleze utambuzi wa walemavu je, wizara imefanya upembuzi wa walemavu, kujua kwanza idadi halisi ya walemavu katika Zanzibar, aina ya walemavu, labda walemavu wa macho wako wangapi, walemavu wa miguu wako wangapi, walemavu wa masikio wako wangapi. Hii itasaidia kupanga mipango bora na endelevu kwa ajili ya kuwapangia watu wenye makundi maalum wenye ulemavu kuwapangia mipango yao ili iweze kusaidia kuweza kuendeleza taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima la elimu mjumuisho. Elimu mjumuisho imewezaje kuwasaidia walemavu na hasa ukizingatia madarasa wanaosomea inakuwa mchanganyiko baina ya walemavu na watu wasiokuwa na ulemavu. Je, kufaulu kwao kukoje, kiwango chao cha elimu kikoje na imeweza kuzingatia yote hayo. Pia katika maksi za kufaulu kwao wanaangaliwa vipi. Mfano kupasi inatakiwa upate maksi 50 je, mlemavu anaangaliwa vipi kutokana na hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye madawa ya kulevya, hili ni tatizo kubwa kwa taifa. Tukizingatia vijana wengi wamejiingiza katika madawa ya kulevya, vijana ambao ni taifa letu la kesho na ni watendaji kazi wa taifa la baadae. Lakini hapa nimuulize Mhe. Waziri tunaweza kusema ni asilimia ngapi ya Wazanzibari wanaotumia dawa za kulevya na serikali imetilia mkazo gani kuhusu suala zima la ujenzi wa kituo cha kubadilisha tabia cha Tunguu ili iweze kuwanusuru vijana wetu hawa walioathirika na madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri ana mikakati gani ya kupunguza idadi ya vijana ambao wanaathirika na madawa ya kulevya likiwemo suala zima la udhibiti na uingizaji wa madawa yenyewe. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, nianze kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa pamoja na wenzangu Mwenyezi Mungu aliyetupa pumzi kufika hapa tena leo.

Niseme bajeti ya leo ni bajeti ambayo inazungumza majanga ambayo ni mazito na wenye dhamana ya mambo haya ni sisi sote Wazanzibari. Mhe. Mwenyekiti, leo ni Mwezi 15 Shaaban kwa Zanzibar nasema ni siku ambayo Kasmatriski ni jambo kubwa sana na hasa mambo tunayoyazungumza leo haya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametoa hotuba yake na akaelezea masuala yote ya umuhimu wa madawa ya kulevya, walemavu, janga la mazingira kwa taifa na Ukimwi. Ukenda siku kama ya leo tunayoiadhimisha Waislamu na wasiokuwa Waislamu yanakatazwa mambo haya yote ya ubadhirifu katika sehemu ya mazingira ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na suala hili la madawa ya kulevya. Mhe. Mwenyekiti, madawa haya ya kulevya labda nataka nimwambie tu Mhe. Waziri kwamba mporomoko wa maadili ni moja ambayo yametufanya hapa tulipofika taifa letu hili la Zanzibar. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, madawa ya kulevya yanahitaji mashirikiano makubwa na taasisi zote ikiwemo Ofisi ya

Makamu wa Kwanza wa Rais, Jeshi la Polisi, Mahakama na sehemu nyengine zote hizi zinahitajika kuwa na *co-ordination* ya pamoja ili kufikia lengo ambalo hili ambalo tunataka kulifikia. Nasema kwa Zanzibar uwezo tunao, nia tunayo na tunaweza kulimaliza tatizo hili kama tutakuwa na nia moja na tutakuwa na uadilifu wetu sisi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni ndogo sana na unaposema suala la madawa ya kulevya hili jambo kama nilivyosema, nitatoa mfano mmoja. Mhe. Mwenyekiti, awamu iliyopita ya Rais Mstaafu Mhe. Dokta Amani Abeid Karume, msaidizi wake alikuwa ni Mhe. Waziri Kiongozi Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, aliitisha kikao cha Kamati kuhusu masuala ya madawa ya kulevya pale kwenye Baraza la Wawakilishi lililokuwepo. Iliitwa Kamati yeye ndiye akiwa Waziri Kiongozi ambaye sasa hivi ni Waziri Kiongozi Mstaafu na walipata fununu kulikuwa na suala zima la *co-ordination* namna ya kuwakamata wahusika wa suala la madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikwambie pamoja na Mhe. Waziri, kikao kilipomalizika tu *information* ile ilivuja na ilipovuja wahusika wakawa wameipata, na lile suala lilikuwa lifanyiwe kazi na lilikuwepo. Mimi nilimtafuta mchana Mhe. Waziri Kiongozi Nahodha nikamwambia bwana Mhe. Waziri Kiongozi suala letu siye ni maadili hatuko wakweli, kikao mlichokifanya saa 4:00 - 7:00, uhakika saa 7:10 watu wametoka tayari mmoja kesharusha ujumbe ndani, kwa hivyo hilo suala mnalotaka kulifanya halipo tena. Akanambia hivi kweli Raza, nikamwambia nakwambia.

Sasa ninachotaka kusema kwamba kama tutakuwa na nia thabiti na kama tunaitakia mema nchi yetu, hili suala kwa Zanzibar haliwezekani likashindikana kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu lakini yote haya yanataka *co-ordination* ya watendaji na hasa jeshi la Polisi. Mimi naamini kuna vijana wa jeshi la Polisi wana watendaji wazuri sana. Lakini ninachotaka kutoa mawazo yangu kwamba bila ya *co-ordination* kwa sababu Wizara inayohusika haina mamlaka ya kwenda kukamata. Wizara inayohusika haina mamlaka ya kuweza kumfunga.

Sasa haya yanataka *co-ordination* yetu siye sote, tukifikia hapo tutaweza kuona hawa mnaokuwa mnawaendea, wale mapapa wapo lakini njia ya kuwafika inataka *co-ordination* na njia inayotaka tuwe na uadilifu katika masuala yetu ya pamoja. Kwa hivyo Mhe. Waziri nilikuwa nataka kuwaambia kwamba *co-ordination* ni jambo muhimu sana katika taasisi kwa kuweza kufanikisha jambo hili.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, hili suala la mchanga na masuala ya mazingira. Mimi narejea tena pale pale bila *co-ordination* na wizara

zinazohusika, tatizo hili litaendelea. Kwani humu sote tuliokuwemo tunaongozwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa ikiwa waziri tunapiga kelele na suala la mchanga limekuwa ni janga la taifa. Huyo anayetoa kibali yumo kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sasa mheshimiwa ni sawa sawa na sikio kulikama hapa halafu unakuja kulikamata huku. Kwa hivyo hili suala bila ya *co-ordination* kwa sababu anayetoa kibali yumo ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tena kwa watendaji pamoja na sehemu zote, watu wakae pamoja watafakari kwa maslahi ya nchi, nini tunachotaka, shimo gani litatuathiri.

Mhe. Mwenyekiti, wakati watendaji wapo na tunao wazuri, tuna wataalamu wazuri sehemu zote ni kukaa kwa pamoja kuona jinsi gani tunaweza kuyaondosha matatizo haya ambayo yanaweza kutuathiri. Leo tukiona kwenye vyombo vya habari sehemu za visiwa katika pwani zote hizo tunazoziona 40, 41, 36 namna gani Zanzibar imeathirika visiwa vyengu vya Unguja na Pemba katika masuala haya.

Lakini haya mambo yanafahamika hata sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, kama hatukuwa wakweli, leo Mwanakwerekwe padogo tu hapo, pana Diwani, kuna Sheha, wote hawa wamo ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini utakwenda jioni utapita utakuta mifupa ya binadamu pale. Mimi mwenyewe nimeshuhudia sehemu yetu pale Mwanakwerekwe, nguzo za umeme tunasikia kwenye redio zinaathirika anayetoa kibali nani, ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa ni kukaa pamoja tukinaiyane tuwe wakweli tuona kwamba haya mambo tunayazuia kwa pamoja. Lakini useme wewe unazuia, huyu katoa kibali, huwezi kumshtaki. Ndioa tunaona tunapata mfarakano ambao tusioutakia mema Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri turejee kwenye utamaduni wetu wote ni mashirikiano kutoana elimu ili tufike hapo tunapotaka kufika kwa faida ya vizazi vijavyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la walemavu ni mitihani ya Mwenyezi Mungu hakuna mtu anayetaka mwenzake yamfike. Ni mitihani ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu ametwambia nitaleta kila mitihani kwa binadamu lakini mwisho anasemaje wapeni habari wanaosubiri. Kwa hivyo hii ni mitihani lakini sasa lazima na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tuone namna gani tunaweza kuwasaidia na tunakaa sisi binafsi namna ya kuwasaidia walemavu.

Kwa mfano majengo ya serikali alhamdulillahi inaanza kujenga majengo mazuri kabisa lakini wafikirie vile vile walemavu katika suala la wao kuwape utaratibu wa kuweza kufika ghorofa mbili, tatu zinahitajika zana kama *lift* kuwepo na utaratibu maalum kwamba Wizara inajenga hii lakini imfikirie

yule ambaye hawezi kupanda ngazi. Kama tumetumia shilingi kumi, mimi sioni kwamba unaongeza sumni au shilingi ukasema ni hasara kwa sababu ya maslahi ya wenzetu. Kwa hivyo majengo ambayo tunakwenda nayo kwa kipindi hiki lazima kuwe na utaratibu wa kuwasaidia walemavu na wenzetu wanashindwa kupanda ngazi. Maana unaweza kumwambia yuko ghorofa ya nne nipe ajira. Sasa kama huna sehemu ina maana umemnyima haki yake kwa sababu tulikuwa hatukufikira *vision* ya mambo ambayo tunayokwenda nayo mbele. Mwenyekiti, hili suala naomba litizamwe katika sehemu zote kwenye taasisi binafsi, taasisi za serikali na kutoa upendeleo kwa mitihani iliyowafika kuona jinsi gani tunaweza kuwasaidia hata katika masuala ya mikopo au mambo mengine ambayo yatawawezesha wakajituma wakaweza kujisaidia wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukimwi mimi ninafikiri kwa utamaduni wa Zanzibar ni kuwaomba Mashekhe na viongozi wa dini wa Kiislamu na wasiokuwa Wakiislamu ni kuimarisha kutoa mawaidha ya dini katika suala la ukimwi. Lakini ukija katika masuala ambayo kwa Zanzibar hatuna utamaduni nayo hatutaweza kuyaondosha kwa sababu utasema bwana kujikinga chukua mipira sita, kwa Zanzibar utamaduni huo hatuna. Sasa utamaduni wa Zanzibar nchi yetu haina dini, Katiba yetu haielezei kwamba hakuna dini angeweza kuabudu sanamu, mbuyu, ng'ombe ruhusa lakini Zanzibar tuna utamaduni.

Mimi ninafikiri Mashekhe na viongozi wa dini pande zote Waislamu na wasiokuwa Waislamu watumie nafasi kubwa sana katika kuwahamasisha vijana na vyombo vyetu vya habari hasa vya serikali vitumie mawaidha sana juu ya suala hili la zinaa, ninafikiri hiyo itasaidia sana katika masuala kuliko masuala ambayo sio utamaduni naona yatazidi kuongezeka. Maana unampelekea mtu shamba unamwambia bwana jikinge chukua mipira 20 ndio wale wanaomwambia fanya zinaa zaidi na wakati tunaambiwa la "*takrabul zinaa"*.

Sasa kuna mambo haya Mhe. Mwenyekiti, kwa utamaduni wetu *is very sensitive issue.* Sasa huwezi kuwa na *problem* isiyokuwa na *solution,* halafu unatizama *what is next* kwamba ninamshauri Mhe. Waziri katika Wizara yake masuala yote haya yanahitaji mashirikiano na Wizara zote zilizohusika. Kuna Wizara ya Kilimo, Wizara ya Ardhi, Jeshi la Polisi, yote haya huweza kufanikisha hili si la mtu mmoja Mhe. Mwenyekiti, wala si la wizara moja. Maana ukisema wizara hii haina sheria ya kusema twende tukavamie bila ya kuwa na sehemu zinazohusika katika sheria yetu ya Katiba, maana nchi hii tunaongozwa na sheria. Sasa lazima tutizame sheria zetu kama kunataka kufanywa marekebisho yafanywe marekebisho kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar sio kundi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie hapa kwa leo kutoa ushauri katika masuala mazima haya ambayo yanamgusa kila

binadamu. Lakini kuna mambo mengine tukiyafumbia macho, tukisema urafiki katika nchi, ujirani mwema yatatuumiza hayo na tutakuwa siku zote tunakuja na bajeti tunatumia, Wizara zinatenga pesa za mchanga, majanga yanaendelea hatufiki huko tunakofika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie hapa niishukuru Wizara inayohusika kwa ushauri nilioutoa na ninafikiri tukimuomba Mwenyezi Mungu tutafika. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi fursa ya kuweza kutoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijaalia na mimi afya njema na uhai wake nikaweza kusimama hapa mbele ya Baraza hili. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushukuru na wewe pia kwa kunipa fursa hii lakini pia nichukue fursa hii kuishukuru Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais, pamoja na waziri wake lakini pia na watendaji wake wote kwa kubeba mzigo huu mkubwa katika kushughulikia Wizara hii na mambo mazito yaliyomo katika Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kuwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba vina ardhi ndogo lakini vina eneo kubwa la bahari. Sasa kwa mantiki hiyo Mhe. Waziri umakini unahitajika sana katika kuhakikisha kuwa hakuna uchafuzi wa mazingira katika maeneo yote mawili.

Mhe. Mwenyekiti, kulijitokeza tatizo moja ambalo kuwa Ofisi pia inahitajika kupata pongezi ya kuweza kulichukulia hatua tatizo hili la kuzuia misumeno ya moto. Hili limekuwa ni tatizo kubwa ambalo ni moja linalosababisha uharibifu wa mazingira katika maeneo yetu ya visiwa hivi. Kwa hivyo nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na Ofisi yake na kuliweza kuliona hili na hatimaye wakaweza kulishughulikia na likafikia hatua nzuri. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninamuomba aongeze juhudi ya kuwa pale tunapofikia basi tusiweze kurudi nyuma.

Lakini Mhe. Waziri jengine katika suala zima la mazingira katika maeneo yote ambayo kuwa wananchi wengi wanajitafutia riziki hasa katika maeneo ya vijijini katika mabonde haya ya mpunga. Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo linaenea sana na linasababishwa na uchafuaji wa mazingira pia kwa ajili ya watu kukata miti ile iliyomo pembezoni mwa bahari na hatimae kuiruhusu chumvi kuingia katika mabonde hayo. Mheshimiwa hili ni tatizo hasa katika maeneo yetu ya vijijini wanaolima katika mabonde haya kwa asilimia kubwa huwa wanapoteza nguvu zao zilizokuwa hazina tija. Ingawa Mhe. Waziri juhudi zinachukuliwa na serikali lakini pia na wahisani miradi mbali mbali

lakini bado limekuwa ni tatizo la maeneo ya mabonde haya kuingia chumvi na hatimae kupelekea usumbufu mkubwa kwa wakulima hawa.

Mhe. Mwenyekiti, maeneo ambayo kwa mimi ninayajua tu basi maeneo ya Tumbe, Wingwi, Gando humo yamo mabonde lakini pia Micheweni kuna bonde ambalo limejengwa tuta lakini bado halijamalizika sijui tatizo ni kitu gani. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuombe Mhe. Waziri katika Jimbo lile la Tume basi mabonde mengi kwa sababu tupo pembezoni mwa bahari yana matatizo haya. Kwanza ni Kwamwanasoza halafu kuna bonde moja Kwa Mzibua lakini kuna bonde jengine kwa Mane Mmadi pia bonde jengine kwa Kowa Kinowe huko, lakini mpaka kwa Pape hayo ni mabonde ambayo yameathirika sana na chumvi. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba katika suala hili ombi langu kwa Mhe. Waziri kuna pesa huku katika kitabu chako *paragraph* ya 126 hitimisho, kuna pesa zisizopungua milioni 800. Kwa hivyo Waziri ningekuomba sana kuhusu hili na matatizo ya mabonde haya basi fedha hizi ungeangalia ikiwezekana kuyaona haya mabonde na kuyapatia ufumbuzi ijapokuwa si yote, lakini japo moja au mawili ili hili suala liweze kuendelezwa na hawa wananchi wetu wanapotumia nguvu zao wapate mahitaji na wao.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumzie kwenye suala la watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu na wao wana haki kama watu wengine na serikali inapiga kelele sana kuhusu suala hili lakini sasa hufika pahala tukajiuliza kuhusu hii miundombinu ya majengo, jee, serikali wanalimudu hili kwa sababu ukiangalia ofisi nyingi za serikali ni majengo ya kurithi. Bado tuko nyuma katika majengo ambayo kuwa tunategemea ni ya kisasa. Lakini hata hayo yaliyoko hivi sasa bado hayaelekezi miundombinu ya watu wenye ulemavu. Kwa hivyo hili ni tatizo mheshimiwa na sasa Ofisi zetu zote kama ninavyosema ni kuwa ni Ofisi zile kongwe za kurithi na Ofisi hiyo moja utakuta mna Wizara pengine mbili. Sasa tunataka mambo tuyarekebishe au tuyatengeze lakini tukijiangalia sisi wenyewe bado hatuna muelekeo mzuri.

Ofisi nyingi Mhe. Waziri zimo katika majengo ya kurithi yaliyokuwa yana ngazi karibuni sijui ngapi. Sasa kufikia watu wenye ulemavu katika majengo hayo bado ni tatizo lakini ndio hayo yanayozungumzwa hasa katika majengo mapya hayazingatiwi hayo. Sasa ni maeneo ya kusema kwenye vitabu, maneno mazuri ya kupendeza lakini hatimae ukizunguka ukifanya utafiti hakuna kinachoongezeka. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hilo ni tatizo.

Jengine Mhe. Waziri hii Tume ya Kuratibu na Kudhibiti dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni visiwa lakini na hili jambo bado serikali hawajawa na umakini nalo, kwa sababu walipotaka kudhibiti magendo ya karafuu walifunga ukanda. Jinsi ya bandari nyingi zilizopo lakini

walihakikisha kwamba karafuu kwa asilimia kubwa haitoki Zanzibar. Hili lilikuwa ni tatizo lisilopata ufumbuzi, siku zote madawa ya kulevya na ukiangalia bado madawa yanaingizwa. Kwa hivyo Mhe. Waziri na juhudi zako unazozifanya lakini bado kuna tatizo la uingizaji wa madawa ya kulevya na hii itakuwa ni historia.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumzie kuhusu Tume ya Ukimwi. Mhe. Mwenyekiti, nalo hili pia ni tatizo na fedha nyingi kama walivyosema wachangiaji wengi kuwa zinakwenda katika mawizara, lakini hatma yake ukija kusikia takwimu ya masuala haya basi sijui unahisi utafanya nini linalofanywa. Kwa sababu kila Wizara kuna fungu ambalo kuwa linashughulikia masuala ya Ukimwi lakini katika ukurasa huu Mhe. Waziri kaandika hapa kuwa Tume ya Ukimwi kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilipangiwa malengo yafuatayo:

"Kuimarisha mazingira mazuri ya wafanyakazi wa Tume kwa ajili ya kuleta ufanisi katika shughuli za uratibu na masuala ya Ukimwi".

Hili ndio linaloshamiri, Mhe. Waziri ndilo wanalojengea mazingira mazuri watendaji wa serikali kwa sababu ukenda kwenye vifungu hivi ukihoji utakuta ni ufuatiliaji, ni tathmini, ni watu wa Wizara kupewa mafunzo kujikinga na maambukizo ya ukimwi. Sasa hili tunalolitafuta au tunatafuta kitu gani. Kwa hivyo Mhe. Waziri katika suala hili la Ukimwi bado hatujalipatia ufumbuzi tutaendeleo kuchukua pesa tukiziingiza kila Wizara hatimae zinazofaidika ni wizara zile lakini matokeo halisi hayaoneshi kupungua kwa tatizo hili. Sasa Mhe. Waziri pamoja na fedha nyingi zinazokwenda kwenye maeneo haya lakini kuna haja ya kuona nini kinachotudhuru, tatizo ni nini hasa linalotuathiri katika masuala haya tujiulize. Lakini tusichukue pesa au ni bora hizi pesa ziondolewe hasa kwenye hizi Wizara kwa sababu hatuoni kazi inayofanyika.

Kwa sababu hapa kasema kuimarisha, uratibu na utekelezaji wa sera ya sheria na mkakati wa taifa wa pili na ufuatiliaji tathmini na utafiti katika program za ukimwi. Sasa hii ndio mantiki ya kuchukua hizi pesa tukizipeleka tu. Sisi juzi kwenye kamati yetu tuliwashauri liondolewe hili fungu katika mawizara halina kazi, kwa sababu ingelikuwa angalau kunafanywa jambo hatimae tukaona matokeo mazuri. Lakini sasa kunafanywa jambo pesa kuzipeleka maeneo mengi yapo ya kupeleka hazipelekwi linakwenda kutafutwa suala hili, zinapelekwa pesa hatimae matokeo hatuyaoni.

Mhe. Waziri kwa suala hili mimi ningeomba hivi vifungu viliomo katika mawizara vya fungu hili la ukimwi tusivipitishe havina faida yoyote na hasa hivi tunavyolichukulia hili suala la matatizo haya ya ukimwi. Kwa sababu

Mhe. Waziri hakuna maradhi mazuri yanayompata binadamu ikabidi ayaone kuwa haya ni maradhi mazuri yote ni maradhi mabaya. Lakini sasa suala hili linavyochukuliwa la ukimwi linavyotiwa kipa umbele ukisema unamnyanyapaa, ukizungumza hivi usifanye hivyo, lakini kumbe kuna maradhi chungunzima watu wanatengwa lakini hawakuonekana limeonekana suala hili kwa sababu ni chumio la watu.Mhe. Waziri ninakuomba sana na wajumbe wenzangu jamani tuangalieni hali halisi ilivyo haya masuala hayatusaidii kitu.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema naunga mkono hoja kwa asilimia mia.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu mfupi sana kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambayo ameiwasilisha mapema leo asubuhi.

Mhe. Mwenyekiti niombe niseme tu kwamba si tatizo kutamka kwamba naunga mkono hotuba hii lakini unapotamka lazima uwe na sababu ya kutamka. Si vyema kutamka jambo ambalo ndani ya roho yako hamna imani hiyo. Kwa hivyo mimi niungane na Mhe. Jussa kwamba siungi mkono hii hotuba, kwa sababu nikisema ninaiunga mkono nitajisuta nafsi yangu. Siungi mkono kwa sababu ambazo nimeziona mpaka Waziri ambapo atanipa maelezo mimi nitaunga mkono na akishindwa kunipa maelezo ya kutosha basi si vibaya mtu kumtoa mwanawe kikoa nitamminya mwanzo leo ili aone kwamba mimi siungi mkono hii hotuba.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwenya mafungu wenzangu wamezungumza na si vibaya kurejea rejea lakini kuna fungu ambalo nataka nisisitize kwamba kwanza Afisi Kuu Pemba kuna kasma 220508 ununuzi wa magazeti. Mwaka jana bajeti iliyopita Wizara ilituomba shs.1,168,000 na tukawaidhinishia mara hii hawakuomba kitu. Sasa nauliza ile haja ya magazeti Pemba imemalizika au yale ya mwaka jana hayana maana tena au mara hii mtapewa bure, maana yake mara hii hamna gazeti hata moja mtasoma nini tujue mmeomba ziro hapa mara hii.

Kasma ya pili 220509 ada ya ushauri wa kitaalamu. Mwaka jana ushauri wa kitaalamu ilikuwa ziro mara hii mmetuomba milioni 29.3 kipi ambacho mwaka jana hamkushauriwa vyema Pemba, mara hii mmetuomba milioni 29.3 ili tuwape mshauriwe. Naomba Mhe. Waziri utueleze kasma hiyo.

Kasma ya tatu 220517 uimarishaji wa mpango wa bajeti, mwaka jana mlituomba milioni 45.4, mara hii mmeomba milioni 15.5 jee, mwaka huu

ambao unakuja keshokutwa kuanzia Julai 1, hamna tena shida ya kuandaa mpango wa bajeti hapa mkapunguza fungu. Mwaka jana milioni 45 au utaalamu ushaingia vichwani, kwa hivyo hamna haja tena ya kuitafuta nyingi. Mhe. Mwenyekiti, fungu jengine 211101 hii ni Idara ya Uendeshaji na Utumishi, wenzangu wamezungumza lakini ukiangalia fedha ambazo zimetengwa miaka 3 ni milioni 622.4, mwaka huu tunaokwenda 2013/2014 zimetangwa milioni 663 ni ongezeko la milioni 40.6, maana yake miaka 3 mfululizo imezidiwa na mwaka mmoja kwa milioni 40.6. Hii ina maana kwamba kwanza itakuwa mmeajiri waajiriwa wengi, mtakuwa mna lengo la kuajiri waajiriwa wengi ama mnakusudia kuajiri waajiriwa wataalamu zaidi ambao sio wale machapa.

Maana yake serikali ina waajiriwa wengine machapa, kuna waajiriwa wengine ambao faida yake ndogo. Utwambie sasa jee, umeongeza fungu hili mara tatu kwa maana kwamba unaajiri waajiriwa wengi ama umeamua kuajiri waajiriwa wenye kiwango kikubwa cha elimu. Naomba utupe maelezo kwa sababu umeongeza fedha kutoka mwaka jana kwa milioni 427, maana yake mwaka jana ilikuwa mia mbili na kidogo, mara hii wametiwa 634. Sasa twambie lengo nini kwamba kuna waajiriwa wapya wataongezwa wengi au ndio zile bilioni 17.5 zimetengwa kwa ajira watu wanagawana gawana ili zimalizike. Kwa hivyo mimi ningefurahi kama tunaambiwa utaajiri wapya ambao si machapa, sio wale mpaka umwandikie ndio akafanye kazi. Sasa twambie Mhe. Waziri ili fungu hili niweze kuliruhusu.

Vile vile sambamba na wenzangu wamesema maposho maana yake ukiongeza ajira maana yake unaongeza na maposho, maposho yamepanda kwa milioni 200. Mwaka jana ilikuwa milioni 107, mara hii zimetiwa 307.7 umezidisha milioni 200. Hii ni wastani milioni 16.7 kwa mwezi posho la Idara hii moja. Sasa utwambie Mhe.Waziri vile vile kwa nini umeongeza fungu hilo.

Mhe. Mwenyekiti Idara nyengine ambayo ninataka nihoji vifungu ni Idara ya Watu Wenye Ulemavu kasma 220504 mwaka jana uliweka 510,000 vifaa vya komputa. Mara hii umeweka milioni 35.9, sasa naomba kujua tu maana yake imepanda karibu asilimia nyingi sana. Sasa kwa nini mwaka jana ilikuwa 510,000 mara hii milioni 35.9 ni vifaa vya kompyuta au ni kompyuta halisi, sasa naomba Mhe. Waziri hiyo utuelezee.

Kasma nyengine Idara ya Ulemavu ni 263129 huduma za watu wenye ulemavu, naomba nijue ni zipi kwanza, maana yake mimi Mhe. Mwenyekiti, ni mwanachama wa walemavu kadi yangi ni 384. Sasa mnahudumia vipi watu wazima hamna au Unguja hakuna Pemba hakuna sasa ni huduma zipi. Mwaka jana mlituomba milioni 373.5, mara hii mmetenga milioni 255.02, sasa hizi huduma zimepungua au vipi, maana yake hatuelewi ni kizungu mkuti tu na

wanapewa nani, au walemavu wamepungua mshaonyoosha viungo au wamefariki au vipi. Maana yake kuna mradi wa kunyoosha viungo pengine mshapunguza viungo vyengine mshanyoosha, sasa mtwambie mmepunguza pesa kwa sababu walemavu wamepungua, mmepunguza na mnatoa huduma gani tuzijue.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nasema nazuia shilingi kwenye Ofisi ya Faragha kidogo utashangaa kwa sababu ni Ofisi ya mtu mkubwa lazima nizuie, kwa sababu sijaridhika na sababu ambazo wameeleza mpaka utaponitosheleza. Ofisi hizi tatu za Mhe. Rais, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais ningesemea zingelingana kwenye mafungu ya faragha.

Kwa mfano, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais mwaka jana ilitengewa milioni 365.2, mara hii imeombewa milioni 780.03 ongezeko la milioni 414, hiyo ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Tumeongeza mara mbili ya fungu la mwaka jana, kwa maana mahitajio yameongezeka. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais mwaka jana milioni 511.3, mara hii 515.2 tumeongeza milioni 3.8. Sasa maana yake nini, maana yake Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hakuna ongezeko la gharama kama mwaka jana alikula *panadol* mbili na mara hii ale mbili, sasa twambie kigezo nini. Ili nipitishe vifungu hivi nisizue maana kuzuia sio kuongezeka tu na kupungua vile vile ni sababu. Kwa hivyo twambie kigezo nini, kwa nini Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais zimeongezeka milioni 414 ya Makamu wa Kwanza wa Rais zimeongezewa milioni 3.4. Sasa yeye hasafiri sana, yeye hapandi ndege za Serikali, hupanda hizi *charter* za kina ndugu yangu Raza au hupanda zipi, sasa twambie maelezo turidhike au pengine hakuna huduma nyengine za msingi au wafanyakazi wake ni wachache atupe maelezo, maana yake naona hili fungu limeshuka sana tofauti na mafungu mawili ya faragha ambayo yamepanda mara nne ya fedha za mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametuelezea suala zima la ghafla ya chakula cha usiku cha walemavu kwa wawakilishi walishawishiwa hapa na kamati ikaundwa mimi bahati mpaka sikuwahi kuhudhuria, lakini nakumbuka mchango nilitoa. Sasa hebu tusaidie kwanza ahadi ilikuwa milioni ngapi ziweke wazi. Hao waliokuja kwenye chakula cha usiku waliahidi milioni ngapi na hadi leo ulipotwambia kwamba zimepatikana milioni 158.2 bado ngapi ambazo hazijapatikana hadi mwaka huu unamalizika. Lakini pia nijue kwamba ziko kwenye usimamizi wa nani wa Idara yenyewe ya walemavu au ziko kwenye fungu kubwa la Wizara, baadae fungu la Wizara mnachota mnawatumia walemavu na usalama wake ukoje. Kwa sababu nimeshtuka na ile hoja ya Mhe. Jussa ambayo pia nitaielezea na hasa kwa sababu mimi mweyewe ni mlemavu ningependa kujua kwamba hii fedha na niliwahi kusema mwaka jana Mwenyekiti, hapa kwamba Zanzibar kila kitu *deal*. Hapa

ukiumwa ni mtaji wa watu, ukifariki ni mtaji wa watu, ukigongwa na gari mtaji wa watu. Nilisema mwaka jana, kama hapa kila *deal*, maana yake mtu anaomba mmoja awe mlemavu yeye apate kijio, lakini tatizo kuna watu humu wakisema wanaonekana wanaropoka tu, tunasema kwa hoja, hapa ukiangukiwa na mnazi ni biashara ya mtu, maana utapelekwa Wizara ya Afya, ikisha upelekwe India ni biashara ya watu.

Mhe. Mwenyekiti, jana alipelekwa Sheha wa Tomondo India Mwenyezi Mungu amjaalie apone arudi salama lakini nina hakika ni biashara ya watu, ndiyo tunavyokwenda. Kwa hivyo yule Sheha alipoumia yeye kaumia lakini watapata kijio watu pale pale, kwamba milioni kumi matibabu tuweke hamsini, ni tatizo la Zanzibar na tumesema mara nyingi haya lakini tukisema ndio utaonekana mtu mgonjwa au mwendawazimu. Sisi tuko makini sana na tunaumwa na hizi fedha za watu. Kwa hivyo kama tukigonjwa ndio mtaji wa watu kwa kweli mtatajirika sana kwa sababu wagonjwa wanaongezeka, walemavu wanaongezeka sana, lakini kwa nini iwe hivi, kwamba mwenzako apate mtihani wewe ndio uwe mtaji wako.

Mhe. Mwenyekiti, ninaomba mimi niongezee kwa nini mmetumia dawa naambiwa boksi nne tu kwa milioni kumi na sita. Ninavyokumbuka kama sijakosea hili fungu lilikuwa zaidi ya milioni mia tatu, je mlishindwa kutumia hata ikawa hivi sasa hamna pakutumia mkanunue dawa ambazo hazihitajiki na nani aliyewaambia kwamba wagonjwa wa akili wanataka dawa. Kwa sababu sisi tulipanga fedha kwenye Wizara ya Afya kwa ajili ya wagonjwa wa akili, nani aliyewaambia mkawaonee huruma wale, kwa nini msitafute vifaa vya viungo mkawapa walemavu, kwa nini msiwapelekee *sober house* fedha, lakini ni kwa sababu ya *deal*. Kwa hivyo Mhe. Waziri kwa heshima kubwa naomba turidhike utwambie uzembe huu nani kaufanya, kama wewe umegundua, kama Katibu Mkuu amegundua na mmetoa taarifa na jana Makamu wa Pili alisema kuna Waziri ambaye amempa taarifa baada ya kufanya utafiti ni wewe uliyempa taarifa, Serikali imechukua hatua gani au tena baada ya taarifa ndio yamekwisha. Kama ni hivyo basi narejea tukomeleeni kule benki baadae mtuachilie tuondoke, maana hapana *impact* yoyote ile. Maana kama kuiba baadae dawa yake ni kuondoshwa pahala basi tukomelee benki, mimi nipeleke *NMB*, mwenzangu mpeleke *PBZ*, mwenzangu mpaleke *BARCLAYS*, baadae mutuondoshe mutuambie haya ondokeni kimbieni, tutakimbia.

Mhe. Mwenyekiti, tusionekana sisi Wawakilishi kama wagonjwa hivi au wendawazimu. Kama kusema tumesema sana kwamba watu wanadhalilishwa, wanaonewa lakini ukisema unaonekana kama unajenga mtoni, lakini lazima tuseme kweli kwamba maneno tumezungumza mengi sana na maneno kama

tunayozungumza mnayafanyia kazi au Serikali inayafanyia kazi hapa leo tusingefika.

Mhe. Mwenyekiti, fedha za umma zinapotea kiholela sana. Mimi naomba nipate maelezo kama *Accounting Officer* wa Wizara hii au Katibu Mkuu amegundua uoza huo, kama Waziri mwenye dhamana amegundua pia uoza huo, nini sasa hatua itakayofuata na kwa nini mara hii tuwatilie fedha ambazo hamuendi kuzitumia. Maana yake hamukutumia mpaka munakamata kamata tu, boksi nne ukifungua pengine ukifungua humo mna panya hamna dawa mashaka tu. Kwa hivyo kwa nini mara hii zitengwe fedha wakati mmeshindwa kutumia mwaka mzima.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwa uchungu kwa sababu mambo mengine watu wazima hayazungumzwi hadharani lakini inabidi tuseme. Ofisi kama hii sasa watu wanafanya *deal* na Ofisi kama hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais na Ofisi ya Rais ikifanyika uzembe au wizi ni sura mbaya ambayo haipendezi, kama ni ofisi za watu wengine wache wafanye mambo watakavyo lakini hizi ofisi tatu hizi ukifanya wizi au ukifanya uzembe inakuwa ni aibu kubwa. Mimi ninaomba maelezo katika hilo na hasa kwa vile imewagusa walemavu sitapitisha bajeti hii mpaka nipate maelezo, na ukishindwa kumtaja yule aliyefanya uzembe sitakutajia, maana tatizo lenu mnashindwa kutaja na niliwaambia hii Zanzibar haina siri, hii ukizungumza sasa hivi nyumbani kwangu basi kesho asubuhi Mhe. Jussa anajua, ni nchi ndogo sana, mitandao imejaa, usiku mmoja *website* inafanya kazi nchi nzima hii, kuna hili kuna hili na kuna hili. Kwa hivyo ukificha sisi tutakwambia kwamba huyu ndiye aliyeharibu na hichi ndicho alichokiharibu.

Mhe. Mweyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba mwaka jana nilisema kwamba tusitenge fedha kwenye Tume ya Ukimwi kwa sababu haina maana. Mhe. Waziri, nimechukua *hansard* hapa alisema mambo mengi tu sana matamu na ndio maana Marekani wakaona huyu jamaa alete ukimwi tumpe nishani, pengine. Nilisema kwa mdomo wangu kwamba haina maana, watu gharama yao ni kuchapisha bango, Madungu, Kengeja, Muwambe, Chaani, Matemwe kuhusu ukimwi, ndio hiyo tu na hiyo ukimpa mtaalamu mzuri wa kuchora atakuchoroe mabango mia siku moja. Kwa hiyo mnatoa bilioni nne kwa mabango tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitawashangaa sana Wawakilishi wa Baraza hili waliopewa dhamana na Wazanzibari milioni moja na nusu tulivyoambia ingawa mimi siamini vizuri, wakaamua kupitisha kwa fungu hili, hakuna faida, maana kama mipira ya *condom* wanaonunua ni wafanyabiashara wenyewe sijaona mimi Serikali kugawa, labda siku ya mwenge na sisi wengine hatuendi kwenye mwenge wala hatutumii *condom.* Sasa nadhani

Mhe. Mwenyekiti, hatuna sababu ya kuja kutenga fedha kuwapa watu watajirike, fedha hizi ambazo zimekuja kwa masuala ya ukimwi kila mtu ameshajua kwamba ukimwi ni janga na unauwa na una hatari, fedha hizi tuzichukue tuzipeleke hospitali, tupeleke makulini na sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niwaombe sana Wawakilishi na Mhe. Waziri, nikuombe sana mwaka jana ulinipa maneno makubwa nikasema kwa maneno haya Ijumaa haifiki tutafanikiwa. Mimi nakuomba mara hii ukubali kwamba usitumie fedha nyingi kama Idara inakufa na ife na hasa kwa vile jana tuliambiwa kwamba Mratibu wa Ukimwi ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na zimetengwa milioni 52,000,000/= kwa kazi hii tu ya kuratibu. Kwa hivyo kama kuratibu basi ratibuni kule baadae mtuambie kuna wagonjwa wangapi na wangapi wamekufa lakini fedha tuitoe tupeleke sehemu nyengine ili wananchi wapate maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, tunasema haya si kwa nia mbaya kwa sababu hatuoni faida. Mimi sidhani kwamba hizi fedha zinawafika, naamini haziwafiki fedha. Sasa Mhe. Waziri tukubalie kwamba hii fedha tuitoe tubakishe mishahara tu, kwa sababu mishahara tutawapa hao wenzetu na mutazigawa sehemu nyengine watafanya kazi, lakini tusizipeleke sehemu ambayo sasa watu wanatajirika kwa mgongo wa watu, nyie jamani mtasuhiri tugongwe tu watu watajirike mpaka lini.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba mazingira kwa Pemba ukiacha huwezi kutengeneza barabara wala gati kama hujazungumza Vitongoji, Muambe na Micheweni. Mhe. Waziri nikushukuru sana wewe na Katibu Mkuu kwamba mmekuja na mmeona hali ya Muambe, lakini hatuoni faida ya Idara yako ya Mazingira. Kwa nini hatuoni kwa sababu fedha nadhani ambazo mnazitengea Idara ya Mazingira ni ndogo. Sasa badala ya kuwapa watu wa Ukimwi wakatudaganya nadhani hii fedha watengewe mazingira wafanye kazi ili wananchi waweze kulima, bahari katika maeneo ya Muambe na Kengeja tayari inapanda juu, Idara ya Mazingira hawana nyenzo. Kwa hiyo baadae watamlaumu Mkurugenzi wa Mazingira na Katibu Mkuu kila siku wakati hakuna fedha. Kwa hivyo mimi nashauri kwamba fedha hii ya Ukimwi tuihaulishe tuipeleke Idara ya Mazingira ili wenzetu wafanye kazi wananchi wapate maeneo ya kulima.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo kwa sauti kubwa na kwa nia safi siungi mkono hotuba hii mpaka nipate maelezo ya kina ambayo Mhe. Waziri atakayatoa.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa. Pia ninamuomba aniwezeshe

kuzungumza nililolikusudia. Vile vile namshukuru kwa kukumbusha kama na mimi nipe na ukanipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi naomba nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad kwa namna anavyoisimamia ofisi yake, pia nampongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais, kwa ujasiri wake anaouonesha katika kumsaidia Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais katika majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitakuwa na mchango mkubwa ila nimesimama hapa kutoa baraka ya bajeti hii. Katika kufanya jukumu hilo naomba nimpongeze Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais kusimamia uangamizaji wa kunguru weusi. Mhe. Mwenyekiti, hili ni kero kubwa naomba nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, kwani siku zote hapa tunazungumzia kero za muungano lakini na kunguru hawa wamekuwa ni kero mno, imekuwa ni adha kubwa Mhe. Mwenyekiti, kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 14 Mhe. Waziri amesema kwamba amemudu kuangamiza kunguru kama elfu kumi. Suala langu kwa Mhe. Waziri Serikali imekusudia kuangamiza wangapi na hao elfu kumi walioangamizwa Serikali imefikia lengo la asilimia ngapi, na suala langu jengine ambalo namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ni sababu zipi za msingi zilizopelekea mradi huu kuhamishwa katika Wizara yake na kupelekwa katika Wizara ya Kilimo na Maliasili na jee ni ufanisi gani unaotarajiwa kupatikana katika Wizara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kiambatanisho nambari 1 ukurasa wa 48 Wizara yako Mhe. Waziri imejitahidi sana kusomesha wafanyakazi 20 kwa mwaka huu unaomalizika. Hili ni jambo zuri Mhe. Mwenyekiti, lakini majukumu makubwa ya Wizara hii ni kudhibiti masuala ya ukimwi, madawa ya kulevya, mazingira na pia kusimamia shughuli za walemavu. Sasa suala langu Mhe. Mwenyekiti, hawa wanafunzi 20 waliosomeshwa mwaka huu uliomalizika hawakusomeshwa hakuna hata mfanyakazi mmoja aliyesomeshwa ama kudhibiti ukimwi, dawa za kulevya, mazingira, sasa sijui Mhe. Waziri ufanisi wa Wizara yako utakapatikana vipi wakati mafunzo waliosomeshwa hayaoani na majukumu ya Wizara yako.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika ukurasa wa 68 kuna kiambatanisho nambari 11, kinachohusu mgao wa fedha za matumizi kwa mwaka 2013/14.Mhe. Mwenyekiti, katika mgao huo jumla ya fungu la Wizara yake ni zaidi ya shilingi bilioni tatu. Lakini la kusikitisha kilichotengwa na Ofisi Kuu Pemba ni kiasi cha shilingi milioni mia tatu na thalathini tu. Ninamuomba Mhe.

Waziri anifahamishe Ofisi Kuu Pemba haoni kwamba fedha hizi ni kidogo na je fedha hizi kidogo hakutayumbisha maendeleo ya ofisi yake Pemba. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anipe majibu mazuri hapa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kwa sababu kiswahili ni kigumu na sio wengine hatukielewi, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe katika hii rasimu ya maelezo ya bajeti inatumia programu *PBB* ukurasa wa 4, kuna kifungu nambari moja hapa Mhe. Mwenyekiti, naomba nikinukuu,

"Programu ya kwanza ni udhibiti wa dawa za kulevya ambayo dhumuni lake kubwa ni kuwepo jamii ya Wazanzibari kuwa huru na matumizi ya dawa za kulevya"

Mhe. Mwenyekiti, yaliyofuatia huku chini katika vifungu vyengine vidogo hivi dhamira yake ninaiona ni nzuri na maana yake inaonekana inaridhisha, lakini hapa aliposema kuwepo kwa jamii ya Wazanzibari kuwa huru na matumizi ya dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, nafahamu kuwa huru ni kuwa kile kitu maana yake nifanye hakuna pingamizi. Sasa namuomba Mhe. Waziri hapa aje anipe ufafanuzi.

Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, naomba niipongeze sana Ofisi hii ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa jinsi walivyoweza kupunguza unyanyapaa kwa wananchi walioathirika na pia wale watu wanaoishi na virusi kwa sababu kuna waathirika na wanaoishi na virusi. Walioathirika Mhe. Mwenyekiti, hata wale waliofiliwa na wazazi wao, hutokezea watu wakawanyanyasa watoto wale wakaambiwa pia ni waathirika ikawa hawana raha na wengine hata kuzuiwa kucheza na watoto wengine. Hivyo hapa mimi naipongeza sana ofisi hii. Vile vile nawapongeza kwa kuweza kuziunga mkono nyumba za kurekebisha tabia, naona nyumba hizi zimetusaidia sana kurejesha hali za vijana wetu ambao walikuwa tayari wameshapoteza muelekeo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nitaunga mkono hoja ya bajeti hii pale Mhe. Waziri atakaponipa jawabu nzuri hasa ya ile lugha iliyotumiwa pale ya kuwa huru na madawa ya kulevya na pili kuhusu fungu dogo la Ofisi Kuu Pemba. Nakushukuru.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Bismillahi Rahmani Rahim. Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, leo sauti haitoki vizuri kwa sababu kifua kinaniuma, jana nilikaa sana nangoja asali lakini sikuletea na Mhe. Saleh, kwa hiyo tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na dibaji. Wenzangu Waheshimiwa waliokuwa wametangulia hapa wakiongozwa na Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti na Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Serikali walizungumzia suala linalohusu Skuli ya Kisiwandui. Mimi sitaki nilizungumze hilo kwa sababu tayari limezungumzwa, lakini ninachokiomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa sababu suala lile liko tokea wakati wa Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, likafanyiwa mpaka mahesabu hili eneo ambalo linataka kurekebishwa, lakini hadi leo eneo lile halijafanyiwa kazi. Mhe. Waziri akija hapa nitamuomba anipe ahadi ni lini kadhia ile itamalizika katika Skuli ya Kisiwandui, hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nilitaka vile vile kueleweshwa juu ya suala zima la ufutaji wa hati miliki katika eneo la la Kilimani ambapo mwaka juzi ilikuwa tukilizunguza hapa na mpaka leo hii hatujapata ufafanuzi wa suala lile limefikia wapi. La tatu mwaka jana nilipokuwa ninachangia katika bajeti ya Wizara hii nilizungumzia juu ya mahitaji ya Skuli hiyo hiyo ya Kisiwandui kwa wanafunzi ambao wana mahitaji maalum, nilitaka kufahamu vile vile Mhe. Waziri wamefikia wapi katika kuliangalia suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nikishakumaliza hiyo dibaji kwa leo katika mchango wangu kwenye kitabu hichi, mimi sitaki kwenda kwenye hotuba ya Mhe. Waziri, mimi nakuja kwenye vifungu moja kwa moja. Ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe ufafanuzi wa kifungu 0301 *bullet 211104,* ninaomba ufafanuzi wa kina katika hilo. Pili *bullet 211110* pia nataka ufafanuzi kuna *figure* hapa ambazo haziendani vizuri nataka maelekezo ya ziada ili nikubaliane na kuweza kupitisha fungu hili.

Mhe. Mwenyekiti, halafu ninakwenda katika hilo hilo buku kubwa ukurasa wa 79, *bullet 220806* nataka maelezo ya ziada. Tukiondoka hapo tunakwenda ukurasa wa 80 buku kubwa pia *bullet 211108* nataka ufafanuzi vile vile, lakini pia naomba ufafanuzi *bullet 211116*. Katika ukurasa huo wa 80 namalizia kwa *bullet 220105*. Nikimaliza hapo ninakwenda kwenye ukurasa wa 81 *bullet 220509* naomba ufafanuzi, tena hapa ndio nataka ufafanuzi wa kina. Nikiondoka hapo ninaelekea ukurasa wa 82 buku kubwa bado hilo hilo naomba ufafanuzi *bullet 211110,* ukurasa pia wa 82 huo huo naomba ufafanuzi wa *bullet 212101*. Nikiondoka hapo nakuja ukurasa wa 87 buku kubwa humu ndimo mashine na zana katika *bullet 311200* naomba ufafanuzi *bullet 311202.*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nakuja ukurasa wa 91 naomba ufafanuzi katika kifungu 220500, lakini naomba ufafanuzi wa *bullet 220504*, lakini pia naomba ufafanuzi wa *bullet 220700* na *bullet* namba 220701. Na mwisho

kabisa ukurasa wa 93 naomba ufafanuzi katika *bullet* namba 211201 na ukurasa wa 94 *bullet* namba 220504.

Mhe. Mwenyekiti, kwangu mimi kwa leo yalikuwa ni hayo, baada ya maelekezo hayo sitaunga mkono hoja mpaka nipewe maelekezo yatayayoniridhisha juu ya mambo yangu ambayo nataka ufafanuzi. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nakuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo katika majukumu yetu ya utekelezaji wa shughuli zetu za kitaifa. Lakini pia nachukua nafasi ya kukushukuru wewe Mwenyekiti kunipa nafasi hii angalau na mimi kutoa mchango wangu mfupi katika hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote juu ya kupanga hotuba hii vizuri na kwa ufanisi na uwasilishaji wake uliokuwa mzuri vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nitaanzia kwenye kitengo cha Ukimwi. Maradhi ya ukimwi ni ugonjwa hatari sana, ni ugonjwa ambao unapoteza nguvu kazi ya taifa. Vijana wengi wanaangamia katika gonjwa hili hatari, gonjwa hili thakili, gonjwa hili baya na vijana wanasema kwamba kwa kweli ukimwi umekaa pabaya, kama ingelikuwa katika ubwabwa basi labda wangeweza kuuwacha. Kwa hivyo Mhe. Waziri una kazi ngumu ya kuweza kuwaelimisha vijana wetu wakasamehe hapo ulipo ukimwi wakaendelea na ubwabwa.

Mhe. Mwenyekiti, inasemekana kwamba ukimwi miongoni mwa maambukizo makubwa ni makundi ya wanaume kwa wanaume ambao wanafanya ulawiti, wanafanya mapenzi jinsia moja. Mhe. Waziri hii ni hatari lakini vile vile ukimwi unaenea kwa kasi katika makahaba wanaojiuza, lakini vile vile na wale wanaojidunga shindano. Je, Mhe. Waziri una mikakati gani juu ya kutoa taaluma ya hali ya juu kabisa juu ya makundi haya ya hatari mbali ya hatari yao binafsi, ni hatari hata ya nchi nzima. Mhe. Waziri una kazi ngumu pamoja na ujasiri ulionao basi unatakiwa uendeleze ujasiri ziada juu ya kupambana na vikundi hatari katika nchi yetu ambavyo vinaeneza ukimwi kwa asilimia kubwa. Niache hapo katika ukimwi kwa sababu muda unakwenda haraka haraka na mimi labda nitakuwa mchangiaji wa mwisho niende katika uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu ya Zanzibar hivi sasa imekuwa ni mfano wa jangwa, tunakata miti ovyo bila ya kujali kwamba ukataji wa miti ni hatari ni athari ya visiwa vyetu vya Zanzibar. Visiwa vyetu ni visiwa vya ardhi ya kijani vyenye kuota miti mingi lakini bila ya huruma, miti hii tunaikata. Mhe.

Mwenyekiti, ukataji wa miti ni athari kubwa Mwenyezi Mungu kabla hajatuleta sisi wanadamu hapa duniani alipopenda tu kutuleta hapa duniani na akaiumba ardhi hii basi aliijaza miti ili tuje tustarehe tufaidike tupate virutubisho na hewa nzuri kwa miti hiyo. Lakini hivi sasa inaonekana kwamba suala hili tumeliweka kando na miti tunaikata ovyo bila ya kujali. Mhe. Waziri una kazi kubwa ya kutoa taaluma kwa wananchi wa Zanzibar ili kurejesha hadhi ya visiwa vya Zanzibar, kuirejesha miti iliyokuwepo na kupanda miti mipya ili kuendelea kufaidika na miti hii kupata virutubisho pamoja na hewa iliyo nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba upandaji wa miti ni kitu muhimu sana, kulikuwa na miti kadhaa hapa Zanzibar ambayo ilikuwa inaonekana katika baadhi ya miji na vijiji, hivi sasa miti hii imekuwa adimu kama vile mivule. Mhe. Mwenyekiti, kuna miti aina kwa aina ambayo ilikuwepo Zanzibar hivi sasa haipo na kuwepo kwake labda kama ipo basi ni kwa asilimia ndogo sana. Sasa basi kwa kuwa kuna vikundi vinavyohifadhi mazingira na vinapanda miti Mhe. Waziri una mpango gani wa kuviwezesha vikundi hivi ili vikaondolewa kupanda miti na kuieneza katika miji yetu. Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka niende katika dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, dawa za kulevya ni tatizo, taifa linaangamia, vijana wetu wengi wanajishughulisha na dawa za kulevya dawa ambazo kila siku tunapiga makelele wala hatupati ufumbuzi wa kulitatua tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti, taifa letu na taifa lolote linahitaji watu wenye elimu, linahitaji watu wenye nguvu linahitaji watu wachapa kazi, linahitaji watu wenye mawazo na busara. Lakini Mhe. Mwenyekiti, vijana wanaingia katika dawa za kulevya watapatikana wapi watu wenye elimu, wenye nguvu, wachapa kazi na wenye mawazo na busara. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ana kazi pevu, wizara yake pamoja na wananchi wote kwa jumla tuna kazi ya kuvilea vizazi vyetu katika utamaduni wetu wa asili wa Uzanzibari ili kuepukana na suala zima la dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, dawa za kulevya kwa kweli ni hatari, kutokana na hatari hii basi serikali inapaswa kwa nguvu zote isimamie masuala mazima ya kupinga uingizwaji wa dawa za kulevya hapa Zanzibar. Mhe. Ismail Jussa alisema magazeti mengi hapa ya kutoka nchi mbali mbali ambayo yanaelezea hatari ya madawa ya kulevya ambayo yanaingizwa hapa Zanzibar, tufanye nini?

Mhe. Mwenyekiti, la kufanya ni kuondoa muhali ili kuwakamata na kuwaingiza katika hatia wale wenye hatia katika madawa haya ambayo yanaathiri wananchi wetu na taifa letu la kesho.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 31 wa kitabu nukta ya 86. Mhe. Mwenyekiti, hapa Mhe. Waziri nataka nimnukuu, anasema

> "Mhe. Spika, ziara ya kupitia kila wilaya ili kuyatambua mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa ajili ya kupatiwa visaidizi imefanyika, kufuatia ziara hiyo watu wenye ulemavu kutoka shehia mbali mbali walipatiwa visaidizi ili kuwarahisishia kupata mahitaji yao".

Swali, Mhe. Waziri hivi vilikuwa ni visaidizi gani, viligaiwa vipi kiwilaya zetu za Zanzibar.

Lakini nikienda katika suala la watu wenye ulemavu kuna michango mbali mbali ambayo imechangwa na wafadhili pamoja na wafanyabiashara mbali mbali hapa Zanzibar, michango hii ilikuwa ni kiasi gani na kama imeshagaiwa imegawiwa vipi.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye ulemavu ni binadamu kama binadamu mwengine isipokuwa Mwenyezi Mungu tu kwa rehema zake na si kwa jengine amewapa utaratiubu ule wa kuwa watu wenye ulemavu. Tunapaswa watu wenye ulemavu tuwalee, tuwatunze na tusiwanyanyapae kwa sababu sote ni walemavu watarajiwa. Tuna watu wangapi Mhe. Mwenyekiti, wanaondoka nyumbani wakiwa wazima kwa mambo mbali mbali yanayowafika katika safari zao, katika ziara zao wanarudi wakiwa na mguu mmoja umekatika, wanarudi wakiwa mkono mmoja umekatika na vyenginevyo. Kwa hivyo, ni juu yetu kuwalea vizuri watu wenye ulemavu na pia kuwatunza bila ya kuwanyanyapaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri kuna madarasa maalum kule Pemba, Pandani na Michakaeni. Madarasa haya ni kwa ajili ya watu wenye ulemavu. Je, Mhe. Waziri madarasa haya umewahi kuyatembelea? Na kama umeyatembelea umeyasaidia vipi walimu wanaowasomesha watu wenye ulemavu lakini pia kuwapa mahitaji watu wenye ulemavu. Nawapongeza sana walimu wa skuli hizi kwa sababu naamini kwamba wanafanya kazi ngumu na kazi ya ziada. Kwa hivyo, Mhe. Waziri kama madarasa haya unayatambua na umeshayatembelea basi naomba ufafanuzi juu ya hili na umewasaidia vipi ili kuendeleza kufanya kazi vizuri na kuwa na moyo wa kuendelea kuwasaidia watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haya machache nasema kwamba nashukuru kunipa nafasi hii na mimi angalau kutia ubani katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa zimebakia dakika sita kumaliza muda wetu, sasa kama kuna Mheshimiwa ambaye anaweza kuchangia kwa muda wa dakika sita ili tumalize basi ningeshauri tufanye hivyo. Kwa sababu kesho tunataka tumalize mchanga.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata dakika hizi sita ambazo naamini kwamba na kesho nitapewa nyengine sita tukijaaliwa na Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kutoa shukurani za dhati kabisa na pongezi kwa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa namna alivyokisoma kitabu hiki tukakifahamu na Mwenyezi Mungu amzidishie kila la kheri. Pia Mheshimiwa huyu namsifu panapotokea matatizo yoyote ya mazingira na akapelekewa taarifa anakuja kwa haraka, ikiwa gari inafika, ikiwa gari haifiki na ni waziri pekee katika Jimbo la Mtambwe ambaye kafuatilia katika jimbo langu sehemu kadhaa ambako wananchi wanapanda miti kwa kupambana na mazingira na kuona namna ya ardhi inavyomong'onyoka kutokana na tabia ya nchi ndio akaambiwa mwanamke jasiri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza tunajua Mwenyezi Mungu kaijaalia nchi hii na miti yake, watu wake, ardhi yake na kadhalika ili viumbe viweze kuishi. Miti iweze kuishi, wanyama waweze kuishi na viumbe vyengine katika ardhi kuweza kuishi. Ukiharibu sehemu yoyote ya uhai wa viumbe hawa ni sawa na kusema ndio kuharibu mazingira. Kwa hivyo, mazingira yanaweza kuharibiwa katika hewa, katika ardhi na katika maji. Kuwa na Idara hii ya kupambana na mazingira ni ujasiri mkubwa wa Mhe. Rais wetu wa kuona kuwa kuna umuhimu wa kufanya hivyo ili tuweze kuishi kwa usalama na amani.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu hii hali ya wananchi wetu tunaijua kuwa ni masikini sana na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kuwa wanajitahidi kutumia uwezo wao katika hali yoyote ya halali ili waweze kujipatia maisha. Na moja kwa bahati mbaya huwa wanashiriki kikamilifu kwa njia ambayo haiwezi kuepukika ili waweze kuishi kwa kuharibu mazingira.

Moja kati ya mazingira yanayoharibiwa sana Mhe. Mwenyekiti, ni ukataji wa miti ovyo, tunajua umuhimu wa miti, miti ndio inayosafirisha hewa chafu, miti ndio inayorutubisha ardhi na miti ndio iliyokuwa baadhi yao ni chakula chetu, bila ya miti hakuna uhai. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ni wajibu wa kila wizara kushirikiana na Mhe. Waziri kuona kuwa inawasaidia kuwaelimisha wananchi kujiepusha sana na ukataji wa miti ovyo. Si suala la kuachiwa Mhe. Waziri tu peke yake, lakini ni letu sote. Miti haimo katika wizara yake, miti

imo katika Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara hii kwa bahati mbaya ndio wale watu waliokwenda katika wizara ndio inayotoa vibali vya kukata miti. Kwa hivyo, pamoja na kuwa wanatoa kibali kwa kuongeza fedha lakini wakati ule ule wanaharibu mazingira, kwa hivyo mashirikiano ni jambo muhimu sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna mazingira yanayoharibiwa katika ardhi vile vile kwa saabu ya maisha. Kwa sababu mwanadamu hali mchanga, lakini ili ale wakati mwengine mchanga unakuwa na bei kubwa anachimbua, anauza na kadhalika kwa kujipatia maisha yake. Anayatafuta maisha kwa njia ambayo ina athari kwa upande mwengine. Lakini ardhi si wizara yake ni Wizara ya Ardhi, hivyo Wizara ya Ardhi ishirikiane kikamilifu na Mhe. Waziri kuona kwamba anamsaidia katika mazingira haya pamoja na mambo mengine yanayoelekea na hayo.

Mimi kama mwakilishi natoa wito kwa wananchi wote waone kuwa kuna umuhimu mkubwa sana wa kuhifadhi mazingira yetu. Tupunguze ukataji miti ovyo na natoa wito kwa Wizara ya Kilimo isaidie katika jimbo langu kwa sababu mtindo ulioko hivi sasa ni kuwa watu kutoka majimbo mbali mbali wanahujumu katika jimbo langu kwa kukata miti ya kujengea na kadhalika. Kinachonisikitisha ni kwamba huwa inapita pale pale Bahanasa ambapo kunakuwa na mtu wa kilimo kati yake ni kuhesabu miti iliyomo katika gari na kutoa kibali. Hili linatukera sana na kama Mhe. Waziri hakushirikiana na Mhe. Waziri wa Kilimo likaondoka mara moja, tunaweza tukafanya mpango wowote tukaonekana ni watu wabaya kwa sababu hatutokubali kabisa kuharibiwa mazingira kiasi kile.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hii wizara inakuwa na tatizo jengine kubwa kabisa ambalo ni kazi ya kupambana na UKIMWI. UKIMWI tunaujua, UKIMWI ni maradhi ambayo yakikufika unakuwa unaondokewa na kinga mwilini. UKIMWI ni maradhi hayaambukizi lakini akikupata ndio safari moja kwa moja ya akhera, ama kwa ghafla au kidogo kidogo na serikali inapoteza pesa nyingi sana kwa kutoa mafunzo, kuelekeza watu na kutoa dawa za kuongeza maisha za UKIMWI na hauwezi kuondoka UKIMWI kama hatukupambana na viashiria vya kuondoa UKIMWI ambavyo hivi ni vigumu kuzuilika.

Mhe. Mwenyekiti, tunaona nchi yetu inavyoingiliwa na watu wengi sana, utamaduni, silka zetu, mila zetu, desturi zetu zimebadilika kabisa, sasa kumeingia mambo ambayo yameharamishwa katika dini yetu na ni haya ndio yanayosababisha UKIMWI kuingia. Kuacha si rahisi kutokana na vijana wetu walivyo wakati biashara iliyopo ni ya bure kabisa.

Hii habari ya kuingia katika nchi kwa watu ovyo hata *passport* hapana si wizara yake, lakini ni wizara ya *Immigration* kadhalika. Kwa hivyo, naomba sana tusizungumze tu kuwa tunahimiza, tunafanya, kupambana na UKIMWI ni kuondoa viashiria vya UKIMWI tuone kuwa tunashirikiana na Mhe. Waziri kuhakikisha kuwa utamaduni wetu unarudi kiasili ili mambo haya yapungue kama ilivyokuwa hapo zamani.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kuchangia kuna haya madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Salim Abdalla Hamad ahsante sana lakini muda hauko na sisi. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano mazuri na utulivu wenu na sasa niahirishe kikao hadi kesho asubuhi saa tatu kamili.

(Saa 1:45 Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 26/06/2013 saa 3:00 asubuhi)